# Nipashe

Jumatatu Machi 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580174

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Serikali yalifunga kwa siku 10 daraja la Mwanza-Musoma

UKURASA 3




UKURASA 13

# Vyama vyaitumia Siku ya Wanawake kujinadi

**VYAWAKUSANYA** Dar, Mbowe agusia safari za Ikulu kwamba...*Endelea ukurasa wa 2*




Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (wapili kulia), akikata utepe kuzindua tawi la 225 la Benki ya NMB lililopo Busega mkoani Simiyu akiwa na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji (watatu kulia), Mbunge wa Busega, Raphael Chegeni na Kaimu Mkurugenzi wa benki hiyo, Ruth Zaipuna (wapili kushoto). Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## WASAFIRISHAJI WALALAMIKIA KUWAJIBIKA KWA MIZIGO

UKURASA 3

# Samia: Mikopo asilimia 4 kwa wanawake imekosa uhalisia

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** AZAM FC YAWAFUNGA WATATU MIAKA MITATU UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**

## HABARI KITAIFA




Baraza la Wanawake la Bawacha wakiwa kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vyama vyaitumia Siku ya Wanawake kujinadi

**Na Waandishi Wetu**

VYAMA kadhaa vya siasa jana vilitumia Siku ya Wanawake Diniani kwa kujinadi kwao sambamba na kufikisha ujumbe kwa wananchi.

Mikutano ya kisiasa haijaruhusiwa, na vyama vya upinzani vimekuwa vikilalamikia kutoruhusiwa kwa kuwa uchaguzi mkuu unakaribia.

Tangu kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, vyama vilizuiwa kufanya mikutano isipokuwa wawakilishi wa wananchi kama wabunge na madiwani kwenye maeneo yao pekee.

Vyama ambavyo viliitumia siku hiyo kwa kufanya makongamano, midahalo na shughuli mbalimbali ni vya Chadema na ACT-Wazalendo, ambao walikutana na wawakilishi wa wanawake kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mikutano hiyo ilihudhuriwa na wanawake na viongozi wakuu walizungumza mambo mbalimbali, ikiwa ni namna ya kufikisha ujumbe waliotarajia.

**CHADEMA: Yalilia Tume Huru**

Jana, Chadema walikuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza la Wanawake (Bawacha), ambapo mgeni rasmi Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, alisema ili uchaguzi wa mwaka huu uwe huru na wa haki lazima mabadiliko ya sheria ya uchaguzi yafanyike.

"Tumemsikia Rais akitoa ahadi ya kwamba uchaguzi wa mwaka huu utakuwa huru na wa haki sasa mimi niseme 'position' (msimamo) wa Chadema katika hili unaposema tunataka maridhiano ya kitaifa siyo maridhiano ya Mbowe na Rais John Magufuli wala sio vyama vya siasa pekee, ila wananchi wote tukifikia namna bora ya kupeleka nchi yetu mbele tukifikiria mchakato wa Katiba ambao tumeuweka pembeni," alisema Mbowe.

IKULU

Mbowe alisema yeye hakuitwa kukutana na Rais na hajui walioitwa walikwenda kuazungumzia ajenda gani, na kwamba kama kuitwa Ikulu haitaji kuitwa yeye peke yake bali ni maridhiano ya wananchi wote.

**KAULI YA DK. BASHIRU**

Kuhusu kauli iliyotolewa na Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kuwa chama hicho kinatumia dola kubaki madarakani, alisema kauli hiyo inastahili kupingwa kwa kile alichodai inaweza kuleta migawanyiko na hisia mbaya katika jamii na kumtaka kuomba radhi.

**UKIMYA WA MSAJILI WA VYAMA**

Mbowe alionyesha kushangazwa na ukimya wa Msajili wa vyama vya siasa nchini kuhusiana na vyama kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara, na kwamba suala hilo linaviweka vyama katika wakati mgumu kwa kuwa CCM ikiendelea na mikutano bila kuchukuliwa hatua.

"Hivi majuzi tumepata barua kutoka kwa ofisi ya msajili ambayo imepelekwa kwa vyama vyote vya siasa kuwa kuanzia tarehe 10 mwezi huu mpaka Aprili 10, mwaka huu kuwa anahakiki vyama vya siasa kujiridhisha kama vina sifa ya kushiriki uchaguzi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha), Halima Mdee, alisema wameandaa sera ya wanawake wa chama hicho iliyopewa jina la 'sera ya wanawake wa Tanzania' na kwamba ni chama cha kwanza kuwa na sera mahususi. "Baraza tumeandaa programu maalum ya kuwapika na kuwajengea uwezo ili kuwa imara na madhubuti na kulisongesha Taifa hili sisi tunaamini umadhubuti katika uongozi pamoja na mambo mengine unatengenezwa," alisema Mdee.

**ACT -WAZALENDO**

ACT-Wazalendo ilifanya mkutano mkuu wa uchaguzi wa Ngome ya Wanawake, na mgeni rasmi alikuwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo Bisimba.

Akizungumza na wanawake hao ambao walimkabidhi tuzo maalum kwa mchango wake katika haki za binadamu na maendeleo ya mwanamke, Bisimba alisema hakutarajia kupewa tuzo hiyo licha ya kualikwa kwa haraka na kufika, lakini walimpa tuzo hiyo kubwa yenye thamani kwake.

"Aliniomba sana Zitto Kabwe nije kuongea na wanawake wa ACT-Wazalendo. Siku kama ya leo imetokana na mapambano ya wanawake kwa kuwa wamekuwa wakipata matatizo mengi kiasi cha kuwalazimu kuinuka kupambana na kuzaa hali nzuri iliyopo kwa sasa," alisema na kuongeza:

"Mambo hayakuwa hivi miaka 40 iliyopita, kuna mabadiliko makubwa, maadhimisho ya mwaka huu tunazungumzia kuja pamoja kuzungumzia usawa wa kijinsia, nilienda Beijing na tulikutana na wanawake wa kila aina na wote shida zimefanana," alisema.

Bisimba alisema bila usawa, amani, maendeleo, na kwamba kusipokuwapo usawa hakuna amani na bila amani hakuna maendeleo.

"Wanawake wa ACT- Wazalendo wanapaswa kuhakikisha usawa kwenye uchaguzi kwa kuwa usawa si kwa wanawake na wanaume tu bali kuchagua ambaye atasimama kwa wanawake ndani na nje ya ngome ya chama hicho," alisema.

**HISTORIA YA UWT**

Alisema chama kikipata viongozi wazuri watasaidia ndani na nje ya chama kwa kuwa shida za wanawake kokote kule ni za wote.

Alisema Jumuiya ya Wanawake wa CCM (UWT) ilifanya kazi kwa ajili ya wanawake wote Tanzania chini ya uongozi wa Sophia Kawawa na walitetea sana kiasi cha wanawake waliotambulika kama vimada wakatambuliwa kisheria kuwa ni ndoa, na wasichana waliruhusiwa kwenda jeshini wakae mwaka mmoja, wafanye kazi mwaka mmoja halafu ndiyo waende chuo jambo ambalo lilikuwa gumu sana.

"Wamama wale walipambana, walikuwa hawapambanii chama, walikuwa wanapambania wanawake. Na sisi kama wanawake tungeweza kutazama matatizo yetu kama wanawake na kujivua kutoka ndani ya vyama na kukutana kama wanawake ili tuangalie shida za wanawake tuzipigie kelele zishe," alisema.

***Imeandikwa na Salome Kitomari na Enock Charles***

# Samia: Mikopo asilimia 4 kwa wanawake imekosa uhalisia

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameonyesha kutoridhishwa na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake kwa Halmashauri ya Bariadi Mjini mkoani Simiyu, kwa kuwa inaonyesha kwenye makaratasi zaidi kuliko uhalisia.

Akihutubia mamia ya wananchi katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kitaifa iliyofanyika mkoani Simiyu, kwa kauli mbiu ya 'kizazi cha usawa kwa maendeleo ya sasa na baadaye, alisema ni vyema vikahudumiwa vikundi vichache vitakavyotoa matokeo chanya kuliko kuwa na orodha ndefu.

"Nimepita kwenye banda la halmashauri ya Mji Bariadi na vikundi vipo pale vimefaidi mikopo...sikuridhishwa mikopo inavyotoka inatolewa, lakini haiwafikii vikundi, inatolewa kuweka kwenye taarifa kwamba vikundi kadhaa vimepata mikopo hii," alisema na kuongeza:

"Lengo la mikopo hii ni kumwendeleza mwanamke na kuendeleza vikundi vya wanawake, naomba tupunguze utitiri wa vikundi tushughulike na vikundi ambavyo vitatoa matokeo chanya, tushughulike navyo vizalishe ili tupate matokeo."

Alisema mikopo hiyo ni bila riba kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu, huku akiwataka wanaopewa mikopo hiyo kurejesha ili wengine wapate.

Alisema kwa miaka mitano halmashauri zimetoa mikopo ya Sh. bilioni 39.7 kwa vikundi 19,874, na kwamba ili kuongeza serikali imezielekeza benki kutoa mikopo yenye urahisi kwa wanawake nchini.

Awali, Makamu wa Rais, alitoa salamu za Rais John Magufuli kuwa alisema licha ya jitihada mbalimbali zilizofanyika bado safari ya maendeleo ya wanawake ni ndefu, na kwamba serikali inabeba jukumu la kukuza na kulinda haki za binadamu na hasa za wanawake na itaendeleza kutekeleza yale yote yaliyoanzishwa kuelekea usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake kuelekea kwenye usawa wa kijinsia.

Alisema ni muhimu kuhakikisha masuala ya usawa wa kijinsia yanazingatiwa katika mipango ya maendeleo, na kwamba nchi imekuwa mstari wa mbele kutekeleza maazimio ya Beijing.

Alisema zilizofikiwa kama nchi usawa wa kijinsia kwenye elimu na mafunzo, na kwamba elimu bure imewezesha wanafunzi kuongezeka kutoka 8,00,000 wanafunzi milioni 10.1 mwaka 2018, na udahili sekondari umeongezeka kutoka milioni 1.7 hadi milioni 1.9 mwaka 2018.

"Ni matarajio ya serikali kuwa sera ya elimu bure itaondoa tofauti ya kijinsia katika elimu baina ya mtoto wa kike na kiume, natoa wito kwa wazazi wote kuhakikisha watoto wanatumia fursa hii bila kukosa na wanaokiuka sheria ichukua mkondo wake," alisema.

Alisema serikali inatoa mikopo yenye masharti nafuu kuwawezesha wanawake wa kiuchumi kupitia asilimia nne ya mapato ya halmashauri.

Makamu wa Rais alisema jitihada mbalimbali zinafanyika kupeleka maendele vijijini katika nyanja za umeme, ardhi, maji, elimu na afya kwa kuhakikisha mwanamke anakuwa salama, na kuwataka kuchangamkia fursa mbalimbali zilizopo.

Aidha, alisema vitendo vya ukatili ni tishio kwa maendeleo kwa kuwa vitendo vya ubakaji, vipigo, kunyimwa mali vinarudisha nyuma jitihada za serikali katika usawa wa kijinsia kwa kuwa inaleta madhara ya kimwili, kisaikolojia na kiuchumi.

"Aina nyingine ya ukaliti ulioibuka kwa kasi ni ukatili wa kingono ambao ni athari kubwa na ni sawa na uhujumu uchumi kwa kuwa wanaofanyiwa ni sehemu muhimu ya ujenzi wa nchi na sekta mbalimbali," alisema.

**MAKONDA KUWABANA**

WANAOPIGA WAKE ZAO

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza kiama kwa wanaume wanaowapiga wake zao kwa kueleza kuwa atakula nao sahani moja.

Vilevile, amesema ameshapeleka mapendekezo ya kufanyiwa mabadiliko kwa sheria ya mirathi kwa Waziri wa Sheria na Katiba ambayo itakuwa inamtambua mama kuwa ni mrithi namba moja wa mali za mume wake pindi anapofariki.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani.

"Kuanzia leo Machi 8, 2020 mwanaume yeyote atakayempiga mke wake nitakula naye sahani moja, chukueni namba yangu 0682009009 pigeni simu halafu kazi niachieni mimi, kwa yoyote akipigwa na mumewe, uwe kwenye uchumba au kwenye ndoa unachotakiwa ni kunitaarifu tu halafu mimi nitashughulika naye," alisema Makonda.

**RITA YASISITIZA WOSIA**

Jamii imetakiwa kuondoa dhana potofu ya kuwa kuandika wosia ni uchuro kwani suala hilo halina uhalisia wowote bali ni ulinzi wa haki ya familia.

Aidha, wosia ni suala la kisheria na kwamba utunzaji wake ni moja ya kazi zilizoainishwa kwenye sheria hivyo si uchuro kwa sababu kifo hupangwa na Mungu pekee.

Wito huo ulitolewa jana na Mwanasheria wa Serikali Mwandamizi, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), Janeth Mandawa katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Halmashauri ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu.

***Imeandikwa na Salome Kitomari na Gwamaka Alipipi***

## HABARI KITAIFA

# Serikali yalifunga kwa siku 10 daraja la Mwanza-Musoma

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

DARAJA la Mto Simuyu lililoko wilayani Magu katika barabara kuu ya Mwanza-Musoma limeharibika, hivyo serikali kulifunga kwa siku 10 ili kupisha matengenezo makubwa.

Daraja hilo limeharibika kutokana na uchakavu uliosababisha vyuma kukatika.

Akiwasilisha taarifa ya ufungwaji wa daraja hilo Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Marwa Rubirya, alisema ameifunga barabara hiyo kuanzia jana hadi Machi 18, mwaka huu ili kupisha matengenezo makubwa ya daraja.

Mhandisi Rubirya aliongeza kuwa wameamua kufanya matengenezo ya haraka ili kujiepusha na athari zitakazoweza kujitokeza kwa sababu kuchelewa kwa ujenzi huo unaweza kuwasababishia athari watumiaji wa barabara hiyo.

Alisema kuwa barabara hiyo imefungwa ili kupisha matengenezo kuanzia saa tatu usiku hadi saa 11 asubuhi, huku akiomba ushirikiano wa Jeshi la Polisi katika kutekeleza kazi hiyo.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa daraja hilo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema kutokana na changamoto hiyo njia zitafungwa kwa muda uliopangwa kwa siku kumi ili kupisha matengenezo hayo.

Alisema serikali ina mpango wa kujenga daraja jipya, hivyo hatua zinazofanyika sasa ni za muda mfupi, na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu ili waboreshewe njia itakayowanufaisha na kuendeleza ujenzi wa taifa.

"Hali halisi ilivyo na nyie mmeiona... ninachowaomba muwe wavumilivu, ujenzi ufanyike ili kuepusha madhara makubwa ya baadaye," alisema Mongella.

Lusia Isack, mkazi wa Magu akizungumzia adha hiyo, alisema wanakuwa wa hofu kila wanapopita kwenye daraja hilo hasa wanapofika katikati, hivyo wanaishukuru serikali kwa kuliona hilo na kutatua changamoto hiyo kabla haijaleta maafa.

Aliongeza kuwa uchakavu wa miundombinu pamoja na ufinyu wa daraja hilo umekua ukisababisha msongamano mkubwa wa magari, ambao umekuwa ukiwapotezea muda wa kufanya shughuli za uzalishaji mali, hivyo aliiomba serikali kuharakisha marekebisho ya daraja hilo.

"Hili daraja ni bovu sana, hata ukiwa umebebwa kwenye baiskeli ukifika katikati daraja linaanza kucheza... sasa ukiwa kwenye gari unawaza sijui nitapita salama kwa sababu likidondoka tu sidhani kama kuna mtu atakayepona," alisema na kuongeza:

"Kinachobaki ni kuomba Mungu akitutengenezea, watakuwa wametusaidia sana."

Daraja hili lililojengwa mwaka 1962 katika eneo la Kisaba Kata ya Lubugu linakabiliwa na uchakavu wa miundombinu ambapo kwa kuonyesha nyufa baada ya vyuma vilivyokuwa vinalishikilia kukatika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NIC, Margret Karume (wa tatu kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (katikati mwenye suti nyeusi) wakionyesha ishara ya kauli mbiu ya mwaka huu ya Siku ya Wanawake Duniani "#EachforEqual" pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo, baada ya kukabidhi zawadi kwa wagonjwa wa fistula kwenye Hospitali ya CCBRT mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taboa yalia kubanwa mizigo ya abiria

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa), wamepinga kanuni za sheria ya usafirishaji iliyoweka masharti mbalimbali ikiwamo kuwataka wamiliki kuwajibika pindi mizigo ya abiria inapopotea.

Wakizungumza wakati wa mkutano wa wamiliki hao kujadili kanuni za sheria hiyo zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu Tanzania (Latra) na kutoa maamuzi, walisema hawakubaliani na uwajibikaji huo wa kuwa dhamana ya mizigo ya ndani ya basi ipo kwa abiria.

Walisema kwa kanuni hizo mpya, itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa basi kutunza mizigo iliyolipiwa na isiyolipiwa (ya mkononi) ya abiria, jambo ambalo alisema ni gumu kwao, kwa kuwa mizigo isiyolipiwa abiria na thamani yake haijasajiliwa popote, hivyo ni ngumu kujua kiwango cha mizigo aliyonayo.

"Wewe umepanda gari kuna mizigo imewekwa kwenye buti, hivyo tuna rekodi zake kuwa ipo wapi na imelipiwa, tatizo ni wewe umepanda ndani ya gari una mizigo mingine ikiwamo vitu vya thamani kama simu halafu vikaibiwa baadaye unasema umepoteza simu ya Sh. milioni 2 kumbe ni Tecno ya Sh. 300,000," alisema mmoja wa wasafirishaji.

Jingine wanalopinga ni gari ikiharibikia njiani mmiliki atatakiwa kuleta gari lingine ndani ya saa nane, jambo ambalo ni gumu kwa kuwa kanuni hazijaangalia uharibifu huo utakuwa umetokea wapi.

Wasafirishaji hao walisema watatumia njia mbili, mojawapo ni ya kisiasa kwa kuwasiliana na viongozi wa kisiasa na wakiona hawapati msaada watakwenda mahakamani kudai mabadiliko.

Aidha, wasafirishaji hao walisema kanuni hizo ni ngumu na zenye vikwazo vingi kwa ustawi wa kiuchumi wa wamiliki hao.

Awali, Katibu Mkuu wa chama hicho, Enea Mrutu, alisema kanuni hizo mpya zilizo katika Sheria ya Usafirishaji ya Mwaka 2019 ya Mamlaka hiyo sio rafiki na zina mazingira ya kuwakandamiza wamiliki wa mabasi.

"Kanuni mpya za usafirishaji za mwaka 2020 zilizowekwa sisi hatukushirikishwa na kwa kweli ni kandamizi na zisizo tekelezeka," alisema Mrutu.

Alisema kwamba chini ya kanuni hizo mpya, Latra ndiyo yenye jukumu la kuidhinisha mtoa huduma ya vidhibiti mwendo katika mabasi (VTS), jambo ambalo limepingwa vikali na wamiliki hao wa mabasi kwa maelezo kuwa gharama zitakazotozwa zitakuwa kubwa kupita kiasi, hivyo kutaka uhuru katika kuamua mtoa huduma hiyo.

"Tunalazimishwa mtu atakayetufungia vts (vidhibiti mwendo) awe ameidhinishwa na Latra, na pia sasa wanataka mtu atakayefungu mifumo ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao amwidhinishe yeye, kitu ambacho kinafanya wasafirishaji kupata ugumu kwenye kufanya kazi," aliongeza.

## Saba matatani vifaa uvuvi haramu, dawa za kulevya

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linawashikilia watu saba kwa makosa mbalimbali ikiwamo la kupatikana na zana haramu za uvuvi pamoja na dawa za kulevya aina ya mirungi na bangi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, ACP Muliro Jumanne, alisema tukio la kwanza lililotokea, Machi 3, mwaka huu, maeneo ya Bwiru wilayani Ilemela, mkoani hapa baada ya jeshi hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama kuwakamata na kuwashikilia watu watatu ambao ni mfanyabiashara Jeremiah Asam (48), mkazi wa Bwiru na wake zake wawili Joyce Jeremiah (40) na Getruda David (26), ambaye pia ni mfanyabiashara.

Watuhumiwa hao walikamatwa kwa kosa la kupatikana na zana haramu za uvuvi ambazo ni nyavu 7,401, timba 178, nyavu za dagaa tatu na kokoro la dagaa rola moja katika makazi yake maeneo ya Bwiru na dukani kwake Liberty, wilayani Nyamagana.

Hata hivyo, alisema baada ya watuhumiwa hao kukamatwa yalijitokeza madai yaliyowalenga baadhi ya askari polisi kuwa wanadaiwa kukiuka maadili ya utendaji kazi na uchunguzi wa madai hayo unafanywa kwa kufuata mfumo wa kijeshi na ikibainika hatua za kinidhamu za kijeshi zitachukuliwa.

Alisema jeshi hilo linatarajia kumfikisha mahakamani mtuhumiwa Peter Mwita, maarufu Peter Mirungi (46), mkazi wa mtaa wa Rufiji, wilayani Nyamagana kwa makosa ya kusafirisha, kusambazwa na kuuza mirungi jijini hapa, hata hivyo, baada ya mtuhumiwa huyo kujua kuwa anafuatiliwa na polisi Februari 1, mwaka huu, alitelekeza gari namba T.787 DQX aina ya Probox, maeneo ya Igoma Mashariki likiwa na mirungi kiasi cha kilogramu 9.02.

Vile vile, Februari 15, mwaka huu, mtuhumiwa huyo alikamatwa akifanya biashara hiyo haramu kwa muda mrefu.

ACP Muliro, aliongeza kuwa Machi 2, mwaka huu majira ya 12:00 asubuhi huko katika kizuizi cha magari kilichopo Kijiji cha Ngashe, Kata ya Lugeye, Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, askari wakiwa doria walikamata bangi kiasi cha kilogramu 50 zikiwa katika magunia matatu iliyokuwa ndani ya gari lenye namba za usajili T.881 AFX na tela namba T.822 CZZ lori aina ya Scania, iliyokuwa ikitokea Tarime kuelekea Mwanza.

Gari hiyo iliyokuwa ikiendeshwa na Joseph Achiyo, ambaye aliruka kwenye gari na kukimbia wakati gari ilipojsimamishwa na askari, jeshi hilo linaendelea na msako wa kuhakikisha mtuhumiwa anatiwa nguvuni na gari limekamatwa.

UNITED REPBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA

CIVIL REVISION NO. 4/2019
(Arising from Civil case No. 41/2019
REV. MSGR. GOSBERT BYAMUNGU ..............APPLICANT

VERSUS

MULT BUILDERS CO. LTD & OTHER............RESPONDENTS

TO, 1. MULT BUILDERS CO. LTD & OTHER
2. THE REGISTERED TRUSTEE OF KISHURO CHRISTIAN SOCIAL AND EDUCATION SERVICE TRUST.

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Civil Revision No. 4 of 2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 25th day of March, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge F.H. Mtulya. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 3rd day of March, 2020.

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

UNITED REPBLIC OF TANZANIA
JUDICIARY

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA

CIVIL REVISION NO. 5/2019

(Arising from Civil case No. 42/2019
REV. MSGR. GOSBERT BYAMUNGU ................APPLICANT

VERSUS

MULT BUILDERS CO. LTD & OTHER..............RESPONDENTS

TO, 1. MULT BUILDERS CO. LTD & OTHER
2. THE REGISTERED TRUSTEE OF KISHURO CHRISTIAN SOCIAL AND EDUCATION SERVICE TRUST.

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Civil Revision No. 5 of 2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.
Take notice that the above said case has been scheduled for mention on 25th day of March, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge F.H. Mtulya. You are authorized to appear in person or through your Advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this 3rd day of March, 2020.

J.M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

HABARI KITAIFA

# CRDB yahamasisha usawa wa kijinsia katika jamii

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imeungana na taasisi nyingine duniani kusherehekea Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ikilenga kuhamasisha usawa wa kijinsia katika jamii. Akizungumza katika hafla iliyoandaliwa kwa ajili ya wafanyakazi, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, alisema Benki ya CRDB inachukulia kwa umuhimu suala la kumwezesha mwanamke na ndio maana wametoa kipaumbele cha ajira kwa wanawake katika ngazi mbalimbali. "Asilimia 46 ya wafanyakazi wa benki ni wanawake, na tunatamani kuona tunaongeza kufikia asilimia 50," alisema Nsekela.

Alisema Benki ya CRDB pia inafanya jitihada za kuwanyanyua wanawake kupitia nafasi za uongozi huku akibainisha kuwa benki hiyo ina jumla ya wanawake viongozi 284 katika ngazi za umeneja, wakuu wa vitengo na wakurugenzi.

Nsekela alisema benki imedhamiria kujenga mazingira, rahisishi, mazuri na rafiki ya kujenga usawa ili kuwasaidia wanawake waweze kukua katika mazingira yao ya kazi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akiwatambulisha baadhi ya viongozi wanawake wa benki hiyo, kutoka kulia ni Mkurugenzi wa Mawasiliano, Tully Mwambapa, Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo na Mkuu wa Kitengo cha Mikikati ya Biashara, Jessica Nyachiro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Akiongelea mikakati ya Benki ya CRDB ya kumkomboa mwanamke wa kitanzania, Nsekela alisema benki hiyo imefanikiwa kuingiza sokoni bidhaa na huduma maalumu kwa ajili ya kinamama ikilenga kutatua changamoto hizo. Nsekela alisema bidhaa hizo ni pamoja na Akaunti ya Malikia, Mikopo ya WAFI pamoja na huduma za bima za Lady Jubilee.

"Akaunti ya Malkia ni akaunti maalum inayowawezesha kinamama kujiwekea akiba ili kutimiza malengo waliyojiwekea, kama vile kujiendeleza kielimu, kupeleka watoto shule, kujijengea nyumba na kuongeza mitaji ya biashara." Alisema Nsekela huku akibainisha kuwa mpaka sasa zaidi ya kinamama 25,000 tayari wameshajiunga na akaunti hiyo.

Kuhusu huduma za mikopo Nsekela alisema Benki ya CRDB pia imebuni mikopo maalum kwa ajili ya wanawake ijulikanayo kama WAFI yaani "Women Access to Finance Initiatives', Mikopo ambayo inalenga kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwapatia fedha za uendeshaji na uwekezaji ili kusaidia kuboresha biashara zao. Nsekela alisema mikopo ya "WAFI" imepokelewa vizuri sana sokoni kwani zaidi ya kinamama 1,000 wameshapewa mikopo hiyo na tayari Benki ya CRDB imeshakopesha zaidi ya kiasi cha shilingi bilioni 500.

Katika hafla hiyo Benki ya CRDB pia ilizindua kampeni maalum ya kusaidia kutoa taulo za kike (sanitary pads) kwa wanafunzi shuleni. Kampeni hiyo ilianza kwa kuzindua zoezi la uchangiaji lililokuwa likiendeshwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Mwambapa na wafanyakazi wa Benki ya CRDB wamejitokeza kuchangia gharama za ununuzi wa taulo hizo. "Tunashukuru Mkurugenzi wetu Mtendaji ametufungulia kwa kuchangia kiasi cha shilingi milioni moja, hii ni zawadi ya kipekee kwa wanawake wote, lakini pia inaonyesha ni kwa namna gani anawathamini," alisema Mwambapa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, Siophoro Kishimbo, alisema benki hiyo imeweka mikakati endelevu ya kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanawake wa benki hiyo wanapata fursa sawa na wanaume. "Tunaihamasisha jamii kuzingatia usawa katika sehemu zote iwe ni kwenye kazi na hata nyumbani kwenye familia hii itaongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za maendeleo na hivyo kujenga taifa imara zaidi," alisema Kishimbo.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**
To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302


# Serikali kununua magari 300 ya Tanesco

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amesema, wizara hiyo iko kwenye mchakato wa kununua magari 300 kwa ajili ya ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco), ili kuondoa changamoto iliyopo kwa sasa.

Mgalu alisema hayo juzi, alipokuwa akizungumza na wananchi wakati akizindua ofisi ya Tanesco, Kata ya Manerumango, Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani.

Alisema, kwa sasa wako kwenye mchakato wa ununuzi kwa ajili ya kununua magari hayo ambayo yatarahisisha utendaji kazi kwa watumishi na kuwafikishia wananchi kwa haraka.

Mgalu alisema kufunguliwa ofisi hiyo kwenye kata, ni moja ya njia za kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi na kuwapunguzia kutembea umbali mrefu kufuata huduma.

Meneja wa Tanesco Wilaya ya Kisarawe, Nyanda Mlagwa alisema, mwaka 2015 kulikuwa na vijiji vinane vyenye umeme na kwa sasa vijiji zaidi ya 30 vina umeme na wateja 42,000.

Alisema katika kurahisisha utoaji huduma wameandaa mpango mkakati wa kuwafikia wananchi walio mbali na ofisi, kwa kuwa wengi wao walikuwa wakitumia gharama kubwa kwenda Kisarawe mjini kupata huduma.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kisarawe na Diwani wa Kata ya Manerumango, Hamis Dikupatile, alisema, kuwa tatizo la ukosefu wa umeme lilikuwa kubwa na uwapo wa ofisi hiyo utasaidia kutatua kwa haraka.

# MATANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## President's Office – State House
## TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

### Tender No. TZ-TASAF-161184-NC-RFB for Printing Handbooks, Manuals, Publicity Materials and Reports

### Invitation for Tenders

**Date: 4th March, 2020**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.

2. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments for printing services.

3. The The Tanzania Social Action Fund now invites sealed Tenders from eligible providers of for printing services.

4. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering procedures specified in the Public Procurement (Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 as amended in 2016 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.

5. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the *Secretary of the Tender Board, Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 from hours 0800 to 1600 hours* on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

6. A complete set of Tendering Documents in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 5 above and upon payment of a non-refundable fee of *Fifty Thousand (50,000) Tanzanian Shillings or in a convertible currency.* Payment should be direct *deposit to CRDB Bank PCL, Vijana Branch, Dar es salaam, Tanzania Social Action Fund account number 01J1005174000.*

7. All Tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.

8. All Tenders in one original plus three copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be:

| ADDRESSED to: | DELIVERED to: |
|---|---|
| ***The Executive Director,*** <br> ***Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,*** <br> ***P. O. Box 2719,*** <br> ***Dodoma, Tanzania*** <br> ***Phone: +255 26 2963866*** <br> ***Facsimile: +255 26 2963871*** <br> ***Email address: info@tasaf.go.tz*** <br> ***Website: www.tasaf.go.tz*** | ***TASAF, Dar es salaam,*** <br> ***Old Kilwa /Malindi Road,*** <br> ***Main Building, Third Floor,*** <br> ***Room No. 20,*** |

at or before **10:00 hours on 31st March, 2020.** Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the Conference Room.

9. Late Tenders, portion of Tenders, electronic Tenders, Tenders not received, and not opened and not read out in public at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215653102

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## President's Office – State House
## TANZANIA SOCIAL ACTION FUND

**Request for Bids**
**Framework Agreements for Goods**
**(Primary Procurement, One-Envelope Bidding Process)**

**Procuring Agency: Tanzania Social Action Fund**

**Country: Tanzania**

**Name of Project: Productive Social Safety Net Project II**

**Framework Agreement Title: Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts**

**RFB Reference No.: No. TZ-TASAF-148779-GO-RFB to Supply ICT Consumables, No. TZ-TASAF-148787-GO-RFB to Stationery and No. TZ-TASAF-148782-GO-RFB to Motor Vehicle Spare**

**Credit No.: 6489-TZ**

**Date: 4th March, 2020**

1. The Government of the united republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds toward payments under Call-off Contracts that may be awarded under Framework Agreements to Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts. The Primary Procurement to conclude Framework Agreements award Call-off Contracts will be governed by the World Bank's Procurement Regulations concluded through this RFB Primary Procurement process.

2. The Procuring Agency is undertaking the Primary Procurement with a view to concluding Framework Agreements. The Procuring Agency is the sole Purchaser under the Framework Agreements. The Procuring Agency now invites sealed Bids from eligible Bidders to Supply ICT Consumables, Stationery and Motor Vehicle Spare Parts.

3. The Framework Agreements to be concluded will be Single-User. The Single-User entitled to purchase under the Framework Agreements is the Tanzania Social Action Fund.

4. The Framework Agreements to be concluded will be Single-Supplier.

5. The selection of a FA Supplier to be awarded a Call-off Contract will be direct to the Single-Suppliers for each Lot who a particular Framework Agreement is concluded with. However, the conclusion of Framework Agreements shall not impose any obligation on the Procuring Agency to purchase Goods under a Call-off Contract. The conclusion Framework Agreement does not guarantee that a FA Supplier will be awarded a Call-off Contract.

6. Bidding will be conducted through National Competitive Procurement using a Request for Bids (RFB) as specified in the World Bank's "Procurement Regulations for IPF Borrowers" the World Bank's "Procurement Regulations for Investment Project Financing (IPF) Borrowers" (Procurement Regulations) dated July 2016 and revised in November 2017 and August 2018 ("Procurement Regulations"), and is open to all eligible Bidders as defined in the Procurement Regulations.

7. Bidders may submit Bids for one or more lots in a particular bid.

8. The Framework Agreements shall be concluded for a Term of 3 years subject to appraisal annually from the commencement date stated in the Framework Agreement.

9. The Primary Procurement shall establish Closed Framework Agreements.

10. Interested eligible Bidders may obtain further information from Secretary of the Tender Board, Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 and inspect the Bidding document during office hours 0800 to 1600 hours at the address given below.

11. The Bidding document in English may be purchased by interested Bidders upon the submission of a written application to the address below and upon payment of a nonrefundable fee of Fifty Thousand (50,000) Tanzanian Shillings or in a convertible currency. The method of payment will be direct deposit to CRDB Bank PCL account number 01J1005174000 Name of the account is Tanzania Social Action Fund. The document will be collected by bidder at Tanzania Social Action Fund, Dar es salaam, Old Kilwa /Malindi Road, Main Building, Third Floor, Room No. 20 upon presentation of evidence for payment of fees for purchase of bidding document.

12. Bids must be delivered to the address below at or before 10.00 hours East African time on 31st March, 2020. Electronic Bidding will not be permitted. Late Bids will be rejected. Bids will be publicly opened in the presence of the Bidders' designated representatives and anyone who chooses to attend, at TASAF Dar es salaam, Conference Room, Old Kilwa/Malindi on 31st March, 2020.

13. The addresses referred to above is are:

| Bids must ADDRESSED to: | Bids shall be DELIVERED to: |
|---|---|
| **The Executive Director, Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road,** <br> **P. O. Box 2719,** <br> Dodoma, Tanzania <br> **Phone: +255 26 2963866** <br> **Facsimile: +255 26 2963871** <br> **Email address: info@tasaf.go.tz** <br> **Website: www.tasaf.go.tz** | **TASAF, Dar es salaam,** <br> **Old Kilwa /Malindi Road,** <br> **Main Building, Third Floor, Room No. 20,** |

215653102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Utaratibu vitambulisho vya waandishi TFF uchunguzwe

SHIRIKISHO la Soka nchini (TFF), limekuwa na utaratibu wa kutengeneza vitambulisho ama pasi (accreditation) za kuingilia uwanjani kwa waandishi wa habari kwa msimu mzima, zikiwamo za washika dau (stakeholders), timu na watoa huduma mbalimbali.

Kwa ujumla ni utaratibu ambao bila shaka umekuwa mzuri na wakupongezwa na wanahabari wote wa michezo kwani huwaondolea usumbufu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku katika kuripoti mechi viwanjani.

Hata hivyo, kabla ya msimu huu wa 2019/20 kuanza, TFF ilichelewa kuvitengeneza hivyo kuwatangazia wanahabari wa michezo kuendelea kutumia vya msimu uliopita.

Lakini ilivyofika mechi ya watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga Januari 4, mwaka huo, TFF ikatangaza kutovitambua vya msimu uliopita na kutengeneza vingine maalum kwa ajili ya mchezo huo.

Na kabla ya mechi ya Yanga dhidi ya Simba jana, Jumapili, tayari TFF ilishatengeneza vitambulisho vya msimu mzima na vikawa vinatumika katika mechi zote za Ligi Kuu.

Lakini Nipashe lilishangazwa na siku mbili kabla ya mechi hiyo ya watani wa jadi, TFF kutangaza kutovitambua vile vya msimu mzima na kugawa vingine vilivyoandaliwa maalum kwa ajili ya mchezo huo. Na hilo halikuwa kwa waandishi tu bali 'accreditation' zote za msimu mpaka zile za washika dau, timu na watoa huduma mbalimbali hata kwa VVIP waliokata za msimu mzima.

Suala hili wanahabari walilikemea sana katika mechi ya mzunguko wa kwanza ya watani hao wa jadi, wakieleza kuwa huenda lipo kwa ajili ya kuwanufaisha watu wachache wanaotumia mwanya huo kujitengenezea fedha, lakini TFF imefunga masikio na kuendelea nalo jambo ambalo linaonyesha pengine kweli kuna wanufaika.

Cha kujiuliza na kinachokera zaidi waandishi wanaotekeleza majukumu yao ya kila siku ni walewale waliopewa pasi za msimu mzima ndio waliotengenezewa nyingine kwa ajili ya mchezo huo, ingawa pia hatuna uhakika kama wote walipata pasi hizo.

Lakini pia wanahabari za michezo wanahoji je, hawaaminiwi? Ama wanatakiwa kufanya kazi ya kuripoti mechi nyingine na ikifika siku ya mchezo wa Simba na Yanga wapunguzwe idadi ya watakaoruhusiwa kwenda kuripoti?

Je, kuna faida gani inapatikana kwa TFF kutoka kwa mzabuni wa kuvitengeneza au hiyo ni nafasi ya kuwapa na watu wengine vitambulisho ambao si waandishi? Ama ni moja ya kupunguza waandishi kwa sababu wanajaza uwanja ili fedha zipatikane kwa wingi zaidi?

Hayo ni maswali ambayo TFF inatakiwa kuyatolea ufafanuzi ili waandishi wa michezo ambao wamekuwa wakifanya majukumu yao katika kila mechi waweze kujua ukweli wa suala hilo hasa kutokana na usumbufu huu inapofika siku ya mchezo wa Simba dhidi ya Yanga.


Nipashe limechunguza suala hili kwa mapana zaidi, na inaonyesha mbali na maswali hayo pia inawezekana kuna mtu anajitengenezea mazingira ya kazi na kupata pesa kwa sababu kama inafikia hatua pasi zote zinafutwa katika mchezo huo na kutengenezwa zingine maalum, hiyo inamaana ana uhakika wa kulipwa fedha nyingi na kwa wakati kwa kuwa mechi hiyo huingiza kipato kikubwa.

Hapa inaonyesha kuna 'kamtandao' kavitambulisho kanacheza na akili za viongozi wa TFF ili kujipatia fedha ambazo kimsingi ni kuhujumu mapato ya klabu na serikali kwa ujumla.

Hivyo, kuna haja ya TFF kuja na majibu ya kina kutuelewesha nini maana yake, lakini pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ianze kulichunguza kwa kina suala hili kwani kimsingi inaonekana kuna 'kamfumo' kalikotengenezwa kaupigaji hela kupitia pasi hizo za uwanjani inapofika mechi kubwa ambazo wanaamini zinaingiza fedha nyingi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




### Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Singida United inapojishusha daraja yenyewe

INASIKITISHA sana kuona hali mbaya iliyokuwa nayo Singida United kwa sasa, huku ikionekana dhahiri kuwa itakuwa ni moja kati ya timu zitakazoshuka daraja msimu huu.

Ina pointi 12 tu mpaka sasa ikiwa imecheza mechi 27 na inaburuza mkia, yaani iko nafasi ya 20 ambayo ni ya mwisho kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Timu ya juu yake, yaani inayokamata nafasi ya 19 ni Mbao FC ambayo ina pointi 22. Ina maana kuwa Singida United imepitwa pointi 10 nzima na timu iliyo juu yake Mbao FC.

Hii ina maana kuwa ni muujiza kwa timu hiyo kusalia Ligi Kuu, kwani msimu huu jumla ya timu nne zinashuka moja kwa moja kuanzia ya 17 hadi ya 20, huku ya 15 na 16 zikienda kucheza 'play off' na timu za zitakazoshika nafasi ya pili kwenye makundi mawili ya Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Kama zitashinda basi zitarejea na kama zitafungwa, basi msimu ujao hatutoziona tena. Tukirejea kwenye timu tunayoizungumzia ya Singida United, niseme tu kama itashuka daraja basi itakuwa imejishusha yenyewe.

Singida United ni timu iliyopanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu kwa mbwembwe msimu uliopita wa 2017/18 na ilikuwa imesheheni nyota mbalimbali wa hapa nchini na nje ya nchi, kiasi cha kutishia si Simba na Yanga tu peke yake, hata timu za aina yake kama Azam FC.

Ilimaliza ligi msimu wa kwanza ikikamata nafasi ya tano kwa pointi 44, na soka lake lilivutia wengi kiasi hata cha kwenda kushiriki michuano ya Kombe la SportPesa nchini Kenya.

Pamoja na matatizo ya uongozi, lakini kuanza kujionyesha ufahari kuwa ina pesa nyingi au uwezo mpaka kusajili baadhi ya wachezaji na kuwapeleka kwenye klabu ya Yanga, hapo ndipo tatizo lilipoanza.

Mchezaji kama Feisal Salum "Fei Toto' ambaye alisajiliwa na Singida United, lakini kabla hata hajaanza kucheza, akapelekwa Yanga na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo wakajinasibu kuwa wameisaidia, ilionekana ni kitu kigeni kidogo kwenye soka, lakini baadhi ya watu walianza kutabiri anguko la timu hiyo.

> **Mchezaji kama Feisal Salum "Fei Toto' ambaye alisajiliwa na Singida United, lakini kabla hata hajaanza kucheza, akapelekwa Yanga na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo wakajinasibu kuwa wameisaidia, ilionekana ni kitu kigeni kidogo kwenye soka, lakini baadhi ya watu walianza kutabiri anguko la timu hiyo.**

Haiwezekani wachezaji wazuri wakapelekwa kwenye timu nyingine, huku timu iliyowasajili ikabaki na wachezaji wa kawaida.

Hii ni sawa na kumnunulia silaha adui yako. Yanga ilikuwa inacheza Ligi Kuu ya Tanzania na Singida United pia, na ilikuwa inahitaji wachezaji bora ili kushindana na upinzani, hivyo kuwatoa wachezaji wazuri na kupeleka timu nyingine ni sawa na kujimaliza mwenyewe.

Ikumbukwe kuwa wakati huo Yanga haikuwa vizuri kwenye masuala ya pesa, lakini ilijikuta ikipata msaada huo wa wachezaji.

Kwa sasa Yanga iko vizuri kidogo na Singida iko hoi kipesa, tunachokiona ni kwamba haijasaidiwa chochote kupewa baadhi ya wachezaji kipindi cha dirisha dogo, badala yake imekuwa ikisajili wachezaji wa muda mrefu kwenye Ligi Kuu ambao nao bado wameshindwa kuipambania timu hiyo kuitoa shimoni.

Wakati yenyewe ilikuwa ikitoa msaada, lakini kwa sasa haipati msaada wowote na inajipambania yenyewe. Nina uhakika ingekuwa na baadhi ya wachezaji ambao iliwatoa kwa msaada, sidhani kama saa hizi ingekuwa kwenye wodi ya wagonjwa mahututi.

Nadhani litakuwa ni fundisho kwa viongozi wengine wa soka kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na timu mbili zinazocheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa pamoja kiasi cha kutaka kusaidiana.

Kwa shida ambazo kwa sasa inapitia, Singida United bado inakumbuka kipindi bora kabisa ilichopitia na viongozi wa klabu hiyo watakuwa wamejifunza kupitia hilo.

## BARUA/ MJADALA

# Tuige ziara za mawaziri

**Mhariri,**

*KATIKA moja ya maelekezo kutoka kwa Rais John Magufuli ni hitaji lake kwa viongozi waandamizi wa kiserikali, akiwataka wawe na muda wa kutosha kuwafikia wananchi mahali waliko.*

*Ninapenda kukiri namna hili linavyotekelezwa. Ukimfuatilia Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, utagundua ni mtu wa safari ndefu kila kukicha kifuatilia mambo uso kwa uso kujua nini hasa kinachoendelea mipango na maendeleo ya Watanzania.*

*Sehemu ya nyayo zake za mwisho, ni namna alivyokuwa katika mkoani Tanga, akisifu mazuri na machafu yaliyoko, lengo ni kuiweka vizuri Tanga na katika mstari wake unaoendana na mchakamchaka wa Rais Dk. John Magufuli.*

*Nimguse mtendaji mwingine aliye chini yake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), naye nakiri mbunge huyo wa Kisarawe anavyowajibika. Si haba, anahangaika huku na kule kusaka majibu, pia kuyajua klwa uhalisia wa macjio yake .*

*Hapo kunaweza kuwepo mtandao mpana, nikiwataja mawaziri kama vile Profesa Makame Mbarawa (Maji) na Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile. Wote hao ni wa 'kiguu na njia.'*

*Sisio wananchi ni jambo linalotuonyesha ishara njema, viongozi kutufikia wananchi tuliko na kutatulia matatzio yetu katika namna sahihi inayopaswa. Pia inajenga sura ya urafiki na ukaribu.*

*Ni jambo jema, somo hio ambalo kama baadhi yetu na v viongozi wa chini hata kama hatujaiona katika uhalisia wake, basi vyombo vya vya habari vinatufikia na kutuhabarisha hata madiwani na vionngozio kata, kufanyia kazi.*

***Mwalimu Saudia Juma, Bagamoyo.***

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# Waarabu na mbinu za kuongeza 'mapro', Tanzania kupunguza!

**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka kadhaa sasa TP Mazembe imekuwa ikizisumbua sana timu za Kiarabu ambazo zimekuwa zinatawala sana soka la Afrika.

Timu za Kiarabu tayari zilikuwa zimemaliza utawala wa soka la timu za Afrika Magharibi, lakini ilikuwa inatatizwa sana na timu ya TP Mazembe ambayo ilikuwa inazinyanyasa timu za huko.

Jumamosi iliyopita, timu ya Raja Casablanca ya Morocco imeiondosha TP Mazembe kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya kushinda mabao 2-0 nyumbani na kufungwa bao 1-0 ugenini.

Kwa miaka michache iliyopita, TP Mazembe imeonekana kama vile imemaliza nguvu za timu hiyo na imekuwa haina makali tena.

Ni kitu gani ambacho Waarabu wameisoma TP Mazembe na sasa imekuwa haifurukuti? Moja kati ya vitu ambavyo Waarabu wamefanya ni kusajili baadhi ya wachezaji wa kigeni ('mapro') hususan wa Kiafrika, ikiwamo kutoka kwa TP Mazembe yenyewe.

Zamani Waarabu walikuwa wenyewe tu kwenye timu zao, na hawakuwa na wachezaji wa kigeni au kutoka mataifa mengine ya Afrika, hasa weusi.

Walitamba kwa muda mrefu, lakini kuanzia miaka ya 2000, kibao kiligeuka na timu za Afrika Kusini na TP Mazembe ya DR Congo zilianza kusumbua na kuzifanya timu za Waarabu kuhangaika. Uzuri ni kwamba inaonekana timu za Kiarabu zilikaa na kufikiri, zikaona zijiongeze.

Zikaacha umimi na Uarabu wao, zikaamua kuanza kusajili wachezaji kutoka Afrika Magharibi, Kusini na hata Congo kwenyewe.

Hata mfungaji wa bao la kwanza la Raja Casablanca ni Mkongomani Ben Malango ambaye awali alikuwa akiichezea timu hiyo hiyo ya TP Mazembe.

Hiyo ni baadhi ya mbinu ambazo wametumia, kuleta aina mpya na mchanganyiko wa soka, wakiwa na wachezaji wabunifu, lakini kwenye maeneo fulani wakiwa na wachezaji wenye nguvu ambazo wao hawana.

Pia wachezaji hao wageni wanawasaidia kucheza kwenye mazingira ya nchi zenye joto, hivyo hawaathiriki sana wanapokwenda kucheza ugenini.

Ukiziangalia kwa sasa timu nyingi za Morocco, Libya, Misri, Algeria, Tunisia zina wachezaji wengi weusi na si Waarabu wenzao, hivyo kuleta upinzani mkubwa zinapokutana zile za kutoka ukanda mwingine wa Afrika.

Tena vyama vya soka kwenye nchi hizo vikakaa na kukubaliana kuwa mchezaji kwenye klabu yoyote kwenye nchi hizo wa Kiarabu asihesabiwe kama mchezaji wa kigeni. Ina maana mchezaji wa Morocco akicheza Zamaleki ya Misri hahesabiwi kama mchezaji wa kigeni.

Na hii ni baada ya kuteseka hasa na timu za Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini na TP Mazembe ya DR Congo.

Hili ni fundisho kwa Watanzania wote kuwa dawa ya kuinua soka la Tanzania si kupunguza wachezaji wa kigeni, bali ni kutafuta mwarobaini na kwa nini timu zetu hazifanyi vema kwenye mechi za kimataifa.

Wakati hata Waarabu ambao wao wanajiona wanajua sana kutandaza kabumbu kuliko maeneo mengine ya Afrika wameshtuka na kuanza kusajili kutoka nchi mbalimbali tena wachezaji wengi, sisi tunafikiria kupunguza wachezaji 10 wa kigeni.

Tena tunataka kupunguza kwa sababu za kufikirika na si za kitaalamu, kwani hata kwetu imedhihirika kuwa wachezaji wa kigeni wameifanya Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa bora, lakini pia ndiyo kwa kiasi kikubwa waliowezesha Simba kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita.

Mabao 18 ambayo Simba ilifunga, 15 yalifungwa na wachezaji wa kigeni. Hata Yanga na Azam kwenye mechi zao za kimataifa msimu huu pamoja na kutolewa, mabao yao mengi yamefungwa na wachezaji wa kigeni.

Soka halina siasa siku zote. Kama Tanzania tunataka kucheza soka la burudani na siasa, basi tupunguze wachezaji wa kigeni. Lakini kama tuna ndoto klabu za Simba, Yanga, Azam na zingine siku moja zichukue Kombe la Afrika, basi ni vema wachezaji wa kigeni wakabaki kuwa 10 au waongezwe na si kupunguza.

Kama hata Waarabu wameshagundua hilo na sasa wanaingiza timu zote nne Al Ahly, Raja Casablanca, Wydad Casablanca na Zamaleki kwenye nusu fainali baada ya kuyafanyia kazi upungufu wao hasa sera za wachezaji wa kigeni, sisi ni nani tupinge na kupunguza?

**KABWELA** NA FADHILI MOHAMMED



# Siku 30 kwa wazalishaji vifungashio plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limetoa siku 30 kwa wazalishaji, wasambazaji na wauzaji wa vifungashio vya plastiki aina ya 'tubing, kuacha kuzalisha bidhaa hiyo na badala yake watumie vifungashio mbadala vilivyoelekezwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hakutakuwa na huruma kwa mfanyabiashara yeyote atakayekaidi agizo hilo kwani serikali imeamua kuzitafsiri kwa vitendo kanuni na sheria zinazoongoza katazo hilo linalolenga kulinda mazingira.

"Uwingi wa aina hiyo ya mifuko unaondoa kabisa mantiki na lengo nzima la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki pia kuongezeka kwa mifuko hiyo na jinsi ilivyobadilishwa matumizi na wananchi," alionya Dk. Gwamaka, na kuongeza kuwa zinachangia kuua viwanda vya ndani naserikali kukosa kodi stahiki.

Mbali ya marufuku hiyo, NEMC imesema kutakuwa na ukaguzi utakaoshirikisha mamlaka zote zinazohusika, likiwamo Shirika la Viwango Tanzania (TBS) nchi nzima kuwabaini wakiukaji wote na kuwachukulia hatua za kisheria na kuwatoza faini.

"Kuna wafanyabiashara wameendelea kuzalisha vifungashio vya plastiki, ambavyo vilipigwa mafuku tangu Juni Mosi, 2019. Kuendelea kuzalisha mifuko hiyo ni kukiuka kanuni, taratibu na sheria za mazingira zinazoongoza katazo la matumizi ya mifuko hiyo. Hivyo tunatoa mwezi mmoja kuanzia sasa wafanyabiashara wanaozalisha mifuko hiyo kusitisha uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa vifungashio hivyo," alisema Dk. Gwamaka.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka, vifungashio hivyo vya plastiki aina ya 'tubing' ambavyo vinatumika kufungia vitu kama karanga, ubuyu na barafu sasa vinazalishwa kwa wingi na ukubwa tofauti na kutumika kama vibebeo kwa bidhaa za sokoni.

Alisema kubaki kwa vifungashio vya 'tubing' ilikuwa ni kwa hisani ya serikali na siyo takwa la kisheria au kanuni zinazopigamarufuku matumizi ya plastiki, lakini kutokana na wingi wake mtaani hakuna sababu ya kuendelea kubaki na huruma hiyo kwa maana kuwa madhara yake hayatofautiani na mifuko mingine ya plastiki.

Aliongeza kuwa marufuku ya 'tubing, itasaidia kuwabana wazalishaji wasio rasmi, kulinda afya za watu na mazingira, kutengeneza ajira, kurahisisha ufuatiliaji wa sheria na kulinda wafanyabiashara waaminifu.



Mwenyekiti wa Masjidi Al-Wahaab, Mohamed Issa, jana, akimkabidhi misaada Mkuu wa Gereza la Kahama, Lusana Shigumha, kwa ajili ya wafungwa na mahabusi wa gereza hilo, mkoani Shinyanga. **PICHA: SHABAN NJIA**

# NMB yaahidi neema wafugaji, wakulima

**Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua tawi jipya Wilaya ya Busega mkoani Simiyu na kufikisha matawi 225 nchi nzima, huku ikitangaza neema ya huduma bora na mikopo nafuu kwa wananchi wakiwamo wakulima, wafugaji na wavuvi kusaidia shughuli za kiuchumi.

Akitoa taarifa ya utendaji wa benki hiyo kwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakati wa hafla ya ufunguzi wa tawi hilo jana, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ufunguzi wa tawi hilo pamoja na mengine maeneo ya vijijini ni utekelezaji sera huduma jumuishi ya kifedha kwa makundi yote ya kijamii hadi vijijini.

Alitaja baadhi ya huduma jumuishi zinazotolewa na benki hiyo hadi katika ngazi ya wilaya, kata na vijiji kupitia mawakala kuwa ni pamoja na mikopo ya mitaji kwa wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa, pembejeo kwa wakulima na aina zote za bima kuanzia ya afya, vyombo vya usafirishaji na ujenzi wa nyumba bora.

Alisema pamoja na huduma ya kibenki ikiwamo mikopo yenye riba nafuu, NMB pia inatoa huduma ya aina zote za bima, malipo kwa njia ya mtandao na elimu ya usimamizi wa fedha kwa wakulima kupitia vyama vyao vya msingi vya ushirika (Amcos) kupitia NMB Foundation.

"NMB imetoa mikopo kwa Amcos 202 kati ya 383 za mkoa wa Simiyu," alisema Zaipuna.

Alisema kupitia huduma ya NMB mkononi, wateja wa benki hiyo wataweza kufungua akaunti kupitia simu zao za kiganjani bila kulazimika kwenda benki na kuwaomba wananchi walioko maeneo ambako hakuna matawi ya benki kuchangamkia fursa hiyo.

Zaipuna alisema NMB imetenga zaidi ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa kurejesha sehemu ya faida kwa jamii.

"Mkoa wa Simiyu tayari imepokea zaidi ya Sh. milioni 200 kugharamia miradi ya maendeleo katika sekta ya elimu, afya na mafunzo kwa wakulima kupitia Amcos zao," alisema Zaipuma.

Akimkaribisha Makamu wa Rais kuzindua tawi hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliiagiza Benki Kuu (BoT) kukutana na benki na taasisi za fedha nchini kuainisha namna ya kupunguza viwango vya riba ya mikopo kutoa nafuu kwa wananchi kukopa kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

Alisema serikali kupitia BoT, imezipunguzia riba iliyokuwa ikiyatoza benki na taasisi za fedha kutoka asilimia 16 mwaka 2016 hadi asilimia saba na kuagiza nafuu hiyo ishuke chini hadi kwa wakopaji wadogo.

Akizindua tawi hilo, Samia alisema uimara na huduma ya sekta ya fedha ni mhimili muhimu katika maendeleo na uchumi wa Taifa na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha shughuli zao huku akiahidi kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira bora na wezeshi kuendeleza sekta hiyo.

Aliipongeza Benki ya NMB kwa uendeshaji mzuri unaoiwezesha kupata faida na hivyo kuiwezesha serikali kuvuna zaidi ya Sh. bilioni 586 kupitia kodi na ushuru mbalimbali. Makamu wa Rais pia aliishukuru NMB kwa kutenga na kutumia zaidi ya Sh. bilioni 5 kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia sera ya kurejesha sehemu ya faida kwa jamii.

# Kaliua yatoa mkopo mil. 345/- kwa vikundi

**Na Tiganya Vincent**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaliua, imekabidhi mkopo wa Sh. milioni 345 kwa vikundi 57 ikiwa ni sehemu ya asilimia 10 ya mapato yake ya ndani katika mwaka wa fedha unaoendelea.

Taarifa hiyo imetolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. John Pima, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo kimkoa yalifanyika wilayani humo.

Alisema kati ya fedha hizo vikundi 28 vya wanawake vimepokea Sh. milioni 184, vikundi 19 vya vijana vimekopeshwa 133.5 na vikundi 10 vya wenye ulemavu vimekopeshwa Sh. milioni 27.

Alisema fedha hizo ni sehemu ya utekelezaji Ilani ya Chama Cha Mapinduzi iliyoagiza kutenga asilimia 10 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vikundi hivyo.

Dk. Pima alisema tangu mwaka 2015 hadi Desemba 2019, Kaliua ilikuwa imeshatoa jumla ya mikopo ya Sh. milioni 839.7 kwa vikundi 209.

Pia mkurugenzi huyo alisema hadi sasa jumla ya Sh. milioni 591.9 bado haijarejeshwa kitendo ambacho kimewafanya waandikie notisi ya siku 90 ili warejeshe.

Akikabidhi hundi kwa vikundi, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, amevitaka vikundi ambavyo bado havijaresha mikopo waliopatiwa kurejesha ili iweze kuwasaidia wengine.

Aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua na kuzitaka nyingine za mkoa huo kutenga asilimia 10 za mapato yake ya ndani kwa ajili ya kupeleka katika vikundi kama ilivyoelekezwa.

Mwanri alisema, ni vema halmashauri zikahakikisha zinatoa fedha ambazo zitavisaidia vikundi kupata matokeo mazuri na kuwapatia maendeleo.

**Alisema fedha hizo ni sehemu ya utekelezaji Ilani ya Chama Cha Mapinduzi iliyoagiza kutenga asilimia 10 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa vikundi hivyo.**

HABARI KITAIFA

# Bil.40/- kusambaza sasa umeme vijijini

**Na Renatha Msungu, CHEMBA**

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 40.2 kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye vijiji mbalimbali nchini.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, wakati akiwasha umeme katika kijiji cha Farkwa wilayani Chemba mkoani Dodoma.

Alisema zaidi ya vijiji 50 vimewekewa umeme na vilivyobaki vitawekewa hivi karibuni, huku akisisitiza kuwa Juni mwaka huu vijiji vyote vitakuwa na umeme.

Kuhusu kijiji hicho, waziri huyo alisema wameanza kulia muda mrefu kuomba umeme ili kujiletea maendeleo.

Aliwataka kuutunza umeme huo ili wafikie malengo waliojiwekea.

"Kila mwananchi hivi sasa anapaswa kuwa na umeme kutokana na kwamba maendeleo hayaji bila kuwa na umeme," alisema.

Alieleza kuwa katika wilaya hiyo kati ya vijiji 114, vijiji vitatu ndio vilibaki havina umeme.

Alisema lengo lao ni kuona vitongoji vyote vya Farkwa vinakuwa na umeme.

"Ni jambo jema kuona kila kijiji kinakuwa na umeme wananchi mtumie vizuri umeme huu," alisema.

Naye Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia, alisema umeme huo utasaidia kubadilisha maisha yao na kuwa watu watafanya biashara ili kujiongezea kipato.

"Wananchi acheni kusikiliza maneno ya uongo fanyeni kazi ya kujiletea maendeleo," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga, alisema kuwashwa kwa umeme Farkwa kumechangia kuongeza maendeleo katika eneo hilo.

# Wakulima pamba watakiwa kufungua akaunti za benki

**Na Happy Severine, SIMIYU**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, amewataka wakulima wa pamba kufungua akaunti katika benki mbalimbali ili malipo yao ya mauzo ya msimu huu yafanyike kwa njia ya benki.

Bashe amesema kuwa serikali imeziagiza benki kuhakikisha kila mkulima anapata namba ya akaunti, na kuzitaka benki kuhakikisha zinazingatia makubaliano yote ambayo waliwekeana.

Naibu Waziri alisema hayo wakati akizindua mpango mkakati wa mapinduzi ya kilimo cha pamba katika Mkoa wa Simiyu kwa miaka mitano, ambao unatekelezwa na taasisi inayoshughulikia masuala la pamba na nguo Gatsby Afrika.

Bashe aliwataka wakulima ambao wanazalisha pamba nchini, kuhakikisha wanajitokeza kwa wingi wakati benki zitakapopita mbalimbali kwenye maeneo yao kwa ajili ya kuwafungulia akaunti.

Mkurugenzi wa Gastby anayesimamia mazao ya pamba na nguo, Samuel Kilua, alisema mkakati huo unalenga kuongeza tija katika uzalishaji wa zao hilo.

Alisema utafiti unaonyesha wakulima wengi wamekuwa wakizalisha kilo 100 hadi 200 kwenye hekari moja, tofauti na inavyotakiwa kwani wakilima kwa tija wanaweza kuzalisha kilo 1,000.

Alieleza kuwa mkakati huo, umelenga kuboresha kwenye maeneo ya ugani, kuwaelimisha wakulima namna bora ya kunyunyuzia dawa, ambapo mkakati huo umelenga kuwafikia wakulima wote katika mkoa huo.

Mkuu wa Mkoa huo, Antony Mtaka, alisema kuwa mkakati huo utaweza kusaidia mkoa wa Simiyu kuongeza uzalishaji kutoka kilo milioni 160 hadi kufikia kilo milioni 400.




Mkurugenzi wa TBL, Philip Redman (kulia), akimkabidhi mfano wa ufunguo wa gari meneja wa kampuni ya usambazaji bidhaa za TBL, ya Fresa Investment Ltd ya Arusha, Happyness Joseph (katikati), baada ya kutangazwa mshindi wa kwanza wa usambazaji wa bidhaa za TBL 2019 na kujishindia gari aina ya lori wakati wa mkutano wa TBL Distributors TBL Conference 2020 jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mkurugenzi wa Mauzo Mikoa ya Nyanda za Kaskazini, James Bokella. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi kuchangia mil. 133/- kituo afya

**Na Sabato Kasika**

WAKAZI wa Kata ya Bugwema, Musoma Vijijini mkoani Mara, wamekubaliana kuchangia Sh. milioni 133.7 ili kuunga mkono mpango wa serikali wa kupanua zahanati ya kijiji cha Masinono kuwa kituo cha afya.

Tayari serikali imetoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya upanuzi huo ambao unaanzia ujenzi wa wodi ya mama na watoto, jengo la upasuaji, maabara, jengo la kufulia nguo, chumba cha kuchomea taka na kuhifadhia maiti.

Upanuzi huo pia utahusisha uwekaji wa miundombinu ya majisafi, majitaka na mingine yote muhimu inayohitajika kwa ajili ya wagonjwa watakaofika kupata huduma katika kituo hicho kitakapokamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, alisema kata hiyo inaundwa na vijiji vinne alivyovitaja; Masinono, Bugwema, Muhoji na Kinyang'erere.

"Wakazi wa vijiji hivyo wamekubaliana kuunga mkono juhudi za serikali katika upanuzi wa zahanati hiyo kuwa kituo cha afya na kila kijiji kitachangia Sh. 33,437, 500 ambazo kwa vijiji vinne jumla yake ni Sh. 133,750,000," alisema.

Mbali na kuchanga kiasi hicho cha fedha, mkuu huyo wa wilaya alisema, wananchi hao pia wamejipangia siku za kusomba mawe, mchanga, maji na vitu vingine vinavyohitajika katika ujenzi huo.

Alisema, wakati zahanati hiyo ikipanuliwa, kuna ujenzi wa kituo kingine cha afya unaendelea katika Kata ya Nyambono na pia ujenzi wa hospitali ya wilaya unaendelea kwenye kitongoji cha Kwikonero, kijiji cha Suguti Kata ya Suguti.

"Vilevile kuna vituo viwili vya afya vinavyotoa huduma kikiwamo cha Kata ya Murangi na Mugango na pia kuna zahanati 24 za serikali zinazofanya kazi huku nyingine 13 zikiendelea kujengwa," alisema.

Naye Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, alisema, mwezi ujao atachangia upanuzi wa zahanati hiyo atakapokuwa jimboni mwake kukagua shuughuli za maendeleo.

"Nilishakabidhi magari matano ya wagonjwa katika zahanati ikiwamo ya Masinono, ambayo sasa inapanuliwa kuwa kituo cha afya, lakini mwezi ujao nitakwenda kuchangia upanuzi huo," Prof. Muhongo alisema.

Alifafanua kuwa alichangia mifuko 400 ya saruji kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya kituo cha afya Murangi na kukabidhi gari za wagonjwa na pia alifanya hivyo wakati wa upanuaji wa zahanati ya Mugango ambayo sasa ni kituo cha afya.

Diwani wa Bugwema, Ernest Maghembe, alisema, wananchi wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kwa ajili ya maendeleo yao.

## HABARI KITAIFA

# Usajili wa kampuni binafsi ulinzi waanza

**Na Mwandishi Wetu**

USAJILI wa kampuni binafsi za ulinzi na askari wa kampuni hizo kwenye kanzi data ya kielektroniki kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Sekta ya Ulinzi Binafsi (PSGP), umeanza mikoani baada ya zoezi hilo kufanyika kwa muda jijini Dar es Salaam.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Narcis Missama, alizindua rasmi usajili huo jijini Dodoma, ikiwa ni mkoa wa pili kufikiwa baada ya Dar es Salaam, katika kikao cha wamiliki na wakurugenzi wa kampuni binafsi za ulinzi takribani 60 zilizopo mkoani humo, kilichofanyika hivi karibuni.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Missama, alisisitiza maelekezo ya jeshi hilo kuwa askari wote wa kampuni binafsi za ulinzi nchini ambao watakuwa hawajapatiwa mafunzo na kusajiliwa kwenye Mfumo wa PSGP hawataruhusiwa kujihusisha na kazi za ulinzi baada ya Desemba 31, 2020.

Alisema endapo wahusika hawatafanikisha suala la kuwapatia mafunzo wafanyakazi wao na kuwasajili kwenye kanzi data ya PSGP, Jeshi la Polisi litawazuia kufanya kazi kwani itakuwa ni kinyume na maelekezo ya jeshi hilo na maazimio ya kikao hicho.

"Kampuni ya ulinzi isiyotoa mafunzo kwa wafanyakazi wake na kuwasajili kwenye mfumo wa PSGP ina maana sisi tutamzuia mlinzi wake kufanya kazi; na hii ina maana kuwa kampuni itakuwa imezuiwa pia kufanya kazi mpaka pale watakapokamilisha taratibu husika," alifafanua Kamishna Msama.

Mkurugenzi wa miradi wa Kampuni ya Data Vision International, Macmillan George, alisema kwa ushirikiano wa wadau wa sekta binafsi ya ulinzi na Jeshi la Polisi wamebuni mfumo wa kusimamia sekta ya ulinzi nchini ili kuhakikisha kuwa wadau kwenye sekta hiyo wanafaidika na wananchi wanapata huduma ya ulinzi yenye uhakika zaidi wa usalama.

Alisema mbali na hatua hiyo ambayo inakumbusha juu ya umuhimu wa utunzaji wa taarifa za kampuni, pia mkutano huo umezindua rasmi utaratibu huo kwa kukutana na wakurugenzi hao wa kampuni binafsi 60 zinazotoa huduma za ulinzi jijini Dodoma.

"Mfumo huu ni wazi kuwa utaratibu utunzaji wa kumbukumbu na taarifa mbalimbali katika sekta binafsi ya ulinzi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na ndio sababu tumekutana hapa Dodoma na wamiliki wa kampuni binafsi za ulinzi," alisema George.

Aliongeza kuwa lengo kubwa la ubunifu wa mradi huo ni kuisaidia serikali katika kuratibu sekta ya ulinzi binafsi katika masuala ya kijamii kwa kuweka mikakati endelevu itakayosaidia kufikia malengo.

Alisema baada ya Dodoma, usajili huo ambao ni endelevu utaingia mikoa mingine na kwamba wamepanga kuzindua pia mikoa ya Kanda ya Ziwa hivi karibuni.

Naye Mkaguzi mstaafu wa Jeshi la Polisi, George Nelson Andala ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni binafsi ya ulinzi, alisema wameipokea kwa mtazamo chanya na wana imani itawasaidia katika mambo muhimu hasa taarifa za askari wao.

Alisema mradi huo ambao pia ni wa kuwasajili askari na watumishi katika sekta binafsi sio tu utawasajili na kutunza kumbukumbu na pia utasaidia kuondoa dhana ya watumishi kuacha kazi kiholela na kuhama kampuni kiholela.




Mkurugenzi wa Masoko wa kampuni ya umeme wa nishati ya jua ya ZOLA, Eric Ballegu (kushoto), akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari Wilaya ya Ilala wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Bukua na Ushinde' ya kampuni hiyo, yenye lengo la kuhamasisha wanafunzi wa kidato cha nne 2020 kufanya vizuri katika mtihani wao wa taifa. Uzinduzi huo ulifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# RC Mahenge ataka wanawake kuiombea amani Tanzania

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaomba wanawake wa madhehebu mbalimbali kuiombea Tanzania ili iendelee kuwa kitovu cha amani hasa katika mchakato wa uchaguzi mkuu.

Dk. Mahenge alitoa ombi hilo jana katika maombi ya wanawake duniani yaliyoandaliwa na Umoja wa Madhehebu ya Kikristo mkoani hapa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema maombi ya wanawake huwa yanafika na kujibiwa, hivyo ni wakati wa kupiga magoti na kuomba ili amani iliyopo iendelee kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

"Amani ndio kigezo cha kwanza katika uwekezaji wowote, hivyo ni wajibu wa kila mmoja kusimama katika maombi ili nchi iendelee kuwa ya amani, mpaka sasa hivi nchi yetu ina amani jambo ambalo ni la kujivunia, kwa kuwa wenzetu hali hii haipo kama kwetu, niwashukuru kinamama ambao leo mmeamua kukutana pamoja na kufanya maombi haya," alisema.

Awali, akizungumza katika maombi hayo, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dodoma, Dk. Dickson Chilongani, alisema wanawake wanahitaji kutiwa moyo kwani serikali imeshaweka mazingira ya kuwafanya wajisikie huru katika Taifa lao.

"Viongozi wengi wanaokaa kujadili mustakabali wa nchi wanasema wamekubaliana kuwa na 50 kwa 50, hivyo ni jukumu lenu sasa kinamama kusimama imara," alisema Askofu Chilongani.

Katika maombi hayo, ilifanyika harambee kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wasichana ambapo zaidi ya Sh. milioni saba zilipatikana, huku Dk. Mahenge akichangia Sh. milioni 1.5 na pia kuahidi kuwapa wataalamu kwa ajili ya kusaidia kuchora ramani ya ujenzi huo.

# Pwani sasa wahimizwa kuchangamkia fursa elimu

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesema uwapo wa utitiri wa viwanda katika mkoa huo bila kuwa na wasomi, inafifisha uzalishaji malighafi bora zitakapokosa soko.

Ndikilo alisema hayo juzi kwenye kikao cha wadau wa elimu kilichofanyika Mjini Kibaha, kujadili hali ya elimu katika Mkoa huo.

Alisema mkoa huo unaongoza kwa kuwa na wawekezaji wengi kwenye sekta ya viwanda, hivyo ni vema wakazi wake wakahamasisha elimu kwa watoto wao waweze kunufaika na ajira badala ya kuacha nafasi hizo kuchukuliwa na watu wengine.

Mhandisi Ndikilo alisema ni wajibu wa wadau wa elimu kutekeleza nguvu katika kuboresha elimu kwa vitendo ili kufikia uchumi wa kati.

"Uwapo wa viwanda bila elimu itakosesha ushauri katika kupata malighafi bora zitakazotolewa katika viwanda, na pia hapatakuwa na wataalamu wa kutosha kwenye viwanda italazimu kuchukua wanaotoka nje ya mkoa," alisema.

Ndikilo alisema kila mzazi akisimama katika nafasi yake, idadi ya utoro shuleni itapungua pamoja na mimba za utotoni ambazo ni moja ya vyanzo vya umaskini.

Akizungumzia namna anavyokabiliana na utoro shuleni, Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma NJuwayo, alisema tangu Januari mwaka huu ameweka utaratibu wa kutembelea shule za msingi na sekondari kuzungumza na walimu, wanafunzi na wazazi.

Njuwayo alisema, kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo na watumishi idara ya elimu, wameandaa mkakati ambao wamewashirikisha walimu na wazazi kila shule kuwa na utaratibu wa kufanya mitihani ya mara kwa mara pamoja na tunzo kwa wanaofanya vizuri.

Katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2019 na ya sekondari mkoa wa Pwani ulishika nafasi ya 10 kitaifa.

## Waanza ujenzi wa sekondari

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WAKAZI wa eneo la Burka lililopo wilayani Arumeru, wameanza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Burka, ili kuwaepusha watoto wao kutembea umbali wa zaidi ya Km.10 kutokana na kata hiyo kutokuwa na shule ya sekondari.

Akizungumza juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, John Pallangyo, ya kusikiliza kero za wananchi wa jimbo hilo, Elisante Mbise, alisema wananchi wa kata hiyo wameanza ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa kati ya 13 vinavyohitajika, ili watoto wao waondokane na changamoto hiyo.

"Mheshimiwa mbunge kata hii haina sekondari na watoto wetu wanalazimika kutembea umbali mrefu hali inayosababisha kutofanya vizuri darasani na ndiyo sababu tumeamua kujenga shule hii, ili kuondoa changamoto ya kutembea umbali mrefu," alisema.

Neema Robert alisema kutokana na hali hiyo wamekuwa wakiishi kwa hofu juu ya watoto wao wa kike kurubuniwa, kutokana na kutembea umbali huo mrefu na kupata mimba.

"Sisi wazazi hatuna amani kabisa tumejawa na hofu kwa kuwa watoto wetu wakati mwingine wanarubuniwa na watu haswa madereva wa bodaboda, ambao wanawapa lifti wakati wa kwenda ama kutoka shuleni na ndiyo sababu kubwa imetuhamasisha wanawake pia kushiriki kwenye ujenzi wa shule hii," alisema.

Baada ya maelezo hayo, Pallangyo alichangia tofali 1,000, zenye thamani ya Sh. milioni mbili kwa ajili ya ujenzi huo na kuahidi kuendelea kutoa mchango zaidi, ili shule hiyo ikamilike kwa wakati.

Aidha, alisema lengo lake ni kuhakikisha wanafunzi wote katika shule hiyo, wanasoma kwenye mazingira salama na rafiki, kwa kuwa Rais Dk. John Magufuli ameweka mazingira ya kuwezesha wananchi wa kipato cha chini watoto wao wanasoma.

"Sasa lazima sisi wadau tumuunge mkono Rais wetu kwani bila elimu bure watoto wengine wasingesoma kutokana na hali duni za wazazi wao, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa shule hii ili kuipa moyo serikali," alisema.

# Jaji Munuo ataka wanawake kupinga ukatili wa kijinsia

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WANAWAKE mkoani Arusha wametakiwa kuwa mstari wa mbele kupinga ukatili wa kijinsia katika jamii zinazowazunguka, ili kuepusha athari zinazojitokeza katika kizazi kijacho kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Akizungumza jana katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake nchini kwenye Baraza la Biashara la Wanawake wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jaji mstaafu wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Eusebia Munuo, alisema ukatili umebeba dhana kubwa na ni janga linaloathiri maisha ya binadamu kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni na kusababisha familia nyingi, kutawanyika na kuwa na visasi visivyoisha.

Jaji Munuo alisema wanawake wanapaswa kutambua wana mchango wa kupata haki za kibinadamu na kuhakikisha wanasimama kuelimisha jamii juu ya ukatili, ili kupunguza matukio ya ukatili na kuleta ustawi wa maendeleo ya biashara kwa maisha ya baadaye.

"Jamii ikiwa na amani itaanzisha miradi midogo midogo itakayowainua kiuchumi na kuwa na taifa lenye maendeleo, lakini hili linawezekana tu pale watu wanapokuwa na amani sababu kama mtoto au mwanamke amefanyiwa ukatili, familia inahangaika kumponya huyo mtoto au mwanamke hivyo muda wa kujiinua kiuchumi haupo," alisema.

Pia alisema kila mwanamke anapaswa kushirikishwa kwenye maamuzi ngazi zote na baadhi wenye dhana potofu juu ya suala hili waondokane nazo, kwani hazitamjenga mwanamke mpaka kuwezeshwa.

"Chama cha majaji kinatoa msisitizo kwa wanawake kunyanyuka kifikra na tunakumbusha kuwajibika katika nafasi zao na kuondoa malalamiko yasiyo na tija, lakini tunapaswa wanawake kusimama kwa kubuni miradi iyakayotukwamua na kulinda familia zetu kwa amani," alisema.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Liberat Mfumukeko, alisema mwaka 2019 Afrika Mashariki ilizindua mtandao wa mwanamke, wenye wanawake takribani milioni 50 ukiwa na lengo la kuwakutanisha kwa pamoja kwa kutumia tovuti na kupata taarifa, kuhusu fursa za kibiashara kama masuala ya kifedha, masoko na kutatua changamoto za wanawake.

"Kupitia tovuti hii, wanawake wengi wamepata maarifa na kubadilika kwa kuanzisha miradi na kuachana na kuwa tegemezi kwa wenzi wao," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, akimkabidhi jana, Mganga Mkuu wa Zahanati ya Maroroni wilayani Arumeru, Marium Mkwera, kitanda cha wanawake cha kujifungulia, wakati wa ziara yake jimboni humo. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI, ARUSHA**

# Vijana Arumeru wapewa fursa ujasiriamali

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

OFISI ya Mbunge wa Arumeru Mashariki, imefungua dawati la vijana la ujasiriamali katika ofisi hiyo, ili kuwapatia vijana elimu ya kilimo, ujasiriamali na ufugaji, ambayo itawawezesha kujiajiri na kuondokana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Msaidizi wa Mbunge wa Arumeru Mashariki, Hungura Mbwana, wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mbuguni wilayani Arumeru, waliofika kumsikiliza mbunge wao aliyewatembelea kubaini kero walizonazo.

Hungura alisema ofisi ya mbunge imefungua dawati hilo, baada ya kubaini uwepo wa changamoto nyingi za vijana kutokuwa na elimu ya maisha ya mtaani ya kujiajiri.

Alisema dawati hilo, linatoa elimu bure kwa makundi yote ikiwamo vijana, kinamama na kinababa ili kuwasaidia kujiajiri wenyewe na kuachana na kutegemea serikali iwaajiri.

Kiongozi wa dawati hilo, Creino Isangya, alisema uwepo wa dawati hilo, utawasaidia kuwaunganisha vijana pamoja, kwa kutumia kauli mbiu ya kutumia ulicho nacho, kupata ambacho hauna.

Alisema kupitia makundi ya vijana ambayo yataundwa na watu kumi, mara baada ya kupata mradi watakaobuni, ofisi itawasaidia kuwatengenezea andiko la mradi, katiba, usimamizi katika utekelezaji na kuwapatia elimu ya mradi husika.

Awali Mbunge wa Jimbo hilo, John Palangyo, alisema nia ya serikali kutatua changamoto zinazowakabili wananchi, hivyo ataendelea kushiriki kikamilifu katika kutatua changamoto zinazowakabili ili wananchi wake waishi maisha mazuri.

"Mimi kama kiongozi wao nitafurahi sana kuona wananchi wangu wanaishi maisha yenye kuridhisha na mazuri ili mwisho wa uongozi wangu niwe na cha kusema nilichowasaidia," alisema.





# Wabunge wataka posho kwa watumishi KIDH

**Na Mary Mosha, SIHA**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya Ukimwi, dawa za kulevya na kifua kikuu, imeitaka Wizara ya Afya kufikiria kuongeza posho na stahiki nyingine kwa matabibu na watumishi wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibongoto (KIDH).

Imetoa mapendekezo hayo kutokana na mazingira hatarishi wanayofanyia kazi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Oscar Mukasa, akizungumza baada ya kamati yake kutembelea hospitali hiyo, alisema ushauri wao kwa serikali unatokana na majukumu waliyonayo watendaji na watumishi wa hospitali hiyo.

"Lengo la ziara yetu katika mkoa wa Kilimanjaro ni kujionea hali halisi ya utendaji kazi katika vitengo vinavyohusiana na kifua kikuu na Ukimwi ili kuona wapi tunaweza kufanya marekebisho kwa kushirikiana na serikali. Hata hili la posho nalo tumeiona na ndio maana tunaishauri serikali iliangaie upya," alisema Mukasa.

Kwa mujibu wa Mukasa, pamoja na kuyatazama upya maslahi yao pia walishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuwakatia watumishi wa hospitali hiyo bima ya maisha.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Hospitali hiyo, Nicholaus Maro, alieleza kamati hiyo kuwa baadhi ya wafanyakazi wanavyofanya kazi katika mazingira magumu na wapo hatarini kupata magonjwa ambukizi na kutishia usalama wa familia zao.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo walisema ipo haja ya serikalia kuangalia maslahi ya watumishi hao yaongezwe kutokana na hali ngumu ya utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kibongoto, Dk. Riziki Kisonga, alisema miongoni mwa changamoto wanazokabiliana nazo ni pamoja na upungufu wa watendaji 356 katika maeneo mbalimbali ikiwamo madaktari bingwa ambao wanahitajika 15 na kwa sasa wapo watano tu.

"Katika hospitali hii ili tuweze kutoa huduma zetu vyema tunahitaji watumishi 631, lakini hadi sasa tuna watumishi 275 katika ngazi mbalimbali ikiwamo ya madaktari bingwa, madaktari, fiziotherapia, wateknolojia maabara, wahudumu wa afya, wafamasia wahasibu na watu wa Tehama (IT)," alisema Dk. Rizik.

# KCMC sasa yajiandaa kukabiliana na corona

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya KCMC, imeanza kuandaa wataalamu wa kukabiliana na ugonjwa homa ya corona.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Gilliard Massenga, alisema kuwa wako katika hatua ya kuwezesha maabara ya kitafiti ya kupima virusi hivyo.

Dk. Masenga alikuwa akizungumza jana mjini hapa, wakati wa uzinduzi wa safari ya kuelekea Jubilee ya miaka 50 ya hospitali hiyo.

"Niwadokeze tu kwamba hivi sasa KCMC tumeanza kuandaa wataalamu wetu ambao watakuwa tayari kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa corona, tumewaandaa na wako kamili kushirikiana na kamati ya mkoa kudhibiti mlipuko wowote endapo utajitokeza mkoani Kilimanjaro," alisema.

Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya matibabu na kupokea washukiwa wa ugonjwa wa corona hapa nchini ni pamoja na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Hospitali ya kudhibiti magonjwa ambukizi ya Buswelu ya Mwanza na Hospitali ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Ugonjwa huo unaosababishwa na kirusi jamii ya corona (Covid 19), ambacho ni tofauti na virusi vingine vya jamii hiyo ambavyo viliwahi kusababisha milipuko ya ugonjwa unaojulikana kama 'Sars-Cov' mwaka 2003 na Mers-Cov corona virusi mwaka 2013.

Ugonjwa huo huambukizwa kwa njia ya hewa kwa kuingiwa na majimaji yenye virusi kutoka kwa mtu mmoja kwa njia ya kukohoa au kupiga chafya au kwa kugusa majimaji au makamasi kutoka kwa mgonjwa aliyethibitishwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Dalili za ugonjwa huo, huanza kuonekana kati ya siku moja hadi 14 tangu kupata maambukizo.

Akizungumza katika maandalizi hayo, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, aliwataka wafanyakazi wa hospitali hiyo kuongeza ufanisi wa kazi katika kutoa huduma bora kwa wagonjwa ili kuendelea kuifanya hospitali hiyo kuwa hospitali bora nchini.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakishiriki maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani juzi, kwa kuchimba msingi wa ujenzi wa darasa moja katika Shule ya Msingi Muheza Estate. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri avionya vituo vya kulea watoto

**Na Mary Mosha, SAME**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezeji), Angela Kairuki, ameshauri vituo na taasisi zinazolea yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, kuacha kutumia vivuli vya watoto wao kama njia ya kujipatia fedha.

Kairuki alieleza kuchukizwa na hali hiyo, alipotembelea baadhi ya nyumba za kutunza watoto waishio katika mazingira hatarishi na wenye ulemavu katika Wilaya ya Same.

Alisema kama jamii itawekeza kwa watoto hao na kuacha kujitafutia kipato kupitia wao, ni wazi kuwa ustawi wa kundi hilo unaweza kuwa na faida ni kubwa baadaye.

Aliitaka jamii kuchukua jukumu la kuwalea watoto hasa waishio katika mazingira hatarishi ili kutimiza matakwa ya Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Alisema hayo baada ya kuona hali ilivyo katika vituo hivyo, hasa Kituo cha Rafiki Center na kutoa kilogramu 150 za sabuni ya unga, pampasi za watoto zaidi ya 1,176 na mchele kilo zaidi ya 100.

Pia waziri huyo akiwa katika kituo cha watoto wenye ulemavu cha Mama Kelvin, alitoa kilo 150 za sabuni ya unga, pampasi zaidi ya 1,300 na Sh. 500,000.

Ali Shehoza, Ofisa Ustawi wa Jamii na mkuu wa kitengo cha malazi na makuzi wilayani Same, alisema hali ya utelekezaji wa watoto ni kubwa na katika kipindi cha mwaka 2019 walipata kesi zaidi ya 1,000.

"Hali ya utelekezaji wa watoto katika wilaya yetu ni kubwa na hii ni kutokana na kipato na hali ya uchumi, lakini wengine hufanya makusudi kushindwa kutekeleza majukumu yao na kamati ya ulinzi na usalama katika kuwashurutisha kutekeleza majukumu yao," alisema Shehoza.

Ritha Mmbaga, mkurugenzi wa kituo cha malezi cha Rafiki Center, alisema katika wilaya hiyo changamoto ya utelekezaji ya sheria ya mtoto ni mdogo hali inayopelekea watoto kuletekezwa na kuachwa kwenye mazingira hatarishi jambo ambalo linaweza kusababisha mtoto kutopeza maisha.

Naye Mtawa wa Kanisa Katoliki Jimbo la Same, Marypaulina Edward ambaye ni msimamizi msaidizi wa kituo cha watoto wenye ulemavu wa viungo na utindio wa ubongo cha Mama Kelvin, alisema wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa eneo la mazoezi baada ya watoto hao kufanyiwa upasuaji pia uhitaji wa watoto wenye ulemavu ni mkubwa kuliko uwezo wa kituo na kuiomba serikali kuangali uwezekano wa kuwasaidia.

NIPASHE JUMATATU MACHI 9, 2020
Nipashe

# Spotika



VIWANGO MASTRAIKA VIWEMBE LIGI 5 ULAYA UK. 14



# MTIFUANO...

Beki wa Arsenal, Sokratis Papastathopoulos katika harakati za kuucheza mpira dhidi ya mshambuliaji wa West Ham, Sebastien Haller (kulia), kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi na Gunners kushinda 1-0. **HABARI UK. 29**

## ISIKUPITE

TANGU kuanza kwa msimu uliopita, Arsenal imefunga mabao 16 kwenye ligi kupitia wachezaji wanaotokea benchi, na hakuna klabu katika Ligi Kuu England iliyozidi idadi hiyo kwa watokea benchi. Alexandre Lacazette amefunga mabao manne kati ya hayo ambayo mengi zaidi ya yaliyopachikwa nyavuni na wachezaji wengine.

SOKA




HAALAND

# VIWANGO MASTRAIKA VIWEMBE LIGI TANO ULAYA

**DORTMUND,** Ujerumani

WASHAMBULIAJI ambao wana mafanikio mbele ya goli ndio wanaotakiwa na timu yoyote duniani.

Wale wenye nafasi nzuri na kubwa zaidi ya kufunga mabao ndio wanaotakiwa zaidi kama vile Robert Lewandowski, Mauro Icardi na wengine wengi. Makala haya yanakuchambulia washambulia wakali na wenye viwango vya ubora mbele ya goli katika Ligi Kuu 5-bora barani Ulaya...

**5. LUCAS PEREZ | LA LIGA | ASILIMIA 29.4**

Mshambuliaji huyu wa timu ya Alaves, Lucas Perez anashika nafasi ya tano kwa kuwa bora zaidi mbele ya goli kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga na anafurahia matunda yake msimu huu kwenye ligi ya nyumbani kwake. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 31, alisajiliwa na Arsenal kwa ajili ya msimu wa 2016-17 na akawa na msimu miwili isiyo na mafanikio pale kwenye dimba la Emirates. Akapelekwa kwa mkopo Deportivo La Coruna na baadaye West Ham, lakini Alaves wakamnunua kwa euro milioni 2.5. Alaves kwa sasa wapo nafasi ya 14 kwenye msimamo wa La Liga, wakiwa pointi nane juu kutoka kwenye mstari wa kushuka daraja.

Hata hivyo, Perez yupo kwenye kiwango cha kuvutia zaidi, kwani katika mechi 24 (sawa na dakika 1,759), raia huyo wa Hispania amefunga mabao 10 yote akiyapata ndani ya dakika 175.9 huku akiwa na pasi za mwisho tano. Na ana asilimia 29.4.

**4. JAMIE VARDY | EPL | ASILIMIA 29.8**

Mshambuliaji huyu wa Leicester City, Jamie Vardy amekuwa mmoja wa washambuliaji wanaovutia zaidi kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu licha ya sasa kukabiliwa na ukame wa mabao. Muingereza huyo amekuwa mmoja wa wanaoibeba Leicester ikiwa inapigania kumaliza kwenye nne bora. Kwa sasa Vardy anaongoza kwenye orodha ya kufunga mabao kwenye EPL akiwa sambamba na nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang ambao wote wametikisa nyavu mara 17, kabla ya mechi za mwishoni mwa wiki. Kwenye orodha hii ya viwango ana asimilia 29.8, huku akiwa na pasi za mwisho nne.

**3. MAURO ICARDI | LIGUE 1 | ASILIMIA 31.4**

Mchezaji wa zamani wa Inter Milan, Mauro Icardi alihamia kwa mkopo pale Paris Saint-Germain kipindi cha majira ya joto kilichopita baada ya kocha mpya Antonio Conte kutokuwa na mpango naye. Hata hivyo, raia huyo wa Argentina amekuwa na mafanikio makubwa zaidi kwenye kikosi cha kocha Thomas Tuchel.

Zao hilo la kituo cha kulelea vipaji cha Barcelona pale La Masia, amefunga mabao 11 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa msimu huu katika mechi 19 (sawa na dakika 1,250) na ana pasi za mwisho tatu. Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Icardi amefunga mabao matano katika mechi sita katika kila dakika 80. Ana asilimia 31.4.

**2. FELIPE CAICEDO | SERIE A | ASILIMIA 32**

Mshambuliaji huyu wa Lazio, Felipe Caicedo bila shaka ni mmoja wa wachezaji anayewashangaza wengi kwa kiwango chake msimu huu. Nyota huyo wa zamani wa Manchester City raia wa Ecuador alinunuliwa na Lazio kwa mkataba wa miaka mitatu akitokea kule Espanyol kwa ada ya euro milioni 2.5.

Ingawa mchezaji mwenzake, Ciro Immobile amekuwa kinara wa mabao, Caicedo amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi. Msimu huu amecheza mechi za Ligi Kuu 20, huku 11 akianza na ana mabao nane na pasi za mwisho mbili. Akifunga bao moja kila baada ya dakika 108. Ana asilimia 32.

**1. ERLING HAALAND | BUNDESLIGA | ASILIMIA 56.3**

Kinda, Erling Braut Haaland kwa sasa dunia ipo mikononi mwake baada ya kuwa na msimu bora zaidi. Mchezaji huyu wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 19, ambaye alikuwa na Manchester United ya Ole Gunnar Solskjaer, aliamua kuondoka pale RB Salzburg na kutua Borussia Dortmund kule kweye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Haaland amecheza mechi sita (sawa na dakika 395) kwenye Bundesliga msimu huu na kufunga mabao tisa, ikiwa ni sawa na dakika 44 kwa bao moja. Kiwango chake cha uchezaji kikamfanya kupewa tuzo ya mchezaji bora wa mwezi wa Bundesliga mwaka 2020. Nyota huyo wa zamani wa Molde kiwango chake ni asilimia 56.3 na kumfanya kuwa mshambuliaji anayeongeza kwa kuwa hatari zaidi mbele ya goli katika Ligi 5-bora za Ulaya.

**JE, WAJUA?**



MOHAMED Salah ni mchezaji wa kwanza Liverpool kufunga mabao 20 kwenye mashindano yote katika misimu mitatu mfululizo tangu Michael Owen alipofanya hivyo msimu wa 2000-01 na 2002-03.

## MICHEZO



Idd Selemani Nado akiwatoka mabeki wa KMC kwenye moja kati ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

# NADO ALIVYO MWIBA KWA SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BAO alilolifunga dakika ya 50 kwenye mechi kati ya timu yake ya Azam FC dhidi ya Simba, limemfanya mchezaji Idd Selemani 'Nado' kuendelea kuwa mwiba mchungu anapokutana na timu kongwe za Simba na Yanga.

**Jumatano Februari 4, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa, nusura alitie jongoo pilau la Simba alipofunga bao la kusawazisha na kama si bao la Meddie Kagere dakika ya 71, huenda ngoma hiyo ilikuwa inakwenda sare ya mabao 2-2.**

Pamoja na Simba kushinda mabao 3-2, lakini Nado alionekana kuisumbua ngome ya Simba hatimaye kupata bao la kusawazisha, kabla ya mambo kuharibika baadaye.

Lakini hii si mara ya kwanza Nado kuwatungua Simba, kwani imekuwa ni kawaida yake kuwafunga makipa wa timu hizi kubwa kila anapokutana nazo akiwa na timu anayoichezea.

Ni mchezaji aliyesajiliwa na Azam FC akitokea Mbeya City mwaka 2017. Kabla ya kujiunga na timu hiyo alitokea mtaani kwenye michuano ya Ndondo Cup na msimu wake wa kwanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2017/18, akiichezwa Mbeya City misimu miwili, akahamia Azam msimu huu wa ligi. Lakini kwa sasa ni mcheza wa timu ya Taifa, Taifa Stars.

Kwenye michuano ya Ndondo Cup, alikuwa akiichezea timu ya Manzese United na kuiwezesha timu hiyo kutwaa kombe hilo, lakini ni mmoja wa wachezaji ambao waliwavutia makocha wengi, hatimaye kupelekwa mkoani Mbeya.

Haya ni mabao yake aliyozifunga Simba na Yanga tangu aanze kucheza Ligi Kuu akitokea Ndondo Cup.

**1. MBEYA CITY 1-1 YANGA (2017/18)**

Nado alianza kuthibitisha kuwa ana uwezo wa kucheza Ligi Kuu licha ya kutoka kwenye mechi za mchangani, aliposawazisha bao dakika ya 90 kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya dhidi ya Yanga.

Awali Yanga ilipata bao dakika ya 57 likifungwa na Rafael Daudi, lakini wakati kila mmoja akidhani Yanga ingeshinda mechi, kiungo huyo mshambuliaji alisawazisha bao, ngoma ikaisha kwa bao 1-1. Mechi hiyo ilichezwa Aprili 22, 2018. Kipa aliyetunguliwa siku hiyo alikuwa ni Youthe Rostand.

**2. MBEYA CITY 1-2 YANGA (2018/19)**

Ilikuwa ni Ligi Kuu ya msimu wa 2018/19, akiendelea kuichezea Mbeya City, Nado alifunga bao kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, timu yake ikicheza tena dhidi ya Yanga.

Mechi hiyo ilichezwa Desemba 29, mwaka 2018 kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya. Alifunga bao dakika ya 24, likiwa la kusawazisha baada ya Heritier Makambo kufunga bao dakika ya 17. Hata hivyo, Mkongomani huyo, ambaye kwa sasa anaichezea Horoya ya Guinea, alifunga bao la pili kwa Yanga dakika ya 41 na mechi ikamalizika kwa Yanga kushinda mabao 2-1.

Kwenye mechi hiyo Nado alimtungua Ramadhani Kambwili, ambaye ndiyo alikuwa amesimama langoni.

**3. MBEYA CITY 1-2 SIMBA (2018/19)**

Pia hii ilikuwa ni mechi ya msimu wa 2018/19, lakini ikicheza na Simba kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu. Mechi ilichezwa Mei 3, Simba ikiichakaza Mbeya City mabao 2-1.

Hata hivyo, Nado ndiye aliyeanza kuwaamsha Simba usingizini alipofunga bao dakika ya 21, lakini baadaye mabao ya Jonas Mkude na Meddie Kagere yalibadilisha sura ya mchezo mzima. Aliyetunguliwa golini siku hiyo alikuwa ni Deogratius Munishi 'Dida' ambaye kwa sasa anaichezea Lipuli FC aliyojiunga kipindi cha dirisha dogo.

**4. AZAM 2-3 SIMBA (2019/20)**

Nado aliendeleza rekodi yake nzuri kwa kufunga bao Jumamosi iliyopita, lakini pia aliendeleza rekodi yake mbaya kwani pamoja na kufunga mabao, lakini hakuna hata mechi moja ambayo timu yake imeondoka na ushindi zaidi ya sare moja na vipigo vitatu, mara mbili kwa Simba na moja kwa Yanga. Ila safari hii aliyemtungua akiwa golini ni Aishi Manula.

**NJE YA UWANJA**

TANGU aanze kucheza michuano ya Kombe la FA kwa mara ya kwanza Januari 2014, Willian amehusika moja kwa moja katika mabao 16 Chelsea (akifunga 11, na kutoa pasi za mwisho tano), ikiwa ni mabao matano zaidi ya mchezaji yeyote klabuni hapo kuanzia wakati huo. Lakini Willian hadi sasa amefunga jumla ya mabao 24 akiwa nje ya boksi tangu alipoanza kuichezea Chelsea kwa mara ya kwanza Septemba 2013.



# KLABU 10 ZISIZOFUNGIKA EPL ZILIVYOANGUKIA PUA




**LONDON,** England

LIVERPOOL ya kocha Jurgen Klopp imekuwa imara siku hadi siku kwenye kampeni ya Ligi Kuu ya England na kukataa kuachia pointi huku ikitawala kwenye kinyang'anyiro hicho hadi sasa.

**Imeonyesha kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu na kuonekana kuwa moja ya timu bora zaidi kwa sasa kwenye historia ya soka la Uingereza.**

Liverpool kwa sasa ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kulitwaa taji la Ligi Kuu ya England kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 30.

Imeweka rekodi ya kuwa moja ya timu ambayo haijapoteza mchezo kwa muda mrefu zaidi kwenye ligi hiyo.

Hadi sasa Liverpool imecheza mechi 44 kwenye Ligi Kuu bila kupoteza na makala haya yanakuchambulia timu 10 ambazo zina rekodi ya kutopoteza mechi kwa muda mrefu zaidi kwenye historia ya Ligi Kuu na namna gani zilivyofikia mwisho.

**10. NOTTINGHAM FOREST (1995) – MECHI 25**

Nottingham Forest ni moja ya klabu kongwe zaidi nchini England na moja ya klabu sita za Uingereza zilizoshinda taji la Ulaya au Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ingawa kwa sasa ipo kwenye Ligi Daraja la Pili, lakini kuna wakati ilikuwa moja ya klabu bora zaidi.

Mabingwa hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 1977-78 walifurahia wakati wao bora wa kutopoteza mechi kwenye Ligi Kuu ya England mwaka 1995. Cha kufurahisha ni kwamba ndio kwanza walikuwa wamepanda daraja.

Februari mwaka 1995, huku ukiwa umebakia nusu ya msimu wa 1994-95 kumalizika, walifikisha mechi 25 bila kufungwa.

Lakini mwisho wao ulikuwa mbaya baada ya kuchezea kichapo safi kutoka kwa waliokuwa mabingwa watetezi, Blackburn Rovers pale kwenye dimba la Ewood Park, ambapo walichapwa 7-0 Novemba 18, mwaka 1996.

**9. MANCHESTER UNITED (2016-17) – MECHI 25**

Manchester United ilifurahia moja ya misimu yake bora zaidi baada ya zama za Sir Alex Ferguson msimu wa 2016-17 chini ya Jose Mourinho. Waliweza kutwaa mataji matatu tofauti.

Kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Chelsea ndicho kilimaliza rekodi yao ya kutofungwa mechi 25.

Kipigo hicho cha watoto hao wa London kikapelekea kichapo kingine kutoka kwa timu nyingine ya London wakati walipofungwa na Arsenal 2-0 pale Emirates Mei 7, 2017.

Baada ya kutozoea vichapo kwa mechi 25, walipoteza mechi mbili mfululizo na nyingine zikaja wakati wakifungwa na Tottenham Hotspur 2-1 pale kwenye dimba la White Hart Lane.

**8. MANCHESTER UNITED (2010-11) – MECHI 29**

Manchester United ni klabu yenye mafanikio zaidi katika historia ya Ligi ya soka la Uingereza, ndio maana wametokea mara nyingi kwenye orodha hii. Katika msimu wa 2010-11 'Mashetani Wekundu' hao walifikisha mechi 29 bila kupoteza.

Wolverhampton Wanderers ndio timu iliyowazuia Man United kufikisha mechi 30 bila kufungwa na hiyo ilikuwa Februari 5 mwaka 2011. Wolves iliyokuwa nafasi za chini ilitoka nyuma na kushinda 2-1.

**7. CHELSEA (2007-08) – MECHI 29**

Chelsea ni klabu nyingine iliyopo kwenye orodha hii. Blues hao nao walijiwekea historia ya aina yake kwenye Ligi Kuu ya England.

Msimu wa 2007-08 ulionekana kuwa wenye mafanikio makubwa zaidi kwao kwenye historia, walikuwa wanapewa nafasi kubwa ya kulitwaa taji la Ligi Kuu hadi siku ya mwisho na walishika nafasi ya pili kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na Ligi Kuu ya England. Na huo ndio ulikuwa msimu wao wa kwanza kumaliza bila taji lolote kwa kipindi cha miaka minne.

Wakiwa chini ya kocha Luis Felipe Scolari waliweza kufikisha mechi 29 bila kufungwa kwenye Ligi Kuu.

Lakini walikuwa Liverpool ambao ndio waliwatibulia rekodi yao pale kwenye dimba la Stamford Bridge wakati walipowafunga bao 1-0, Oktoba 26, mwaka 2008.

**6. MANCHESTER UNITED (1998-99) – MECHI 29**

Manchester United waliingia kwenye vitabu vya historia mwaka 1999 baada ya kutwaa taji la Ligi Kuu, FA, na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa msimu mmoja.

Rekodi yao ya kutopoteza mchezo ilimalizwa Oktoba 3, mwaka 1999, wakati Chelsea wakiwa nyumbani kwenye dimba lao la Stamford Bridge walicheza kwa kiwango cha juu zaidi na kuwafumua mabao 5-0. Licha ya kichapo hicho, lakini waliweza kutetea taji lao la Ligi Kuu msimu uliofuata.

**5. MANCHESTER CITY (2017-18) – MECHI 30**

Manchester City ilikuja kutawala Ligi Kuu ya England wakati walipotwaa taji msimu wa 2011-12. Lakini baada ya kutua kwa Pep Guardiola wakafanya jambo hilo kuwa la kawaida kwao.

Timu hiyo ilikuwa kwenye kilele cha mafanikio msimu wa 2017-18 na kujiwekea rekodi kadhaa msimu huo, ikiwamo pointi nyingi zaidi (100), pointi nyingi za ugenini (50), ushindi mechi nyingi (32), ushindi mechi nyingi za ugenini (16), mabao mengi zaidi (106), tofauti bora zaidi ya mabao (+79) na ushindi mfululizo (18).

Lakini baada ya mechi zao 30 bila kupoteza walikutana na kichapo kutoka kwa Liverpool na wakachezea 4-3 Januari 14, mwaka 2018 pale kwenye dimba la Anfield.

**4. ARSENAL (2001-02) – MECHI 30**

Tangu alipoichukua Arsenal katikati ya msimu wa 1996-97, Arsene Wenger aliwabadilisha 'Washikabunduki' hao kuwa washindani wa kweli wa taji la Ligi Kuu.

Msimu wa 2001-02, waliwazidi kete wapinzani wao Manchester United na kushinda taji la Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi saba.

Lakini mwisho wao ulifikia pale Wayne Rooney aliyekuwa na umri wa miaka 16 kufunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu dakika ya 90 pale kwenye dimba la Goodison Park na kuwafanya Everton kuondoka na ushindi wa 2-1.

**3. CHELSEA (2004-05) – MECHI 40**

Jose Mourinho alijitangaza yeye mwenyewe kwenye Ligi Kuu ya England baada ya kuing'arisha Chelsea. Katika msimu wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu ya England kama kocha, aliwaongoza Blues hao kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu msimu wa 2004-05, huku akivunja umwamba wa Arsenal na Manchester United.

Chelsea ilicheza mechi 40 za Ligi Kuu bila kupoteza na kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya utawala wa soka la Uingereza.

Lakini umwamba wao ulikuja kumalizwa na Manchester United pale kwenye dimba la Old Trafford Novemba 6, mwaka 2005 wakati walipocheza kichapo cha bao 1-0.

**2. LIVERPOOL (2019-HADI SASA) – MECHI 44**

Baada ya kuwa na mafanikio mazuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita kwa kulibeba taji hilo, ilitarajiwa kwamba Liverpool itaanza msimu mpya wa Ligi Kuu kwa ubora zaidi.

Hadi sasa Liverpool imecheza mechi 44 bila kupoteza, huku wakiwa wameacha pointi moja tu kwa Manchester United.

Lakini waliduwazwa na Wartford wakati walipocheza kichapo cha mabao 3-0 mwanzoni mwa mwezi huu na kumaliza rekodi yao ya kucheza mechi nyingi bila kufungwa

**1. ARSENAL (2003-04) – MECHI 49**

Hadi sasa, Arsenal ndio inayoshikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi za Ligi Kuu ya England bila kufungwa na walifanya hivyo msimu wa 2003-04. Wakati huo wakiwa na wachezaji wakali kama Thierry Henry, Dennis Bergkamp, Patrick Viera, Ashley Cole na Fredrick Ljungberg.

Walicheza mechi 49 bila kupoteza, lakini Oktoba 24, mwaka 2004, Manchester United ndio wakawatibulia rekodi kwa kuwachapa mabao mawili kwenye mchezo uliopigwa pale kwenye dimba la Old Trafford.

## Nukuu


"Kila mchezaji duniani anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na kama timu inashindwa kufuzu kwenye mashindano hayo, ni ngumu kuwashawishi wachezaji wakubwa kubaki au kusajili wapya. Nafikiri hakuna namna," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akibainisha klabu hiyo kuwa kwenye wakati mgumu kusajili wachezaji wakubwa kama watashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Mbappe yupo katika kikosi cha awali cha wachezaji 80 kwa ajili ya Michezo ya Olimpiki, kilichoandaliwa na kocha Sylvain Ripoll. Orodha hiyo itapungua na kubaki 50, kabla ya kuchujwa na kuwa 18 + wanne wa akiba. Ana umri unaomwezesha kwenda [U-23]. Kama ilivyo kwa wachezaji wote wa umri wake ambao wana vipaji, kwa hiyo yupo kwenye orodha," **Rais wa Shirikisho la Soka Ufaransa (FFF), Noel Le Graet.**



"Mbio za Ligi Kuu ni ngumu, tumeshinda taji moja na bado tupo kwenye mbio za mataji mawili hivyo, tumejipanga na tupo tayari kwa ushindani huo. Ni ngumu kushinda kwa miaka mitatu mfululizo na hicho ndicho tulichokifanya tunachotakiwa kufanya ni kuendelea kupambana kushinda mataji," **Raheem Sterling baada ya Manchester City kuifunga Aston Villa 2-1 kwenye fainali ya Kombe la EFL.**



## Michezo



Bakari Mwamnyeto (jezi nyekundu) akiwa katika majukumu yake dimbani dhidi ya mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa.

# SAFARI YA MWAMNYETO AKIBISHA HODI SIMBA

**Na Saada Akida**

ACHANA na ubora wake uwanjani huku akimudu kucheza nafasi zaidi ya moja, lakini unapokuja upande wa kuimarika kimwili hakika huwezi kuacha kumtolea jicho beki huyu kisiki wa Coastal Union na timu ya Taifa, Taifa Stars, Bakari Nondo Mwamnyeto.

**Mtazame alivyojengeka kimwili na kubarikiwa umbo la kiuchezaji tofauti na wachezaji wengi wa Tanzania ambao kwa hakika wanakosa sifa hiyo, pasi na shakautakubali wasifu wake kwa nje.**

Wachezaji wa miaka ya nyuma walikuwa na maumbo makubwa na vimo virefu na kwa kiasi fulani Tanzania ilifanikiwa kufanya vizuri hata kufuzu fainali za Afcon nchini Nigeria mwaka 80.

Kwa sasa jina lake limetawala midomoni mwa mashabiki na wadau wengi wa mchezo wa soka huku akihusisshwa kutakiwa na klabu mbili kongwe za mitaa ya Kariakoo Simba na Yanga , baada ya kuonyesha kiwango bora akiwa na kikosi cha Coastal chini ya kocha Juma Mgunda.

Ubora wake ulimshawishi kocha wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, kuanza kumuita kwenye kikosi chake kwenye mechi ya kuwania kufuzu michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), lengo likiwa ni kuchota uzoefu kutoka kwa waliomtangulia.

Akiwa na kikosi cha Stars, beki huyo ameonyesha uwezo mkubwa katika mechi mbili za kimataifa dhidi ya Burundi na Sudan na kuwa miongoni mwa wachezaji waliotoa mchango mkubwa kwa Tanzania kufuzu fainali za CHAN.

Mwamnyeto amekuwa hodari kuokoa mipira ya juu na chini, lakini anatumia akili pale anapopambana na washambuliaji hatari wa timu pinzani.

Beki huyo amezungumza na mwandishi wa makala haya kuhusu masuala mbalimbali ya maisha yake na safari yake ya kisoka hadi sasa anapoitumikia Coastal Union.

**HISTORIA YA TIMU ALIZOTOKA**

Mwamnyeto anasema amecheza timu ya Majengo, baada ya muda kuna shemeji yake aliyekuwa mchezaji wa zamani wa Coastal, Kasa Musa alimchukuwa na kumpleka katika timu hiyo kwa ajili ya majaribio.

"Siku aliyonipeleka aliniambia natakiwa kuonyesha uwezo hakuwaambia viongozi na benchi la ufundi kama alinipeleka pale, baada ya majaribio nilifanikiwa na kucheza msimu mmoja timu ilishuka daraja na baadaye tulifanikiwa kuipandisha hadi sasa," anasema.

**NAFASI ANAZOMUDU KUCHEZA**

Mlinzi huyo anasema mbali na nafasi ya beki anayocheza na kuonekana bora pia ana uwezo mkubwa wa kucheza kama kiungo mkabaji, namba sita, kutokana na awali kucheza nafasi hiyo kabla ya kuhamia beki.

Kuhusu kuichezea Taifa Stars, anasema: "Hakuna maslahi makubwa kuitumikia Stars, ni kupata uzoefu wa kucheza michuano mikubwa, kwa upande wangu sijawahi kucheza, mechi ngumu kwa sasa bado ipo katika akili yangu dhidi ya Equatorial Guinea," anasema Mwamnyeto.

**COASTAL KUMBANIA KWENDA SIMBA, YANGA**

Mwamnyeto anasema: "Sijajua kutokana na mkataba wake bado ni wa mwaka mmoja, hivyo huenda timu hizo ziliendа kufanya mazungumzo na uongozi wa timu inayonimilika na kushindwa maslahi.

"Kazi yangu ni kufuata maelekezo kutoka kwa anayenisimamia ambaye ni Kasa naye huzungumza na viongozi wa timu yangu ya Coastal ambayo bado nina mkataba nayo."

**YUPO COASTAL KWA MKOPO**

Inadaiwa kwamba Simba wameshamalizana na beki huyo na sasa anaitumikia Coastal kwa mkopo, lakini Mwamnyeto anakanusha taarifa hizo.

**KUONDOKA COASTAL**

Mlinzi huyo anasema yupo tayari kuondoka endapo timu itakayomhitaji itafikia maslahi yake kwa sababu kucheza mpira ndio kazi yake na atacheza kwa kiwango cha juu.

Mwamnyeto anasema kwa mabeki ambao anawakubali ni Erasto Nyoni akitamani kucheza kwa kiwango cha nyota huyo wa Simba, kwa washambuliaji ni wengi wanaocheza ambao mara nyingi amekuwa wakimpa shida dimbani.

**NDOTO ZAKE KISOKA**

Mlinzi huyo anasema kiu yake kubwa ni kuona siku moja anabeba Ubingwa wa Tanzania Bara, akiwa na kikosi cha Coastal Union, kwa sababu ni timu ya nyumbani kwao na amekuwa na mafanikio makubwa tangu ajiunge nayo.

Mbali na ubingwa, kingine ambacho Mwamnyeto anakipa nafasi ni kupata mafanikio ya kifedha ili kumudu maisha yake ya kila siku pamoja na kuwasaidia wazazi wake, lakini siku moja angependa kupata nafasi ya kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania.

**NAJUA WAJUA**



KIPIGO cha mabao 2-0 Liverpool ilichokipata dhidi ya Chelsea Jumanne iliyopita kwenye michuano ya Kombe la FA, kinaifanya miamba hiyo ya Anfield kwa sasa kupoteza mechi tatu mfululizo kwenye mashindano yote kwa mara ya kwanza tangu Novemba 2014.

SOKA




# VAR ILIVYOKUWA TATIZO BADALA YA SULUHISHO

**LONDON,** England

TANGU kuanzishwa kwa mfumo mpya wa mwamuzi msaidizi kupitia video (VAR), maswali na changamoto yamekuwa mengi kuliko majibu na suluhisho.

**Katika Ligi Kuu ya England kwa mfano, klabu ya Manchester United in aonekana kunufaika zaidi na mfumo huo wa VAR kuliko timu yoyote na hivyo kuibua maswali kwamba inapendelewa.**

Makala haya ya gazeti la Daily Mail inachambua kwa namna gani imekuwapo migongano mingi juu ya matumizi ya VAR, kwa sababu utata umekuwa mwingi juu ya uamuzi husika, ambapo pia mtiririko wa mechi hukosekana ladha yake pale mwamuzi wa kati anapokwenda kuwasiliana na VAR.

Pamoja na makosa yaliyokuwapo uwanjani kwa waamuzi, iwe wa kati au wasaidizi wake (washika vibendera) wachezaji, makocha, mashabiki na wadau wengine wanaonekana kukerwa zaidi na VAR.

Mabao yamekataliwa ambayo kwa mitazamo ya wengi yalionekana ni halali na mmoja wa walalamikaji ni Kocha wa Chelsea, Frank Lampard pamoja na wengine na sasa kocha wa zamani wa Arsenal ambaye ni Ofisa wa Maendeleo ya Soka Duniani wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), Arsene Wenger, naye ameona kuna walakini.

Anasema kwamba hakuna sababu pale mshambuliaji wa mwisho anapofanya kazi yake, kisha akamzidi beki kwa kiungo kwa kiasi kidogo tu, basi anachukuliwa ameotea.

Mchezaji wa Liverpool, Roberto Firmino alipatwa na VAR kuwa ameotea kwa sababu tu bega lake kimahesabu lilizidi lile la mlinzi wa Aston Villa.

VAR inaharibu mtiririko wa mechi na hivyo utamu unaoambatana nao, mbaya zaidi ni pale uamuzi unapokuwa mbaya usioendana na ukweli wa mambo yaliyotokea uwanjani.

Uamuzi unaotolewa na VAR mara nyingi umekuwa ukiacha watu wa mpira katika wakati mgumu, ambapo hata wale wanaokuwa wamependelewa hujihisi kwamba haki haikutendeka.

Kwenye mechi ya Ligi Kuu baina ya Manchester City na Sheffield United kwenye Uwanja wa Etihad nako kulikuwa na mambo; malalamiko yakawa makubwa dhidi ya VAR, lakini hayakusikilizwa.

Sheffield United au Blades kama wanavyojulikana, walishatia mpira kimiani kupitia kwa Lys Mousset, lakini VAR ikakataa kwa maelezo kwamba mfungaji alikuwa ameotea.

Lakini jamaa hao walilalamikia bao la kuongoza la Sergio Aguero, kwa sababu mwamuzi Chris Kavanagh alionekana kumzuia John Fleck wakati wa utengenezaji wa bao hilo.

Kocha wa Sheffield, Chris Wilder aliondoka uwanjani akiwa ameshaungana na waamuzi wanaolia dhidi ya VAR kwenye wikiendi nyingine ambayo VAR imezidi kulalamikiwa.

Wilder alikataa kueleza ni kipi alichokuwa akijadiliana na Kavanagh kwenye chumba cha waamuzi baada ya mechi hiyo, lakini kwa ujumla alionekana kusikitishwa sana na waamuzi hao.


Alisema alikuwa anajivunia wachezaji wake na timu kwa jinsi walivyojitahidi.

"Ikiwa unapoteza mechi, kuna njia ya kuipoteza. Lakini nimeiona timu yangu na hali ambayo tumekuwa nayo. Je, tulidhani kwamba tungesonga nayo hadi mwisho wa Desemba? Sidhani," anasema Wilder.

"Tumeongezeka katika kujiamini na ujasiri. Ni upinde mkubwa wa kujifunza. Hawa jamaa (Manchester City) wana wachezaji mahiri sana. Klabu mbili hizi ni sawa na tofauti ya miaka miwili ya mwanga kwa umbali; hawakuwa hivyo miaka kadhaa iliyopita.

"Klabu moja haikusonga mbele kwa kasi ambayo City walikuwa nayo, lakini sidhani kwamba pale uwanjani pengo lilionekana kubwa kivile kwa mujibu wa ukali wa mchezo. Timu yangu iliamua kujaribu na ndicho kitu cha msingi tulicho nacho," anasema.

David De Gea amefanya makosa saba yalisababisha moja kwa moja wapinzani kupata bao kwenye Ligi Kuu tangu kuanza kwa msimu uliopita, hivyo kuungana na Jordan Pickford wa Everton, Martin Dubravka (Newcastle United) na Bernd Leno wa Arsenal, kuwa makipa wanaoongoza katika takwimu hiyo ya makosa.



NDANI YA 18



LIVERPOOL ya kocha Jurgen Klopp imekuwa imara siku hadi siku kwenye kampeni ya Ligi Kuu ya England na kukataa kuachia pointi huku ikitawala kwenye

Uk. 16&17

# SABABU 3 ARSENAL KUMFUATA UPAMECANO



**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal kwa sasa inapita kwenye kipindi cha mpito chini ya Mikel Arteta na wanaonekana kwa kiasi fulani kuimarika. Hata hivyo, 'Washikabunduki hao wasipoyafanyia kazi matatizo yaliyopo kwenye kikosi chao, hawatakuwa na uwezo wa kutoa changamoto kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya England haraka hivi karibuni.

Moja ya matatizo yao makubwa ni kukosekana kwa 'moyo' kwenye safu yao ya ulinzi na matokeo yake miamba hao wa London Kaskazini watalazimika kuingia sokoni wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

Arsenal wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kusajili walinzi kadhaa kwa kipindi cha miezi michache na tayari wameanza kuangalia beki gani wa kati wa kumsajili kwa ajili ya msimu mpya ujao.

Katika makala haya tunaangalia sababu tatu kwa nini wakimsajili Dayot Upamecano anaweza kuwa suluhisho la kudumu pale kwenye dimba la Emirates.

**3. NI BORA KATIKA KUMILIKI MPIRA**

Chini ya Arteta, Arsenal imeonyesha uwezo wa kumiliki mpira na kucheza kutoka nyuma, maana yake ni kwamba 'Washikabunduki' hao si tu watakuwa wanawania walinzi wazuri, lakini watakuwa wanaangalia beki wa kati ambaye ana uwezo wa kumiliki mpira na kitu hicho Upamecano anacho.

Klabu anayoichezea ya RB Leipzig mara zote inacheza mpira kutoka nyuma na ubora wake wa kumiliki mpira umeshuhudiwa. Msimu huu kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ana wastani wa kuwa na mpira mara 90 kwa mchezo mmoja, huku pasi zake zikiwa na uhakika wa asilimia 90. Amekuwa mchezaji nguzo na muhimu kwa timu yake.

Hivyo, ubora wa Upamecano kwenye kumiliki mpira unamfanya kuwa mchezaji muhimu zaidi ambaye Arsenal wanatakiwa kumsajili kipindi cha majira ya joto.

**2. SULUHISHO LA MUDA MREFU**

Upamecano kwa sasa ana umri wa miaka 21 na kumsajili mtu kama yeye kutaipa Arsenal suluhisho la muda mrefu zaidi katika matatizo yao ya ulinzi. Washikabunduki hao kwa sasa wana wachezaji kama Sokratis na David Luiz kwenye kikosi chao, wote wana umri zaidi ya miaka 30 kila mmoja kwa sasa, maana yake wanahitaji damu changa kwenye safu ya ulinzi.

Upamecano anaweza kuwa kijana mdogo kwa umri, lakini ana uzoefu wa kutosha ambao utakuwa msaada mkubwa kwa Arteta kwenye kikosi chake.


**1. UWEZO WA KUONGOZA**

Mmoja anaweza kumuita Upamecano kuwa mlinzi aliyekamilika na mwenye uwezo na kipaji cha kuongoza mchezo. Zaidi ni kwamba ana uwezo mkubwa kwa mipira ya juu na ana nguvu.

Arsenal hawana walinzi wazuri kwenye timu yao na kama watamsajili Upamecano, ataweza kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza na ndiye anayeweza kuleta mabadiliko makubwa kwa safu ya nyuma ya kikosi hicho.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 21, ana uwezo mkubwa zaidi wa kucheza nafasi ya beki wa kati na klabu nyingi zitakuwa zinawania saini yake kipindi cha majira ya joto. Hii maana yake ni kwamba, Arsenal watatakiwa kupigana na klabu kubwa kuwania kupata huduma yake.

**USILOLIJUA**



JADON Sancho sasa amefikisha pasi za mwisho 'assists' 15 katika Bundesliga msimu huu, hiyo ikiwa ni rekodi mpya. Hivyo kuifikia rekodi iliyowekwa klabuni hapo na Henrikh Mkhitaryan katika msimu wa 2015/16.



## Polisi yashauri wazazi malezi

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limewataka wazazi na walezi kuwa makini kwenye malezi ya watoto wao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hawawaachi wakicheza peke yao ili kuepuka madhara yanayoweza kuwakuta ikiwamo kusombwa na mafuriko.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema katika siku za hivi karibuni yameripotiwa matukio kadhaa ya watoto kufariki katika mazingira mbalimbali.

Alisema baadhi ya watoto hao walifariki kwa kutumbukia kwenye visima vya maji, madimbwi, mabwawa na wengine kusombwa na mafuriko wanapocheza peke yao ama wanapotoka shuleni.

Matei aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawapeleka na kwenda kuwachukua shuleni watoto wadogo ili kuepuka madhara ya maji ambayo yamekuwa yakigharimu maisha yao.

"Jeshi la Polisi linawakumbusha wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuzingatia ulinzi wa mtoto, malezi bora na kuwasaidia watoto kwa kuwavusha maeneo yenye mito au maji mengi ili kuepuka madhara yanayoweza kuwapata," alisema Matei.

Aidha, aliwataka wananchi wenye visima kuhakikisha wanavifunika muda wote na kufukia madimbwi yaliyoko kwenye makazi yao ili kuepuka madhara ya watoto kutumbukia na kupoteza maisha.

Vilevile Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linawataka wachimbaji wa madini katika maeneo mbalimbali mkoani humo kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua ili kuepuka kufukiwa na vifusi.

Aliwataka pia wachimbaji kufukia mashimo ambayo hawayatumii kwa maelezo kuwa mashimo hayo ni hatari kwa wananchi endapo yatajaa maji.

# Wanafunzi 251 waliokacha sekondari Rungwe wasakwa

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

WANAFUNZI 251 waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu katika shule mbalimbali za sekondari wilayani Rungwe, hawajaripoti shuleni na hawajulikani walipo liche ya muda wa kuripoti kupita.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Julius Chalya, amewaagiza maofisa watendaji wa kata zote za halmashauri hiyo kuwasaka wanafunzi hao na kuhakikisha wote wanaanza masomo mara moja.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akikabidhi tuzo za kitaaluma kwa shule za msingi na sekondari zilizofanya vizuri katika matokeo ya mitihani ya kitaifa kwa mwaka 2019 utaratibu ambao umeanzishwa na wilaya hiyo ili kuchochea elimu.

Alisema suala la elimu sio la hiari na badala yake ni lazima na kwamba ndio maana serikali iliamua kubeba jukumu la kugharamia kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne kupitia sera ya elimu bila malipo.

Chalya alisema serikali haitamfumbia macho mwanafunzi yeyote ambaye kwa makusudi hataripoti shuleni na kwamba mzazi atakayebainika kumzuia mtoto wake kuanza shule atachukuliwa hatua pia.

"Hatuhitaji kisingizio cha aina yoyote kwa sasa, serikali inagharimia fedha nyingi kuendesha sekta ya elimu, hivyo wote ambao hawajaripoti kuanza kidato cha kwanza wasakwe na waanze masomo, haijalishi hawana sare, ili mradi ana nguo yoyote aanze shule," aliagiza Chalya.

Aliagiza pia wazazi na walezi ambao wanawaficha watoto wao na kuwazuia wasiende shuleni kwa sababu yoyote na wao wachukuliwe hatua za kisheria kwa maelezo kuwa wao ndio wenye jukumu la msingi kuhakikisha watoto wao wanaripoti na kuhudhuria shuleni kwa wakati.

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya, Mwalimu Abel Ntupwa, alisema katika mwaka wa masomo 2020, wanafunzi 5,429 walichaguliwa kujiunga kidato cha kwanza wilayani Rungwe, lakini mpaka sasa wengine hawajulikani walipo.

Alisema wanafunzi hao ambao hawajaripoti wanahesabika kuwa ni watoro kwa maelezo kuwa wamefanya uchunguzi na kubaini kuwa wanafunzi hao hawajajiunga katika shule yoyote ya binafsi na hivyo akaomba wasakwe hata kwa kutumia nguvu ili waanze masomo.

Akizungumza kuhusu tuzo zilizotolewa, Mwalimu Ntupwa, alisema shule za sekondari ambazo zilifanya vizuri na kupatiwa kombe na fedha taslimu ni God-Bridge ambayo ni ya binafsi, Shule ya Wasichana ya Kayuki na Shule ya Sekondari ya Tukuyu na kwamba shule za msingi zilikuwa nne.

Alisema walimu 28 ambao wa sekondari walikuwa 12 na wa shule za msingi 16 walipewa zawadi mbalimbali zikiwamo fedha taslimu, kombe na cheti cha kutambua mchango wao katika kukuza taaluma wilayani humo.

Naye mmoja wa wadau wa elimu wilayani humo, Ponsiano Edward kutoka Shirika la Africa Bridge alisema ushirikiano kati ya serikali, wadau na wananchi umekuwa chachu ya mabadiliko chanya ya elimu wilayani humo.



Baadhi ya wanufaika wa mpango wa Taifa wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), katika Mtaa wa Pambogo Kata ya Iyela jijini Mbeya wakimsikiliza Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimeti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa (hayupo pichani), huku wakiwa na baadhi ya vifaa wanavyotengeneza wenyewe na kuuza wiki iliyopita. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Tasaf yaleta matunda ya elimu Chunya

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MPANGO wa Taifa wa kunusuru kaya maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), unadaiwa kuongeza ufaulu wa wanafunzi wanaotoka kwenye familia za wanufaika katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Tasaf wa Wilaya hiyo, David Ngowi, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, ya kukagua utekelezaji wa shughuli za mfuko huo.

Ngowi alisema kuna baadhi ya watoto wanaotoka kwenye familia za wanufaika wanaendelea na masomo katika vyuo na vyuo vikuu mbalimbali nchini kutokana na hamasa ya mpango huo.

Alisema mwaka huu 2020 wanafunzi 171 wanaotoka kwenye familia za wanufaika ambao wasichana ni 66 na wavulana 105 walijiunga kidato cha kwanza katika shule mbalimbali za sekondari wilayani humo baada ya kufaulu mitihani ya darasa la saba mwaka jana.

Vilevile alisema wanafunzi sita wanaotoka kwenye familia za walengwa walimaliza kidato cha sita na kufaulu vizuri ambapo wawili wanaendelea na masomo ya chuo kikuu na wanne wanasoma vyuo mbalimbali vya ualimu.

"Pia uandikishaji wa watoto wa darasa la kwanza kutoka katika familia za walengwa umekuwa mkubwa ambapo mwaka huu watoto 595 ambao wasichana ni 329 na wavulana 266 waliandikishwa katika shule mbalimbali za msingi," alisema Ngowi.

Vilevile alisema wanafunzi wanaotoka kwenye familia za walengwa wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mitihani mbalimbali ya ndani kutokana na kuanzishwa kwa utaratibu wa utoaji wa zawadi kwa wanaofanya vizuri hasa wanaoshika nafasi ya kwanza, ya pili na ya tatu.

Alisema kwenye mitihani ya mwaka 2019, wanafunzi 40 wanaotoka kwenye familia za walengwa walishika nafasi za kwanza, pili na tatu na kupatiwa zawadi mbalimbali kwa ajili ya kuwatia moyo.

Mwanjelwa aliupongeza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Sophia Kumbuli kwa usimamizi mzuri wa mpango huo hasa kwenye usimamizi wa fedha.

Alisema wilaya hiyo ni miongoni mwa wilaya ambazo katika awamu zilizopita ilikuwa kwenye orodha ya wilaya 10 zilizofanya vizuri huku akiwataka kuhakikisha wanaendelea na utaratibu huo.

Mwanjelwa alisema katika nchi nzima serikali imeutekeleza mpango huo kwa asilimia 70 na kwamba asilimia zilizobakia zitakamilika katika awamu inayoanza sasa hivi na kwamba maboresho mbalimbali ya mpango huo yanaendelea.

"Ufaulu wa wanafunzi wanaotoka kwenye familia za walengwa pamoja na miradi ambayo walengwa wameanzisha ndiyo inaitwa 'multiply effect' (Matokeo chanya) ya mfuko na ndio lengo la serikali, sasa nawasihi mwendelee kusimamia vizuri hata kwenye awamu zijazo," alisema Mwanjelwa.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alimhakikishia Naibu Waziri kuwa wataendelea kushirikiana katika kuhakikisha mpango huo unakuwa na manufaa kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema wilaya hiyo ina viongozi wote wa juu ambao ni wanawake na kwamba wana ushirikiano mkubwa ambao unaifanya wilaya hiyo iwe inafanya vizuri kwenye mambo mbalimbali ya maendeleo.





# Sababu za vifo wajawazito zatajwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SABABU tano zinazochangia vifo kwa wajawazito wakati wa kujifungua, ni pamoja na kupoteza damu nyingi, kifafa cha mimba, maambukizi ya bakteria, huduma duni na upungufu wa damu.

Hata hivyo, asilimia 71 ya vifo hivyo imepungua kutokana na matumizi ya njia ya Lupu.

Naibu Mkurugenzi wa Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambaye anasimamia Idara ya Magonjwa ya Wanawake, Dk. Ahmed Mohamed, alisema, katika mkutano wa kinga na afya ya jamii uliofanyika jijini hapa.

Alitolea mfano kuwa huduma duni zilisababisha vifo 1,449 kwa mwaka 2018 nchini.

Alieleza kuwa kutokana na matumizi ya Lupu imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza vifo kutokana na jamii kufuata uzazi wa mpango.

"Hii njia ya Lupu haina madhara yoyote kwa kinamama wajawazito," alisema.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama, Prof. Project Muganyizi, alisema hivi sasa ni asilimia 13 ya wanawake wanatumia Lupu jambo ambalo limesaidia kupunguza vifo hivyo.

"Nafikiri watu kila kukicha wanaona umuhimu wa njia ya Lupu naomba niwaambie wanawake haina madhara yoyote," alisema Prof. Muganyizi.

Alisema awali matumizi ya njia hiyo yalikuwa hafifu, lakini hivi sasa yameongezeka na kufikia asilimia 13 ili kupuka vifo vinavyotokea kwa wajawazito.

Bingwa huyo aliwataka wanawake kuhimizana kutumia njia hiyo kwa kuwa imeonyesha mafanikio makubwa.

**Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Kinamama, Prof. Project Muganyizi, alisema hivi sasa ni asilimia 13 ya wanawake wanatumia Lupu jambo ambalo limesaidia kupunguza vifo hivyo.**

# 'Unyanyapaa kikwazo kufikia malengo ya dunia'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

UNYANYAPAA ni miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha kutofikia malengo ya kidunia ya kukabiliana na ugonjwa wa Ukimwi, kutokana na watu kuogopa kupima na kupata majibu.

Kufuatia hali hiyo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, leo anatarajiwa kuzindua kampeni endelevu ya kupinga unyanyapaa kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi na Kifua Kikuu (TB), jijini Dodoma.

Hayo yalielezwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya masuala ya Ukimwi, TB na dawa za kulevya, Oscar Mukasa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kampeni hiyo itashirikisha viongozi wa dini ili kusaidia kupinga unyanyapaa unaoikwamisha Tanzania kushindwa kufiki malengo hayo.

"Kampeni inafanywa na serikali kwa kushirikiana na Bunge na Nacopha na Spika atawakutanisha viongozi wa dini nchini katika ukumbi wa Pius Msekwa, bungeni jijini Dodoma kujadili namna ya kusaidia kupinga unyanyapaa," alisema.

Alieleza kuwa wameamua kutumia viongozi hao kutokana na asilimia 90 ya Watanzania wanaoabudu kwenye madhehebu mbalimbali ya dini hivyo itakuwa rahisi kutoa elimu kwa jamii.

"Lengo la mapambano haya tunataka ifikapo mwaka 2025 tuwe tumefikia malengo ya kidunia ya 95-95-95," alisema.

Alisema asilimia 95 ya kwanza inataka Watanzania wanaoishi na VVU wawe wanatambua afya zao.

"Asilimia 95 ya pili inataka wawe wameingia kwenye mpango wa kupatiwa tiba na matunzo na asilimia 95 wanatakiwa kutumia vizuri tiba wanayopata kufubaza vidudu," alisema.

Hata hivyo, alisema kwasasa Tanzania katika asilimia 95 ya kwanza ipo asilimia 62 huku 95 ya pili na tatu ni zaidi ya asilimia 90.

"Unyanyapaa unasababisha kutofikia asilimia 95 ya kwanza ya kujua hali zetu, sasa kwanini tumeamua kutumia viongozi wa dini kwa kuwa wana majukwaa yanayounganisha Watanzania wengi sana," alisisitiza.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Nacopha, Deogratius Rutatwa, alisema viongozi hao wana nafasi kubwa ya kuchangia na kuweka mabadiliko katika mapambano ya unyanyapaa.

"Tutakuwa na kiongozi wa dini kutoka Uganda ambaye anaishi na VVU, Mbunge pia anayetoka Zambia anayeishi na VVU ili wazungumze uzoefu wao katika kuishi na VVU tunataka watu wafunguke na hapa Tanzania kwa kuwa Ukimwi hauchagui," alisema.

Alishukuru serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Rais wa Kupambana na Ukimwi (PEPFAR) na Shirika lake la USAID kwa kufadhili kampeni hiyo.

Alisema kampeni hiyo inalenga kuhakikisha Tanzania inafikia malengo ya kidunia na kuwa na kutokuwa na unyanyapaa.

"Hatutaweza kufikia 95 tatu kama hatutaondoa unyanyapaa kwa sababu hata waliopo kwenye tiba wanakimbia kutokana na unyanyapaa, na mwingine anaficha dawa au kuogopa kunyonyesha akiogopa kunyooshewa vidole," alisisitiza.



Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaisha Moyo (kushoto), akimsikiliza Mwalimu mlezi wa Shule ya Elishadai, Rita Suluja, wakati alipokuwa akitoa maelezo ya jinsi anavyomwandaa kumfundisha mtoto wa shule ya awali kwenye mafunzo ya malezi ya watoto wa vituo vya kulelea watoto wadogo yaliyofanyika jijini Dodoma. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Lusinde atoa somo kwa vijana wa CCM

**Na Peter Mkwavila, CHAMWINO**

MJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Livingstone Lusinde, aliwataka vijana wa chama hicho kutokuwa wapagazi wa mikoba ya wagombea ubunge na udiwani kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu.

Lusinde alitoa kauli hiyo kwenye harambee ya kuchangia ujenzi wa nyumba ya Katibu wa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM), wilayani humo.

Alisema vijana hao badala ya kuwa wapagazi ni vyema wakajitokeza kwa wingi kugombea nafasi hizo za uongozi kuwatumikia Watanzania.

"Wakati wenu sasa wa kujitokeza kwanza kwa kujiandikisha na kugombea nafasi hizo, badala ya kuwapigia debe, kuwabebea mabegi na kuwanadi, hivyo tumieni fursa mliyonayo kama vijana mkizingatia kuwa mmelelewa vyema na mna uwezo wa kuongoza hakuna sababu ya kutumiwa kama madaraja ya watembea kwa miguu au vyombo vya moto," alisema.

Kuhusu harambee hiyo, Lusinde ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mtera, aliwataka vijana hao kujiepusha na matumizi mabaya ya fedha kwa kuwa zimechangwa kwa malengo ya kufanikisha azma ya kujenga nyumba za makatibu nchi mzima.


"Fedha hizi zitumike kwa ajili ya kuhamasisha nyumba ya Katibu inajengwa kwa kuwa zimechangwa na wanachama kwa ajili ya chama chao, hivyo ninawaomba zikamilishe ujenzi wake kama ilivyokusudiwa," alisema.

Kwa upande wake, Katibu wa UVCCM wilayani humo, Peter Dafi, alisema kuwa watahakikisha vijana hao wanajitokeza kugombea nafasi hizo huku akisisitiza kuwa hata fedha zilizochangwa na wanachama kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hiyo itakamilika kwa wakati.

Alisema kuwa jumla ya Sh. milioni 70 zinahitajika kukamilisha ujenzi huo wa nyumba ambayo itajengwa kwa miezi saba kama ilivyoangizwa na uongozi wa vijana ngazi ya taifa.

Awali, akizungumza kwenye harambe hiyo, Mwenyekiti UVCCM Wilaya ya Chamwino, Abdalah Omari, aliwataka vijana hao kujitoa kwa mali na fedha na kwa nguvu zao ili kukamilisha ujenzi huo badala ya kasubiri wafadhili kujitokeza kusaidia.

HABARI ZANZIBAR



# SMZ yajiandaa kufanikisha uchumi bahari

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali imejitayarisha kufanikisha dhana ya uchumi wa bahari, ukiwa ni utekelezaji wa mpango mkuu wa Maendeleo wa Dira Mpya ya 2020 - 2050.

Akizungumza katika ufunguzi wa Jukwaa la kumi la Biashara Zanzibar, alisema serikali inashughulikia dhamira ya ujenzi wa bandari mpya ya abiria (Mpigaduri) na bandari ya mafuta na gesi katika eneo la Mangapwani.

Alisema serikali imefanikisha ununuzi wa boti mpya ya kisasa ya uvuvi na inaendelea na ujenzi wa soko la samaki na bandari ya uvuvi eneo la Malindi na uimarishaji wa sekta ya usafiri wa bahari na utalii.

Dk. Shein alieleza kuwa lengo la serikali ni kuongeza maeneo ya shughuli za uchumi wa bahari na kuziunganisha katika mfumo mmoja madhubuti.

"Katika juhudi za kuendesha uchumi wa bahari kupitia mfumo huo mpya, serikali imeangalia utekelezaji wa baadhi ya nchi zilizofanya vyema na kupata mafanikio ya kuridhisha," alisema.

Alizitaja nchi hizo ni pamoja Mauritius, Sychelles na Afrika Kusini, na kusema mfumo huo umegawiwa katika maeneo makuu manne kama inavyotambulika kimataifa.

Aliyataja maeneo hayo ni uvuvi na mazao ya baharini, nishati mbadala na upatikanaji wa mafuta na gesi asilia katika maeneo ya bahari pamoja na utalii wa fukwe za bahari.

Akizungumzia kauli maudhui ya Jukwaa la Mkutano wa Baraza la Biashara la mwaka huu isemayo 'Ushirikishwaji katika kuleta maendeleo endelevu kupitia uchumi wa Bahari', Dk. Shein alisema ujumbe huo ni mzuri kwa wakati uliopo na unakwenda sambamba na wito anaoutoa wenye lengo la kupanua zaidi shughuli za kiuchumi nchini kwa kuangali fursa nyingine zilizopo, ambazo zimeanza kushughulikia.

Alisema maudhui ya ujumbe huo yanabeba maana halisi ya uchumi wa bahari, inayolenga kuishirikisha jamii katika matumizi ya fursa za maendeleo endelevu ya kiuchumi yapatikanayo katika rasilimali za baharini kwa kuzingatia ubunifu wa fursa na mitindo imara ya kibiashara inayokwenda na wakati.

Dk. Shein alieleza kuwa serikali inaendelea kuandaa miradi mingine muhimu ukiwamo mradi wa "Boosting Inclusive Growth of Zanzibar (BIGZ), utakaofuata baada ya kukamilika mradi wa kuimarisha huduma za jamii mijini (ZUSP).

"Jitihada hizo zinalenga kuyafikia mafanikio zaidi ya kiuchumi, kukiwa na matarajio makubwa zitazaa matunda yenye tija iwapo sekta binafsi itazidisha ushirikiano wake na serikali katika kubuni na kuweka miradi mizuri yenye faida kwa pande zote," alisema.

Alisema bado kuna nafasi kwa sekta binafsi ya kuongeza juhudi za mashirikiano na serikali katika kuzitumia fursa kadhaa za biashara, elimu, afya, utalii na nyenginezo zilizopo nchini ili kuongeza ajira.

Alisema hatua hiyo itawaongezea kipato vijana pamoja na kukuza uchumi wa nchi, akitoa mfano katika sekta ya elimu ambako kuna fani nyingi za teknolojia na ufundi ambazo bado hazijashughulikiwa.

Naye Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Saluma Ali, alisema Zanzibar ina fursa kubwa katika kufanikisha dhana ya uchumi wa bahari, kwa kuzingatia uwepo wa rasilimali za kutosha katika bahari na fukwe.

Aliwataka wajumbe kutumia vyema Baraza la Biashara lililoundwa kwa mujibu wa sheria ili kuimarisha mfumo wa kibiashara kati ya serikali na sekta binafsi.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania (Muungano, Mazingira), Mussa Hassan Zungu, aliipongeza serikali kwa kukusanya vyema kodi, hivyo kuiwezesha nchi kupiga hatua kubwa ya maendeleo kupitia fedha zake za ndani.

Alisema changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika uendeshaji wa shughuli za kibiashara, zitaweza kupatiwa ufumbuzi pamoja na kuondokana usumbufu, hususani katika maeneo ya bandari pale panapokuwa na dhamira ya kweli ya kufanya hivyo.

Rais wa Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima, Tawfiq Salim Turki, aliipongeza serikali kwa kufanikisha uaandaji wa Sheria ya Jukwaa la Biashara na kufanikisha utendaji kazi wa Bandari ya Zanzibar kwa saa 24.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), MusSa Zungu (kushoto), akiteta na mawaziri wa Serikali ya Zanzibar, Issa Gavu wa Ofisi ya Rais Zanzibar (kulia) na Haji Omar Kheir wa Vikosi vya Zanzibar, kwenye mkutano wa Baraza la Biashara jana.
**PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wanahabari watakiwa kupiga vita ujangili

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kupiga vita masuala ya ujangili na uharibifu wa wanyamapori ili Tanzania kuweza kupata watalii wengi katika vivutio vya utalii.

Akiwasilisha mada ya uhalifu wanaofanyiwa wanyamapori katika semina ya waandishi wa habari walioshiriki mafunzo ya wanyamapori na utalii, mkufunzi Exper Pius, alisema vyombo vya habari ndio silaha pekee katika kupiga vita masuala hayo.

Alisema waandishi wa habari wana mchango mkubwa katika kukemea usafirishaji haramu wa wanyamapori nchini na kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania.

"Sauti za vyombo vya habari zikitumika ipasavyo, vitendo vya ujangili kwa wanyama yataondoka na watalii wataongezeka," alisema.

Alisema wakati umefika kwa serikali kuongeza bajeti za wilaya katika suala la utalii na ulinzi wa wanyama pori ili na wananchi ambao wamezunguka katika hifadhi za wanyamapori kutowahujumu wanyama hao.

Pius alisema wanyamapori wamekuwa wakikumbana na matukio mengi ya ujangili kwenye misitu ya hifadhi, biashara haramu, biashara ya nchi moja kwenda nyingine.

Naye mtaalamu wa masuala ya utalii, Moses Njole, alisema sekta ya utalii inachangia fedha za kigeni kwa asilimia 25 katika pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), John Chikomo, aliwashauri waandishi wa habari kuwa mstari wa mbele katika kuandika habari zinazohusiana na masuala ya wanyamapori, uhifadhi na utalii.

**"Sauti za vyombo vya habari zikitumika ipasavyo, vitendo vya ujangili kwa wanyama vitaondoka na watalii wataongezeka," alisema.**

# ZEC: Wanawake hawatabaguliwa uchaguzi mkuu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imesema kuwa haitowadhalilisha wala kuwabagua wanawake ambao watajitokeza kugombea katika uchaguzi mkuu mwaka huu.

Hayo yalisema na Mkurugenzi wa Tume hiyo, Idarous Faina, wakati akizungumza katika mdahalo kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika za maendeleo Zanzibar, ambao uliandaliwa na Muungano wa Asasi za kiraia zinazoangalia uchaguzi Tanzania (TACCEO).

Mkurugenzi huyo aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili kuweza kupata nafasi nyingi za uongozi.

"Tuwaambie kuwa wanawake msiogope muda ukifika gombeeni nafasi mbalimbali za uongozi hasa majimbo na Tume haitowabagua wala kuwadhalilisha wanawake," alisema.

Naye Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mgeni Hassani Juma, aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi katika harakati mbalimbali za uchaguzi mkuu na kuwania nafasi za uongozi kupitia majimbo na kuacha kusubiri kuteuliwa nafasi maalumu.

Alisema kila mwanamke ana uwezo wa kuleta maendeleo, hivyo si vyema kujiweka nyuma na kuwaachia wanaume pekee katika kuliletea maendeleo taifa.

Alisema kuwa utafiti mbalimbali unaonyesha wanawake wanapopewa nafasi za uongozi wanazitumikia kwa uwezo wa hali ya juu katika kuleta maendeleo ya nchi.

Mwenyekiti wa Muungano wa TACCEO, Martina Kabisama, aliitaka jamii kuachana na dhana potofu ya kuwa mwanamke hawezi kuwa kiongozi, kinachotakiwa kuwaunga mkono ili kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Alisema kuwa wanawake wa Zanzibar wanakabiliwa na vikwazo vingi wanaposhiriki katika harakati za uchaguzi ikiwamo kutengwa pale ambapo wataonyesha msimamo katika siasa.

# Serikali yajitosa kupaa bei ya chakula mifugo

**Na Moshi Lusonzo**

SERIKALI imewaagiza wadau wa ufugaji wa kuku na nguruwe kujadiliana kwa kina kuondoa changamoto ya bei ya chakula cha mifugo hiyo inayopanda kwa kasi kila siku.

Akizungumza wakati akifungua kikao cha wadau wa kuku na nguruwe jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi na Mifugo Sekta ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema bei kubwa ya chakula imekuwa kikwazo katika ukuwaji wa sekta hiyo.

Alisema katika kikao hicho, serikali inasubiri maamuzi yatakayofikiwa katika kuangalia mnyororo mzima wa thamani ya mifugo hiyo kuanzia uzalishaji wa chakula, ufugaji hadi kwa mlaji ili kuwapo na gharama ambazo zitaleta tija kwa pande zote.

"Serikali itaendelea kuwa pamoja na wadau wa ufugaji wa kuku na nguruwe, kwa kupitia kikao chenu suala la bei ya chakula litapatiwa ufumbuzi kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kunufaisha Taifa kiuchumi," alisema Prof. Ole Gabriel.

Alisema awali alizungumza na baadhi ya wajasiriamali wanaojishughulisha na ufugaji wa kuku, wote kilio chao ni kupanda kwa chakula kila wakati na kusababisha kurudi nyuma.

"Vijana wengi sasa wameamua kuingia katika ufugaji wa kuku na nguruwe, lakini unapowauliza changamoto zao watakuambia ni gharama kubwa ya chakula. Hili ni lazima tulitazame upya kwa ajili ya kuwavutia wengine," alisisitiza.

Akitoa takwimu ya mifugo hiyo, Prof. Ole Gabriel, alisema mpaka jana idadi ya kuku walikuwa milioni 79.2 na nguruwe zaidi ya milioni 2 na kuongoza kwa wingi wao nchini.

Mwenyekiti wa wazalishaji wa chakula cha kuku, Harro Bhagat, alisema kupanda kwa bei ya chakula inatokana na gharama ya ununuzi wa malighafi kama mahindi na soya kuwa juu.

Akitolea mfano mwaka jana mahindi yalikuwa yakinunuliwa kwa Sh. 400 kwa kilo, lakini baada ya miezi michache iliongezeka kwa kasi na kufikia Sh. 900 kwa kilo moja.

"Serikali inatakiwa kuangalia suala hili ili tupate bei rafiki ya kununulia mahindi pamoja na kuturuhusu kuagiza nje maharage ya soya kutokana na uzalishaji wake hapa nchini kuwa mdogo," alisema Bhagat.

Aidha, alisema kikwazo kingine wanachokabiliana nacho ni mlolongo mrefu wa kupata cheti cha ubora wa chakula kutoka TBS, jambo ambalo linasababisha muda mwingi kupotea kabla ya kuanza uzalishaji.

Mwakilishi wa wafugaji wa nguruwe, Doreen Maro, alisema kwa upande wao wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa machinjio ya kisasa pamoja na uhaba wa mbegu bora.

"Wafugaji tunapata shida kutafuta sehemu salama ya kuchinja mifugo yetu kutokana na machinjio kuwa duni na inayohatarisha usalama wa afya na kupunguza thamani ya bidhaa. Tunaomba serikali ituangalie kwa kutujengea machinjio yenye hadhi ili na sisi tupate faida," alisema.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adorf Mkenda, akizungumza wakati wa kikao cha maandalizi ya maonyesho ya Glite Lakes International Tourism Expo (GLITE) mwishoni mwa wiki jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wajasiriamali wanawake waelezwa fursa Comoro

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Balozi wa Comoro nchini, Balozi Bacar Salim, ameuambia mkutano wa maandalizi ya maonyesho ya bidhaa za Tanzania yanayotarajiwa kufanyika Comoro mwezi ujao kwamba washiriki wapeleke Comoro bidhaa za chakula, viungo, dawa za asili, asali, dagaa pamoja na bidhaa za viwandani, hasa samani za ndani.

Mkutano huo umeitishwa na Mfuko wa Saccos wa Wajasiriamali Tanzania (TASWE) au Tanzania Saccos for Women Entrepreneurs kuwaandaa wajasiriamali watakoshiriki katika maonyesho ya siku nane yanayotarajiwa kufunguliwa na Rais wa Comoro, Aprili 17 na kufungwa

Aprili 24, mwaka huu. Maonyesho hayo yatavuma kama wajasiriamali wanawake wa Tanzania tumekuja Comoro.

"Jambo la muhimu kwenu ni kujua bidhaa ambazo Wacomoro wanazihitaji. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiagiza bidhaa za chakula, viungo, dawa za asili, asali, dagaa pamoja na bidhaa za viwandani kutoka nchi mbalimbali. Hivyo wakati mkijiandaa na ziara hiyo ya kibiashara ni vyema mkaangalia hayo maeneo,'' ameshauri Balozi Salim.

Alipongeza jitihada za kinamama ambazo kwamba zinaimarisha uhusiano wa muda mrefu kati ya Tanzania na Comoro.

Alisema watu wa nchi hizo mbili wamekuwa wakifanyabiashara kwa muda mrefu. "Hivyo ni jukumu letu kuweka mazingira mazuri na ambayo ni endelevu kwa manufaa ya vizazi vya leo na kesho."

Mwenyekiti wa Taswe, Anna J. Matinde, alisema kuwa maandalizi yote ya safari hiyo yamekamilika.

"Kwa kiasi kikubwa maandalizi ya safari yamekamilika. Kwa sasa tunaangalia mambo machache ikiwamo viza. Makadirio yetu yalikuwa tuondoke na wajumbe 60, lakini mkutano huu umeongeza hamasa kwani wajumbe wengine wamejitokeza na hivyo kuongeza idadi ya washiriki," alisema Matinde, na kuwapongeza wajumbe kwa kuhudhuria mkutano huo ambao alisema umewapa nafasi ya kufahamu fursa za biashara zilizopo Comoro.

Meneja wa TASWE, Lilian Nyagabona, ambaye anasimamia itifaki, alieleza kuwa maonyesho hayo yanayotarajiwa kufunguliwa na Rais wa Comoro. "Haya yatakuwa ni maonyesho yenye mvuto wa aina yake kwani serikali za nchi zote mbili wameyabariki na tutaondoka hapa. Taarifa tulizonazo ni kwamba yatahudhuriwa na watu wengi wakiwamo wafanyabiashara na wawekezaji wa huko Comoro," alieleza Nyagabona.

# Kamati ya madiwani kufuatilia migogoro mipaka

**Na Yasmine Protace, MKURANGA**

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, limeazimia kuundwa kwa kamati maalum itakayoshughulikia kero ya migogoro ya mipaka sambamba na baadhi ya viwanda ambavyo vinazalisha bidhaa wilayani humo, lakini kodi za huduma wanalipa Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye baraza hilo, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Abdallah Ullega, ambaye ni Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alisema mkakati huo wa ufuatiliaji wa kina umelenga viwanda 86 vyote vilivyoko katika wilaya hiyo ili vilipe ushuru ambao utasaidia katika kuendeleza kutekelezaji shughuli za miradi ya maendeleo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, alisema kamati hiyo ambayo itakuwa na mchanganyiko wa madiwani na wataalamu, itashughulikia migogoro ya mipaka inayohusisha wilaya za Kibiti, Kisarawe, Ilala na Kigamboni kwa kukutana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi na kumwomba kufika Mkuranga ili kusaidiana naye na hatimaye kumaliza mgogoro huo.

Akitoa salamu za serikali, Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, aliwataka madiwani kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua kuwa mabalozi wazuri katika kata zao kuwaeleza wananchi wawe makini wanapovuka mito inayopitisha maji sambamba na kuwazuia watoto wa shule hadi hapo hali itakapokuwa sawa.

Akifunga kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri, Juma Abeid, aliwaomba madiwani wenzake kutumia muda uliobaki kabla ya uchaguzi mkuu kusimamia fedha zinazotumwa kwenye kata zao zinalingana na ubora wa miradi husika.

HABARI KIMATAIFA

# Wanawake walia kukosa haki za msingi

**KHARTOUM,** Sudan

IKIWA imepita miezi 11 tangu kuangushwa kwa utawala wa Rais Omar al-Bashir, wanawake wa Sudan jana wakati wakisherehekea siku yao duniani, wamelalamika kunyimwa haki zao.

Mwanaharakati aliyehusika kuanzia mwanzo wa vuguvuvu la maandamano yaliohitimisha utawala wa miongo mitatu wa Omar al-Bashir, Zeineb Badreddine, alisema hakuna kilichofanyika kwenye kutekeleza madai ya wanawake nchini humo.

Miaka 30 imepita tangu Badreddine alipofukuzwa kazi chini ya Bashir kutokana na dhana zake za mageuzi na haki za kiraia.

Hivi sasa Badreddine amerejea kwenye ufundishaji. Lakini licha ya kupinduliwa kwa utawala wa Bashir, anasema serikali mpya inakosa uwakilishi wa wanawake.

**Baada ya Waziri Mkuu, Abdalla Hamdok kuunda serikali yake Septemba, mwaka jana aliahidi kuboresha hali ya wanawake licha ya ugumu wa kiuchumi.**

Baada ya Waziri Mkuu, Abdalla Hamdok kuunda serikali yake Septemba, mwaka jana aliahidi kuboresha hali ya wanawake licha ya ugumu wa kiuchumi na kijamii nchini humo.

Alitoa nafasi 17 za mawaziri kwa wanawake, ikiwamo wizara nyeti ya mambo ya kigeni. Mwanamke pia aliteuliwa kuongoza idara ya mahakama.

Lakini mamlaka ya juu kabisa ya nchi, Baraza la Uongozi linaloundwa kwa pamoja kati ya raia na jeshi likiwa na mamlaka ya kusimamia kipindi cha mpito kuelekea utawala wa kiraia, lina wawakilishi wawili tu wa kike katika ya jumla ya wajumbe 11.

Iwapo wanawake wangekuwa na uwakilishi mzuri, wangekuwa na sauti zaidi za kuwatetea," alisema Badreddine.

Alisema chini ya utawala wa Bashir, sheria ya utulivu wa kijamii ilitumika kuwaadhibu wanawake hadharani au kuwafunga gerezani kwa uvaaji usiyo wa heshima au kunywa ulevi, vitendo vilivyotazamwa kama ukosefu wa heshima na maadili.

Serikali ya Hamdok iliondoa sheria hiyo mwaka jana, lakini sheria nyingine nyingi za kibaguzi zinaendelea kutumika.

Badreddine analalamikia sheria ya jinai kuhusu unyanyasaji wa kingono. Majaji nchini Sudan wana mamlaka ya kuamua iwapo mwanamke amebakwa au la, jambo ambalo wakati mwingine linapelekea waathirika kushtakiwa kwa uzinzi.

Wakili na mwanaharakati wa wanawake, Inaam Atiq anakosoa sheria ya hadhi binafsi ya mwaka 1991, ambayo alisema inasababisha mateso kwa maelfu ya wanawake kote Sudan.

Alisema sheria hiyo inaruhusu watoto wa kike wenye umri wa miaka 10 kuozeshwa kinyume na matakwa yao.

Mwanaharakati Manal Abdelhalim alieleza kushangazwa na sauti, zikiwamo za wanawake, wanaosema kwamba suala la (haki za wanawake) siyo la kipaumbele na kwamba linaweza kusubiri. **DW**



Wanawake wa Sudan wakiwa katika maandamano wakilalamika kunyimwa haki za msingi. **PICHA: REUTERS**

## Hoteli ya ghorofa saba yaporomoka, 10 wafariki

**BEIJING,** China

IDADI ya watu waliofariki baada ya kuporomoka kwa hoteli moja iliyokuwa ikitumiwa kuwaweka watu chini ya karantini kutokana na virusi vya corona katika mji wa Quanzhou nchini China, imefikia watu 10.

Mamlaka nchini humo zimesema watu wengine 28 bado wamekwama kutokana na ajali hiyo. Awali zaidi ya watu 70 waliaminika kukwama katika jengo hilo la ghorofa saba lililoporomoka jana jioni.

Wakati wa mkutano na wanahabari uliondaliwa na serikali katika eneo la Quanzhou jana, maofisa wa serikali, walisema kuwa kikosi cha uokoaji cha zaidi ya watu 1,000 ikiwa ni pamoja na maofisa wa zimamoto, vikosi vya polisi pamoja na wahisani wengine, walifika katika eneo hilo jana usiku huku watu 43 wakiokolewa na 36 kati yao kupelekwa hospitalini.

Shirika la habari nchini humo Xinhua, limeripoti kuwa ghorofa ya kwanza ya jengo hilo ilikuwa chini ya ukarabati wakati wa tukio hilo. **DW**

## Saudi Arabia yakamata wanawafalme

**RIYADH,** Saudi Arabia

SAUDI Arabia imewaweka kizuizini wanafamilia waandamizi wa familia ya Kifalme ya Saudi Arabia, Prince Ahmed bin Abdulaziz, mdogo wake wa mwisho Mfalme Salman, na Mohammed bin Nayef, mpwa wa mfalme, vyanzo viwili vyenye habari za ndani juu ya suala hilo vimesema.

Mwana wa mfalme Mohammed bin Salman, mtoto wa Mfalme Salman na pia mrithi wa nchi yenye kutoa mafuta zaidi kuliko zote na mshirika mkubwa wa Marekani, alikuwa akijiimarisha kiutawala tangu alipompindua ndugu yake, Mohammed bin Nayef, ambaye alikuwa ndiye mrithi wa kiti hicho cha ufalme katika mapinduzi yaliyofanyika katika kasri ya mfalme mwaka 2017.

Chanzo cha habari kimesema kuwekwa kizuizini kwa wanafamilia hao kulitokea siku ya Jumamosi. Shirika la habari la Uingereza halikuweza kupata ufafanuzi sababu zilizopelekea kuwekwa kizuizini watu hao.

Gazeti la Wall Street limeripoti kuwekwa kizuizini kwa wana wa mfalme wawili hao mapema Ijumaa, na wameeleza inafungamana na madai ya kuwa wanahusika na jaribio la kufanya mapinduzi.

Maofisa wa Saudi Arabia hawakuweza kupatikana mara moja kutoa maelezo yao mapema Jumamosi. Ofisi ya serikali inayoshughulikia masuala ya habari haikujibu ombi la shirika la habari la Reuters likiwataka watoe maelezo. **VOA**

## Rwanda yafunga CCTV kukabiliana na corona

**KIGALI,** Rwanda

RWANDA imeanzisha mikakati kabambe ya kupambana na ugonjwa wa corona.

Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Kanombe uliopo jijini Kigali, umezungukwa na kamera za kisasa (CCTV).

Kamera hizo zilizounganishwa na kompyuta zina uwezo wa kupima virusi ya corona kwa kila mtu anayeingia pasipo kumgusa na kujua kama ana maambukizi au la.

Tangu kufungwa kwa kamera hizo, abiria wanaingia na kutoka katika uwanja huo bila hofu yoyote ya kuambukizwa virusi vya Covid-19.

Kadri wanavyoingia kwenye uwanja huo wa ndege, ndivyo kamera zilizowekwa uwanjani hapo zinafanya kazi ya kupima joto ya kila mtu anayeingia pasipo kuguswa na kutoa taarifa ya joto lake kwenye kompyuta zilizounganishwa na kamera hizo. **RFI**

# Kanyasu akatalia kuvua hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amekataa ombi la wakazi wa Kijiji cha Kilangawana kufanya shughuli za uvuvi katika la Pori la Akiba la Uwanda kwenye Ziwa Rukwa.

Ombi hilo lilitolewa na wananchi hao kutokana na Ziwa Rukwa lililohifadhiwa kuwa na samaki wengi.

Akizungumza katika mkutano wa katika kijiji cha Kilangawana Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Kanyasu alisema sehemu ya pori hilo ambayo wananchi wanataka kuvua samaki ni eneo muhimu kwa ajili ya mazali ya samaki.

Amesema serikali haiko tayari kumruhusu mtu yeyote kuendesha shughuli za uvuvi katika eneo hilo kwa kuwa samaki wakishazaliana katika eneo hilo hutawanyika maeneo ambayo wananchi wanaruhusiwa kuvua.

"Tukiruhusu eneo hilo mvue samaki, mtamaliza samaki wote kama mlivyofanya katika maeneo yenu," alisisitiza Kanyasu.

Alisema sheria za uhifadhi haziruhusu shughuli za kibinadamu kufanyika ndani ya pori hilo na yeyote atakayebainika, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Katika hatua nyingine, Kanyasu amewataka wananchi hao kufuata sheria za uhifadhi na kuacha tabia ya kuingia katika eneo la hifadhi kuvua samaki kwani ni kosa kisheria

"Nimesikia kuna wengine mitumbwi yao imekamatwa, nataka kuwaambia fuateni sheria ili kujiepusha kukamatwa na askari wangu," alisema Kanyasu.

Diwani wa Kata ya Kilangawana, Dennis Kayuni, alimweleza Naibu Waziri huyo kuwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi wa kijiji hicho wanategemea kipato chao kutokana na shughuli za uvuvi, hivyo wanamwomba alegeze kidogo sheria ili waweze kuvua katika eneo la hifadhi.

"Tunajua sheria haziruhusu kuvua samaki katika eneo hili, lakini legeza sheria japo kidogo, tunakuahidi ukifanya hivyo tutakuwa tunalipa kodi zote za serikali," alisema diwani huyo.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Halfan Haule, amewataka wananchi hao kuwa walinzi wa hifadhi hiyo kwa kuwa eneo hilo ni muhimu kwa mazalia ya samaki, ambao hutawanyika maeneo mengine na kuwawezesha wao kuvua.




Mmoja wa wachokoza mada wakati wa Jukwaa la Wanawake la Kujenga Uwezo la Benki ya Absa Tanzania, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi Kinemo (wa pili kushoto), akizungumza wakati wa Jukwaa la Wanawake lililoandaliwa na wanawake wafanyakazi wa Benki ya Absa Tanzania ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Jukwaa hilo ambalo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki. **NA MPIGAPICHA WETU.**

# Serikali yatahadharisha ongezeko maji Ziwa Victoria

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, amewataka wananchi kuzingatia sheria ya maji na matumizi ya ardhi kabla ya kujenga miradi ya maendeleo kandokando ya Ziwa Victoria.

Sheria hiyo inaelekeza kuacha mita 60 ili kuepuka madhara watakayoyapata kutokana na kuongezeka kwa kina cha maji ndani ya ziwa hilo.

Prof. Mkumbo alitoa hadhari hiyo wakati wa ziara yake ya siku mbili kwa wilaya ya Kwimba na Misungwi ya kukagua miradi ya maji inayotekelezwa, na kwamba kipimo cha muda mrefu cha Ziwa Victoria kinaonyesha kwamba usawa wa juu wa bahari ni mita elfu 1,133.19 ambapo kwa mujibu wa kipimo kilichochukuliwa Machi 4, mwaka huu, kimeongezaka na kufikia mita elfu 1,134.28 na ziwa hilo kufunga rekodi ya kuwa na maji mengi .

Ripoti za awali kutoka Bodi ya Maji bonde la Ziwa Victoria zilionesha kina cha maji kuongezeka na kubaki sentimita 3 tu kufikia rekodi ya mwaka 1965 ya mvua za Elnino, hivyo miradi yote inayoandaliwa kwa kutumia Ziwa Victoria lazima izingatie vipimo ili kuepukana na miundombinu isiyofuata utaratibu kubomolewa, ambapo kwa sasa wingi wa maji umesababisha kusogea kwenye kingo za ziwa hilo.

Pia kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwa kipindi hiki cha masika, huenda ongezeko la maji ikawa juu zaidi "Tulishaona baadhi ya mahoteli hapa Mwanza sitotaka niyataje majina, yameshawasogelea na kusababisha kuanza kujenga ukuta, lakini ukiangalia walivyojenga hizo hoteli wamejenga karibu na ziwa, lakini kama wangefuata ile sheria na wakajenga mita 60 tatizo lisingekuwapo," alisema Prof. Mkumbo.

Aliitaka Mamlaka za maji, Wakala wa maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa wasitekeleze miradi yote ya maji inayotegemea Ziwa Victoria bila kufata kibali na ridhaa kutoka bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria.

## Waziri Zungu azibana halmashauri usafi fukwe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mussa Zungu, amewaagiza Wakurugenzi Watendaji wa Manispaa za Ilala na Kinondoni jijini Dar es Salaam, kuhakikisha fukwe zote zilizoko katika manispaa zao zinasafishwa na kufanyiwa usafi kila mara.

Amesema wanapaswa kuhakikisha wanakusanya uchafu wote uliokusanywa katika maeneo ya fukwe ili kuyafanya maeneo hayo kuwa salama kiafya na mazingira.

Zungu alitoa agizo hilo jana baada ya kushiriki usafishaji wa fukwe za bahari eneo la Daraja la Selander jijini, Dar es Salaam akikipongeza kikundi cha utunzaji wa mazingira cha Save the Coast kwa kumwalika kujumuika pamoja nao kusafisha fukwe.

Alisema kikundi hicho ni mfano wa kuigwa kutokana na moyo na ari yao ya kusafisha fukwe za bahari na kuziweka katika mazingira ya usafi.

"Ninawapongeza wote, lakini tushirikiane katika kutunza mazingira ili kuwaachia kizazi kijacho mazingira safi na salama," alisifu.

## Gharama umeme jua kikwazo Korogwe

**Na Beatrice Shayo,** KOROGWE

WANANCHI wa kijiji cha Mpale wilayani Korogwe mkoani Tanga, bado hawana uelewa wa kutosha kuhusiana na matumizi ya umeme jua huku wakilalamikia gharama za nishati hiyo ni kubwa.

Wananchi walieleza hayo mwishoni mwa wiki, wakati wakizungumza na waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) waliofanya ziara katika kijiji hicho kwa ajili ya kujifunza mradi wa umeme jua uliopo katika kijiji hicho.

Nasibu Mhammed alisema gharama za umeme huo ni kubwa kwa kuwa kwa mwezi wanatakiwa kulipa Sh. 11,000 ambayo unalipia kama vocha.

"Mimi sijajiunga na huo umeme wenzangu wanasema ni gharama kubwa kutokana na kipato tulichokuwa nacho hapa kijijini bado ninaendelea kutumia kibatari, lakini wenye sabafu ama majokofu wao nasikia wanalipia Sh. 36,000 kwa mwezi," alisema.

Naye, Mwajuma Issa alisema umeme huo hawautaki kwa kuwa kijiji wameahidiwa na serikali kuwapatia umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

"Sisi wametuambia wanatuletea umeme wa Rea tunausubiri huo huo uje hata kama tutalipa bei, lakini tunausubiria uje kama walivyotuahidi huo wa umeme wa jua ni bei kubwa kwa mwezi," alisema.

Naye, Mwenyekiti wa Kitongoji, Abdallah Mdoe, alisema kwa mkataba wa kwanza kwa mwezi walikuwa wanalipa Sh. 11,000 kwa sasa wamejiwekea utaratibu na kampuni ya Ensol unaweza kununua umeme hata wa Sh. 2,000.

Alisema wapo wananchi wanalalamikia umeme huo ni gharama kubwa ni jambo ambalo haliwezi kukwepeka kwa kuwa nishati hiyo imewasaidia.

Naye, Hassan Bakari alisema anatamani kuacha kutumia mafuta ya diseli katika mashine yake ya kusaga ili ajiunge na umemea wa jua changamoto aliyo nayo bado hajapata elimu ya kutosha katika gharama zake kwa mwezi.

# Presha ya macho yatesa Watanzania

**Na Mary Geofrey**

WATANZANIA wametakiwa kujenga utaratibu wa kupima afya mara kwa mara ili kubaini magonjwa mbalimbali yasiyo na dalili kama presha ya macho.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Daktari wa Macho wa Hospitali ya Taifa Muhimbili tawi la Mloganzila, Dk. Catherine Makunja, wakati wa kufanyia uchunguzi wa macho wakazi wa Jiji la Dar es Salaam katika kuadhimisha Siku ya Presha ya Macho Duniani.

Kauli mbiu katika siku hiyo inayoadhimishwa Machi 7, inasema, "Tokomeza Shinikizo la Macho lililojificha" lengo ikiwa ni kufanya uchunguzi wa macho, kupima presha ya macho, kutoa ushauri juu ya magonjwa ya macho pamoja na matibabu yake.

Dk. Makunja alitaja sababu za kuwapo kwa ugonjwa huo ni umri wa miaka 40 na kuendelea, magonjwa ya kurithi katika familia, kisukari, unywaji pombe kupita kiasi, uvutaji sigara na matumizi ya dawa bila kufuata ushauri wa daktari.

"Tatizo la presha ya macho huwa mara nyingi linapoanza halina dalili na wagonjwa mara tu wanapofanyiwa vipimo huwa wanakutwa na ugonjwa huu ndio maana tunatoa hamasa kwa watu kuja kufanya uchunguzi mara kwa mara," alisema Dk. Makunja.

Alisema duniani tatizo la macho lipo kwa asilimia nne, hivyo aliwahimiza Watanzania kujitokeza kupima macho mara kwa mara kwa sababu tatizo hilo husababisha upofu.

Kuhusu upimaji huo, alisema zaidi ya watu 300 walijitokeza kupata huduma hiyo bure na wagonjwa waliobainika kuwa na tatizo la presha ya macho walipatiwa huduma za matibabu bure.

Alisema kati ya wagonjwa wa awali 200 waliofanyiwa vipimo, wagonjwa tisa walibainika kuwa na presha ya macho bila wao kujua.

Dk. Makunja alisema wale ambao watabainika kuwa na matatizo ya kawaida watapatiwa dawa na miwani kwa msaada wa kampuni ya Salama inayouza dawa na vifaa tiba nchini.

Naye Daktari wa Macho wa MNH-Mloganzila, Dk. Judith Mwende, amefafanua kuwa mbali na wagonjwa kufanyiwa uchunguzi wa macho na kugunduliwa kuwa na presha ya macho madaktari hufanya uchunguzi wa kina ili kutambua aina ya presha ya macho aliyonayo mgonjwa.

Mmoja wa watu waliojitokeza kufanyiwa uchunguzi hospitalini hapo, Nora Charles, aliishukuru Mloganzila kwa kutoa huduma hiyo bure, pia aliwasihi Watanzania kujitokeza kwa wingi kufanyiwa uchunguzi wa magonjwa mbalimbali na kupatiwa matibabu mapema.



Baadhi ya wakazi wa Kata ya Kiriba Wilaya ya Musoma mkoani Mara, wakishirikiana na mafundi juzi, katika ujenzi wa madarasa mapya ya Kiriba Sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Mama wa wenye ualbino watakiwa kuripoti ustawi

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Kimataifa la Under The Same Sun, (UTSS), limewataka wanawake wenye watoto walio na ualbino ambao mzazi mwenza hatoi matunzo ya malezi, wakaripoti ustawi wa jamii ili haki hiyo ipatikane.

Mwanasheria wa Shirika hilo, Maduhu William, aliyasema hayo juzi wakati wa mafunzo kwa wanawake na walezi wa watoto wenye ualbino ikiwa sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

"Siku hii inaambatana na haki zenu, ni jukumu lenu kuhakikisha haki ya matunzo ya mtoto yanafanywa na baba na mama na siyo mama peke yake, wale ambao mnalea mtoto au watoto wenyewe chukueni hatua na Jumatatu (leo) mkatoe taarifa ofisi ya ustawi wa jamii ili mtoto wako apate haki yake," alisema.

William aliwakumbusha wanawake kuwa wakati wakiadhimisha siku yao, wakumbuke mtoto mwenye ulemavu analindwa na sheria mbili, ya mtoto na ya watu wenye ulemavu.

Alizitaja baadhi yake kuwa mtoto ana haki ya kupata chakula na elimu bora, usalama, kuishi, kucheza.

"Msiwafungie ndani watoto wenu wana haki ya kucheza na wenzao nje ila mhakikishe wakati wapo huko wanacheza sehemu salama, msiwaone kama mayai wanahaki ya kushirikiana na wenzao," alisema.

Pia aliwataka wazazi na walimu kutambua kuwa mtoto mwenye ualbino anapokwenda shule sare zake ziwe za kumkinga na jua, wanatakiwa kuvaa shati la mikono mirefu, sketi au suruali.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Grace Wabanhu, aliwasimulia wazazi na walezi hao namna mama yake alivyowalea kwa shida baada ya baba yao kutowajali, kutokana na ualbino.

"Tupo watatu, lakini mama yetu alisimama kama mwanamke alihakikisha tunapata elimu bora na wote tumefika chuo kikuu.

"Pamoja na baba kutengana na mama, tulipomaliza darasa la saba mama yetu alituambia tuende kwa baba, akifanya hivyo ili kutuonyesha kwamba hatutengwi naye, lakini tulipofika siku ya kwanza baba alituambia mmekuja kufanya nini, hatukukaa kesho yake tukirudi kwa mama yetu," alisema.

Alisema mama yao alihakikisha wote watatu wanasoma na sasa wanafurahia mafanikio ya elimu waliyoipata.

"Ninachotaka kusema, msiwatenge watoto wetu na baba zao hata kama wamewakataa, wakati mwingine haya hutokea kutokana na mashinikizo ya jamii au ndugu. Licha ya mambo yote yaliyojitokeza tulimsamehe baba yetu, msiweke vinyongo na muwalee watoto wenu kwa kumjua Mungu," alisema.

Stella Bulinda, mama wa watoto wawili wa kike na wa kiume wenye ualbino, alisema baada ya kujifungua muuguzi alimuonyesha mtoto na kumuuliza kama kwao kuna watu wa aina hiyo.

"Sikutegemea, ilinishtua sana na kuumia na nilimuuliza Mungu kwa nini, namshukuru Mungu ninawapenda watoto wangu na mume wangu anawapenda sana, nilipojifungua mtoto wa kwanza mume wangu alikuwa nje ya jengo la hospitali nilipompigia simu kumweleza alinijibu kwa kifupi usijali yote ni mapenzi ya Mungu," alisema.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Upendo wa Wanawake wenye watoto walio na ualbino mkoa wa Dar es Salaam, Betrana Mbazi, alisema kimewawezesha kuwatunza watoto wao.

HABARI MICHEZO




# GIROUD: NATAKA KUBAKI CHELSEA

**LONDON,** England

OLIVIER Giroud anataka kupata mkataba mpya Chelsea baada ya mshambuliaji huyo "kurudi" ghafla kwenye ubora wake.

Mfaransa huyo alionekana kufunguliwa mlango wa kuondoka Januari, huku klabu za Lazio na Inter Milan zikionekana kumnyatia. Lakini Chelsea walishindwa kumsajili mchezaji wa kuziba nafasi ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 na hivyo kulazimika kubakia pale Stamford Bridge.

Kwa sasa Mfaransa huyo anaonekana kumteka kocha Frank Lampard ambaye anampa nafasi ya kucheza.

Mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal ambaye alianza kwenye mchezo dhidi ya Tottenham Hotspur mwezi uliopita kutokana na kukosekana kwa mfungaji bora, Tammy Abraham. Na akiwa amefunga dhidi ya Spurs, Giroud alipewa nafasi ya kucheza dhidi ya Bayern Munich, Bournemouth na Liverpool.

Na sasa mshambuliaji huyo anataka kuongeza mkataba mpya wa mwaka mmoja hapo Chelsea.

Alipoulizwa kama angependa kubakia hapo London Magharibi baada ya timu yake kupata ushindi kwenye mchezo wa FA dhidi ya Liverpool, alisema: "Ndio, ndio, bila shaka.

"Imebakia miezi michache, kushinda mechi na pengine kutwaa taji jingine na kama mnavyojua nimekuwa na misimu miwili au mitatu mizuri hapa.

"Si muda wa kuzungumza kuhusu mkataba, na kila kitu kitaamuliwa inavyowezekana muda ukifika."

# Mourinho amwonya Ndombele Spurs

**LONDON,** England

JOSE Mourinho alielezea kwa hasira kiwango alichoonesha Tanguy Ndombele wakati wa sare ya 1-1 dhidi ya Burnley Jumamosi na amemwonya kiungo huyo wa Tottenham kuwa uvumilivu wake kwake unafikia mwisho.

Ndombele aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo alianza pamoja na Oliver Skipp kwenye safu ya kiungo pale kwenye dimba la Turf Moor, na Spurs walionekana kukosa muunganiko na walikwenda mapumziko wakiwa nyuma kwa bao la Chris Wood.

Mbinu za kuchezesha walinzi watatu kipindi cha pili zilishuhudia Skipp na Ndombele wakitoa njia kwa Lucas Moura na Giovani Lo Celso, ambao ndio waliotoa mchango mkubwa kwenye kusawazisha bao hilo.

Lo Celso alirudi kwenye kiungo na akamlisha Erik Lamela, ambaye alipeleka kwa Ben Mee na Dele Alli akafunga la kusawazisha na kufikisha bao lake la 50 kwenye Ligi Kuu ya England.

Mourinho amekuwa mkali kwa Ndombele wakati huu wa msimu wake wa kwanza kwa Mfaransa huyo kwenye Ligi Kuu ya England na alimlaumu kwa kucheza chini ya kiwango dhidi ya Burnley.

"Nafikiri ubora wa Lucas na Lo Celso ulileta tofauti, na nataka kusema, lakini siwezi kusema," alisema Mourinho akiiambia Sky Sports baada ya Spurs kufikisha mechi ya tano bila ushindi.

"Tulikuwa na kitu fulani kipindi cha kwanza ambacho hatukuwa nacho kipindi cha pili, hivyo kwenye kipindi cha pili tuliimarika sana."

"Nafikiri ni kuchoka, Lucas alikuwa hivyo na Lo Celso pamoja na (Steven) Bergwijn na Dele Alli alitupa kile mlichokiona. Siulizi sana kuhusu hilo.






# *Simeone aelezea sababu kumtoa Felix*

**MADRID,** Hispania

MASHABIKI wa Atletico Madrid walizomea maamuzi ya Diego Simeone kumtoa Joao Felix wakati wa mchezo wa Jumamosi wa sare ya 2-2 dhidi ya Sevilla, lakini kocha huo alielezea kwamba yalikuwa ni maelekezo kwamba awe "makini" na mchezaji huyo.

Los Colchoneros hao walikosa nafasi ya kuwafunga Sevilla na kupaa nafasi ya tatu kwenye msimamo wa LaLiga, wakati waliposhindwa kupenya ngome ya wageni hao na kujikuta wakiwa nyuma kipindi cha kwanza.

Penalti ya Alvaro Morata na bao la Joao Felix lilifuta lile la ufunguzi la Luuk de Jong, kabla ya Lucas Ocampos kuisawazishia Sevilla na kuondoka na pointi moja.

Huku mashabiki wa Atletico wakishangilia kuondoka na ushindi, Joao alitolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na winga wa zamani wa Sevilla, Vitolo dakika ya 80 na mashabiki walizomea kuonyesha kutofurahishwa na jambo hilo.

Lakini Simeone alielezea umuhimu wa maamuzi yake hayo baada ya mchezo huo.

"Hatuwezi kuwaambia watu kwamba alitoneshwa kwenye kigimbi chake," alisema Simeone akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Daktari aliniambia niwe makini na Joao kwa sababu alikuwa bado hajapona vizuri, ndio maana nikafanya mabadiliko.

## HABARI MICHEZO

# Rais ataka Ligi Kuu Italia kusimamishwa

**ROME,** Italia

RAIS wa chama cha wachezaji wa Italia, Damiano Tommasi, ametaka msimu wa soka nchini humo kusimamishwa baada ya miji kadhaa kaskazini mwa nchi hiyo kuripotiwa kufungwa.

Habari zinaeleza kwamba, mamlaka ya nchini Italia italifunga eneo la Lombardy ambalo linajumuisha majiji ya Milan na Bergamo, na miji mingine jirani 11 ikiwa ni sehemu ya serikali kupambana na kueneo kwa ugonjwa wa corona.

Katika hali hiyo, hakuna mtu atakayeruhusiwa kuondoka au kuingia kwenye maeneo hayo isipokuwa kwa wafanyakazi wa dharura.

Italia imeripotiwa kuwa na wagonjwa 5,061 wa ugonjwa wa corona ambao umeua watu 233 nchini humo.

Kusambaa kwa ugonjwa huo kumesababisha mechi zote kuchezwa bila mashabiki, huku milango ikiwa imefungwa hadi Aprili 3, mwaka huu.

Hata hivyo, kufungwa kwa miji hiyo kutazizuia timu kusafiri, na Tommasi ametaka msimu wa soka la nchini humo kufungwa kwanza.

Tommasi aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Tusimamishe Ligi! Tunahitaji kitu kingine chochote? Tusimamishe mpira wa miguu. Tujali kwanza afya."





# PIQUE AMTETEA KOCHA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique amemtetea kocha msaidizi wa Barcelona, Eder Sarabia, kwa kuwabwatukia wachezaji katika mchezo uliopita wa El Clasico na amesisitiza wachezaji walilipokea jambo hilo kwa hamasa.

Barca ilirudi kwenye ushindi baada ya kushinda 1-0 dhidi ya Real Sociedad Jumamosi, siku sita baada ya kutoka kufungwa na wapinzani wao kwenye Ligi ya Hispania, LaLiga, Real Madrid pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Kuelekea mchezo dhidi ya Sociedad, kocha Quique Setien alieleze kitendo cha kubwatuka kwa Sarabia dhidi ya wachezaji wake kwenye mchezo wa Clasico kama "cha kudhalilisha" na alimshauri msaidizi huyo kujaribu kutuliza hisia zake.

Setien pia alikiomba radhi kikosi hicho, lakini Pique amebainisha jambo hilo halikuwa na athari yoyote baada ya kucheza kwa dakika zote mchezo wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Sociedad juzi Jumamosi kwenye dimba la Camp Nou.

"Kocha msaidizi ana nafasi ya kuonyesha kile anachoona hakiendi sawa kama ilivyokuwa kule Bernabeu, lakini ni jambo la kawaida kabisa kwa upande wetu," alisema Pique baada ya penalti ya Lionel Messi kuipa ushindi huo Barca.

"Wachezaji wote tulijadiliana kwenye vyumba vya kubadilishia nguo. Bosi alituomba radhi na tulimwambia hakuna chochote kilichowaudhi wachezaji.

"Zaidi ni kwamba, tunapenda hali ile ya kuonyesha uimara na hilo linawafanya wachezaji kujua majukumu yao kwenye mchezo pia."

# *Tevez aipa ubingwa Boca Juniors*

**BUENOS AIRES,** Argentina

CARLOS Tevez aliisaidia Boca Juniors kutwaa taji la Ligi Kuu ya Argentina baada ya bao lake kuipa ushindi wa 1-0 dhidi ya Gimnasia ya Esgrima La Plata, Jumamosi.

Tevez alifunga bao hilo kwa shuti kali akiwa umbali wa yadi 20 katika dakika ya 72 pale kwenye dimba la La Bombonera na kuiwezesha Boca kuibuka na ushindi huo mwembamba dhidi ya timu hiyo inayonolewa na kocha Diego Maradona.

Inamaana kwamba, Boca ilimaliza ikiwa kileleni mwa msimamo kwa tofauti ya pointi moja na wapinzani wao wakuu wa soka la Argentina, River Plate ambao walitoka sare ya 1-1 dhidi ya Atletico Tucuman.

Ubingwa huo wa Boca ni wa 34 tangu kuanzishwa kwa klabu hiyo, na sasa wanakaribia kufikia rekodi ya River ambao wametwaa ubingwa huo mara 36.

Tevez hilo lilikuwa ni bao lake la 17 la ligi msimu huu, huku golikipa wa Gimnasia, Jorge Broun akishindwa kabisa kuzua shuti hilo.

Wao River walitoka nyuma na kupata sare dhidi ya Atletico Tucuman kwa bao lililofungwa na Matias Suarez, lakini walishindwa kuibuka na ushindi.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AMPIGIA SALUTI LACAZETTE

**Nina washambuliaji wawili kwa sasa ambao wanafanya maisha kuwa magumu kwa upande...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesifia mchango wa Alexandre Lacazette baada ya kutokea benchi na kuifungia Arsenal bao pekee lililowapa ushindi dhidi ya West Ham kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England, Jumamosi.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, Lacazette aliachwa benchi huku Eddie Nketiah akianza, ambapo ulikuwa mchezo wake watatu wa Ligi Kuu tangu kurudi kutoka kucheza kwa mkopo wa muda mfupi kule Leeds United.**

Huku mechi ikiwa bado haina mabao na muda ikielekea mwisho, Arteta alimwangalia Lacazette na alichukua nafasi ya Nketiah na mshambuliaji huyo wa zamani wa Lyon akawapa ushindi 'Washikabunduki' hao zikiwa zimesalia dakika 12 mchezo kumalizika.

Arteta alielezea uchaguzi wa Nketiah, lakini alieleza kukunwa na kiwango cha Lacazette licha ya kutoanza kwenye mchezo huo.

"Nina washambuliaji wawili kwa sasa ambao wanafanya maisha kuwa magumu kwa upande wangu, lakini kwa wakati huu ni vizuri sana," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Wote wanafunga, wote wapo kwenye nafasi nzuri. Niliamua kumchezesha Eddie ili kuleta presha kwa walinzi, lakini tulimhitaji Laca (Lacazette) kwenye dakika za mwisho.

"Alikuwa tayari kwa hilo. Niliona kwa haraka hali ile na nilimpa maelekezo."

Pierre-Emerick Aubameyang alianza kucheza tena winga ya kushoto, lakini Arteta alibainisha kwamba anamtumia mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon na Gabriel Martinelli kama washambuliaji wa pembeni kutokana na kutokuwa na chaguo jingine.

Wakati alipoulizwa anaona Aubameyang na Martinelli kama washambuliaji wa kati, Arteta alisema: "Ndio, lakini kutokana na uwiano wa kikosi chetu kwa sasa nalazimika kuwachezesha kwenye nafasi nyingine kama kushoto. Hatuna wachezaji watano kwa sababu kuna mmoja namtumia kucheza kama beki wa kushoto wakati yeye si beki wa kushoto.

"Hivyo, tunajaribu kwenda na hali jinsi ilivyo. Tunajaribu kuwaweka wachezaji ambao ni wakali kwenye goli, na hilo linaweza kuwa na mafanikio kwa timu na hiyo ni sehemu ya kuwatengeneza wachezaji tulionao."

Usajili wa Januari, Pablo Mari alianza katika mechi yake ya pili mfululizo bila kuruhusu bao, na Arteta alionyesha kufurahishwa naye kwa kuzoea haraka ligi hiyo."

## ZISIKUPITE

### CITY KUMFUNGULIA AGUERO

KLABU ya Manchester City ipo tayari kumruhusu mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 31, kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto kama wakishindwa katika rufani yao ya kufungiwa kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sun on Sunday)***

### YAMNYATIA HENDERSON

CHELSEA inamwania golikipa wa Sheffield United, Dean Henderson mwenye miaka 22, ambaye anacheza kwa mkopo kutoka Manchester United, kama suluhisho la matatizo yao ya makipa. ***(Star on Sunday)***

### AUBAMEYANG ATAJWA INTER

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang ametajwa kuwa yupo kwenye rada za Inter Milan na kwamba wanataka kumsajili raia huyo wa Gabon mwenye umri wa miaka 30 katika kipindi cha majira ya joto. ***(Calciomercato)***

### GUARDIOLA KUMTWAA SKRINIAR

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anajiandaa kutumia kiasi cha pauni milioni 80 ili kumsajili mlinzi wa Inter Milan, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25 raia wa Slovakia, ili kumaliza matatizo ya ulinzi kwa timu yake. ***(Sunday Express)***

### ABRAHAM AIGOMEA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 22, amekataa ofa ya kuongezewa mkataba na Chelsea na kwamba kwa sasa anataka kuondoka na kwenda kwenye klabu zenye majina makubwa. ***(Sunday Mirror)***

### MATIC KUFUNGWA TENA UTD

KIUNGO wa kimataifa wa Serbia, Nemanja Matic mwenye umri wa miaka 31, anatarajia kusaini mkataba mpya kabla ya mwishoni mwa msimu huu ili kuendelea kuichezea Manchester United. ***(Manchester Evening)***

### AMTAKA STONES WA CITY

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anajipanga kumsajili beki wa Manchester City na timu ya Taifa ya England, John Stones mwenye umri wa miaka 25, kuelekea dirisha la kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Team Talk)***

### AILAUMU JUVE KUMTOSA

NYOTA wa zamani wa Juventus na kocha wa sasa wa Real Madrid, Zinedine Zidane amedai hakupewa kipaumbele na klabu hiyo ya Turin ili arudi kama kocha, lakini amesema hana uhakika wa kuendelea kuwa kocha pale Santiago Barnabeu. ***(Goal.com)***

### INTER YAMWANIA VERTONGHEN

KLABU ya Inter Milan, inawania kumsajili mlinzi wa Tottenham Hotspur, Jan Vertonghen mwenye umri wa miaka 32 raia wa Ubelgiji, kwa uhamisho huru wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(SempreInter)***

### MKHITARYAN KURUDI ARSENAL

MIKEL Arteta amedokeza kwamba, kiungo wa kimataifa wa Armenia, Henrikh Mkhitaryan mwenye umri wa miaka 31, ambaye anacheza kwa mkopo kule AS Roma, bado ana nafasi ndani ya Arsenal. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

## Madundo, Mzee Ole watimuliwa kuinoa Chuoni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Chuoni FC inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, imeachana na kocha wao mkuu, Ramadhani Abdulrahman 'Madundo' pamoja na msaidizi wake, Suleiman Hamid 'Mzee Ole' kwa madai ya mwenendo wa matokeo mabaya ya timu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Mattar Mohmed alisema timu yake kwa mechi za hivi karibuni imekuwa ikipata matokeo mabaya hali iliyosababisha kuchukua maamuzi ya kuachana na makocha hao.

Alisema katika michezo tisa waliyocheza ya mzunguko wa pili, wamefanikiwa kushinda michezo miwili tu, matokeo ambayo kwa upande hayajawaridhisha viongozi wa timu hiyo na hata mashabiki wao.

Mohmed alisema timu hiyo kwa sasa ipo katika mchakato wa kumtafuta mwalimu mpya atakayekinoa kikosi hicho wakati ligi hiyo ikielekea ukingoni ili waweze kufanya vizuri michezo iliyobaki.

Aidha, alisema katika mchezo wao wa leo dhidi ya Zimamoto utakaochezwa katika Uwanja wa Amaan, jukumu la mwalimu litakuwa la kocha wa timu B ya Chuoni, Hassan Juma Haji hadi timu hiyo itakapomtangaza kocha mpya.

# AZAM FC YAWAFUNGA WATATU MIAKA 3

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umesema sababu ya kuwaongezea mikataba ya miaka mitatu nyota wake watatu, mabeki Lusajo Mwaikenda na Oscar Masai pamoja na mshambuliaji Andrew Simchimba, ni ili kuendeleza vipaji vyao lakini kutekeleza maombi ya benchi la ufundi.

**Nyota hao wataitumikia timu hiyo kwa mkataba wa miaka mitatu kila mmoja, hivyo watadumu hapo dimba la Chamazi hadi mwaka 2023.**

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema benchi la ufundi lilipendekeza wachezaji hao kuongezewa mikataba baada ya uhitaji wa huduma zao.

Alisema wanaimani na nyota hao kutokana na umri wao kuruhusu kucheza mpira kwa muda mrefu huku wakionekana kuwa msaada kwa kutimu hapo baadaye.

"Ni wachezaji wazuri, lakini umri wao unaruhusu kucheza soka kwa muda mrefu na kuisaidia timu yetu kwa sasa na hapo baadaye," alisema Popat.

GOFU...




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Abdi Mohamed, akikabidhi mfuko wenye baadhi ya vifaa vya mchezo wa gofu pamoja na nyaraka muhimu za safari kwa mcheza gofu maarufu nchini, Victor Mbunda (kushoto), anayetarajia kushiriki mashindano ya wazi ya gofu yanayotarajiwa kufanyika katika Viwanja vya Karen mjini Nairobi, Kenya katika tarehe itakayotangazwa baadaye na waandaaji wa mashindano hayo. Absa inamdhamini Mbunda kwa gharama zote za ushiriki wake. Kulia ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano wa Absa Tanzania, Aron Luhanga na kushoto kwa Mbunda ni wacheza gofu wakongwe, Martin Warioba na Marian Mugo waliomsindikiza. Hafla ya makabidhiano hayo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Minziro alia ratiba wakiifuata Prisons*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupoteza michezo mitatu za ugenini, Kocha Mkuu wa Alliance FC, Felix Minziro, amesema kucheza mechi mfululizo kimekuwa chanzo cha matokeo hayo mabaya.

Alliance juzi ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa ni baada ya kuchapwa na Yanga na Ruvu Shooting.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Minziro alisema hawezi kuwalaumu wachezaji wake kupoteza mchezo huo kutokana na ukweli kwamba wamejituma ila kupata matokeo haikuwa bahati yao.

Alisema suala la matokeo ni bahati, na kwamba changamoto ya ratiba kwa kucheza mechi kubwa karibu pia kumechangia kutopata matokeo mabaya.

"Nina imani kwa mechi zetu zijazo tutapambana kupata matokeo mazuri, nitahakikisha napanga kikosi kuendana na mbanano wa ratiba ya ligi," alisema.

Minziro alisema kwa sasa wanahitaji kufanya vizuri katika michezo yao bila ya kuangalia wanacheza ugenini au nyumbani.

Alliance ambayo ipo katika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kushuka dimbani mara 27 na kuvuna pointi 29, keshokutwa Jumatano itashuka katika dimba la Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya kuvaana na Tanzania Prisons yenye alama 37 zinazoifanya ishike nafasi ya 11.

## Mwadui walia na washambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupata matokeo mazuri wikiendi iliyopita, uongozi wa timu ya Mwadui FC bado unalia na safu yake ya ushambuliaji.

Akizungumza na Nipashe jana, akiwa njiani kuelekea mkoani Dodoma, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Khaleed Adam alikiri kuwapo kwa upungufu wa kucheka na nyavu katika safu yake ya ushambuliaji.

"Japokuwa hatujapoteza mchezo wetu [dhidi ya Mbeya City), safu hiyo ina upungufu mdogo ambao ninaendelea kufanyia kazi," alisema Khaleed.

Akizungumzia mchezo huo uliopita dhidi ya Mbeya City ambao waliibuka na ushindi wa bao 1-0, alisema ulikuwa mgumu licha ya kushinda.

Alisema anaomba morali iliyopo katika timu yake iendelee huku akiomba ushirikiano kwa mashabiki wao katika mchezo wao wa kesho ugenini dhidi ya JKT Tanzania, utakaochezwa katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunashinda katika mchezo huo na kurudi na pointi tatu nyumbani," alisema.

# Michezo

Jumatatu Machi 9, 2020
Nipashe



Arteta ampigia saluti Lacazette UKURASA 30



Bernard Morrison (kushoto) akishangilia na wenzake baada ya kufunga bao.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# WAMEGONGWA

## Simba yaweka rekodi ya kujaza uwanja na kutobolewa mbele Rais Magufuli, Rais CAF akishuhudia...

**Na Somoe Ng'itu**

GUNDU la kupokea kichapo mbele ya Rais John Magufuli limeendelea kuiandama Simba baada ya kukubali kupoteza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga katika mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Ushindi huo mbali na kuwapa pointi tatu muhimu, wachezaji wa Yanga watapata kitita cha milioni 200 kutoka kwa mdhamini wao, GSM ambao waliahidi kuwapatia kiasi hicho cha fedha endapo watashinda mechi hiyo.**

Kwa matokeo hayo, Yanga iliyocheza mechi mbili pungufu, imefikisha pointi 50 na kubakia kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo, huku Simba iliyoko kileleni ikibaki na pointi zake 68 wakati Azam FC yenye pointi 51 iko katika nafasi ya pili.

Mbali na Magufuli ambaye jana alivaa jezi yenye mchanganyiko wa rangi ya Simba na Yanga pamoja na jaketi la rangi za bendera ya Taifa, mchezo huo ulihudhuriwa pia na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad.

Licha ya kutwaa ubingwa wa msimu uliopita, Simba ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Kagera Sugar mechi ambayo ilikuwa ya kukabidhiwa kombe la ubingwa na kiongozi huyo mkuu wa nchi huku jana ikipoteza mechi yake ya tatu msimu huu, hivyo hii ni mara ya pili kupoteza mbele ya Rais Magufuli.

Bernard Morrison aliipatia Yanga bao la kwanza dakika ya 44 baada ya kupiga faulo iliyokwenda moja kwa moja wavuni huku akimwacha kipa wa Simba, Aishi Manula akikosa la kufanya.

Refa Martin Saanya kutoka Morogoro alitoa adhabu hiyo baada ya Morrison kufanyiwa madhambi ya kiungo wa muda mrefu wa Simba, Jonas Mkude kumchezea Morrison madhambi nje kidogo ya eneo la 18.

Yanga ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa bao hilo pekee lililofungwa na mshambuliaji wake kutoka Ghana na kuwafanya Simba na mashabiki wake kubaki wanyonge kutokana na kuwa nyuma.

Hata hivyo, mechi hiyo iliyokuwa ya kasi na timu zote zikishambuliana kwa zamu, Simba ilikaribia kupata bao dakika ya sita baada ya Kipa wa Yanga, Metacha Mnacha kuokoa hatari iliyoanzia kwa Clatous Chama huku nahodha John Bocco akichelewa kuunganisha krosi hiyo.

Dakika ya 10 Yanga walijibu shambulio hilo, lakini Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr' aliwahi kuokoa mpira baada ya beki mwenzake Erasto Nyoni kuteleza jirani na lango lao huku Morrison akiwa jirani kumalizia hatari hiyo na dakika iliyofuata Ditram Nchimbi akipoteza nafasi kwa kupiga nje na kuinyima timu yake nafasi ya kufunga mapema.

Nchimbi alikaribia tena kufunga bao baada ya kumalizia kazi nzuri iliyofanywa na Haruna Niyonzima lakini Manula aliwahi kudaka hatari hiyo ikiwa ni dakika ya 14 wakati Said Makapu naye akiwahi kuokoa shuti la Meddie Kagere dakika ya 25.

Simba itajilaumu zaidi kwa kupoteza nafasi ya kufunga baada ya Metacha kupangua mara mbili mipira iliyopigwa na Chama na Bocco na baadaye kuokolewa na mabeki wake dakika ya 29 na dakika 10 baadaye Luis Miquissone akikosa tena nafasi ya kufunga kwa kugongesha mwamba.

Yanga ilikaribia tena kupata bao dakika ya 62, lakini Nchimbi alichelewa kuunganisha krosi iliyopigwa na Mapinduzi Balama huku dk 73 Metacha akidaka mpira uliopigwa na Bocco, lakini hata hivyo mwamuzi namba mbili Frank Komba alisema ameshaotea mshambuliaji huyo.

Deus Kaseke alikaribia kuifungia Yanga bao dakika ya 88, lakini shuti lake liligonga mwamba huku Kennedy Juma naye akipiga pembeni na kupoteza nafasi kwa vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kusawazisha dakika moja baadaye.

Yanga ambayo imekoleza mbio za ubingwa, sasa itakuwa imevuna pointi nne kutoka kwa watani zao Simba baada ya mchezo wa mzunguko wa kwanza kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Simba; Aishi Manula, Shomari Kapombe, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Erasto Nyoni/ Kennedy Juma (22), Pascal Wawa, Jonas Mkude, Luis Miquissone, Clatous Chama, Meddie Kagere/ Hassan Dilunga (70), John Bocco na Francis Kahata/ Deo Kanda (dk 61).

Yanga; Metacha Mnata, Juma Abdul, Jaffar Mohammed, Lamine Moro, Said Makapu, Feisal Salum 'Feitoto'/ Kelvin Yondani ( dk 89), Papy Tshishimbi, Haruna Niyonzima, Bernard Morrison/ Patrick Sibomana (56), Ditram Nchimbi na Mapinduzi Balama/ Deus Kaseke (86).

### SIMBA YOSSO YATAKATA

Kikosi cha timu ya vijana cha Simba chini ya umri wa miaka 17 kilipata ushindi wa mabao 2-0, katika mechi ya mapema jana mchana.

Mabao yote ya timu hiyo inayofundishwa na Kocha Nico Kiondo, yalifungwa katika kipindi cha pili, ambacho yosso hao wa Wekundu wa Msimbazi walimaliza pungufu baada ya mchezaji wao mmoja kuonyeshwa kadi nyekundu.

### SIMBA YATANGULIA

Saa 10:07, wachezaji wa Simba ndio walikuwa wa kwanza kuingia uwanjani kwa ajili ya kupasha miili kuwa tayari na mtanange huo.

Kikosi hicho cha vinara kiliongozwa na kiungo wake, Jonas Mkude. Saa 10:09 jioni, wachezaji wa Yanga nao waliingia uwanjani kupasha.

Katika hali ya kuonyesha kushangaa, mshambuliaji wa Yanga, Morrison ambaye hii ni 'dabi' yake ya kwanza alionyesha ishara ya kushangaza umati wa mashabiki kwa kuangalia majukwaa yote mawili na baadaye kuingia uwanjani.

Simba yaendelea kufunika uwanja kwa kuingiza idadi kubwa ukilinganisha na watani zao ambao ndio wenyeji wa mchezo huo wa mzunguko wa pili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >